# Mwongozo wa Mfumo wa Haki za Binadamu wa Afrika

**Maadhimisho ya Miaka 40 Tangu Kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu**

1981 – 2021

**Mwongozo wa Mfumo wa Haki za Binadamu Afrika**

1981 – 2021

**PULP**

Mwongozo huu unachukuliwa kama ni utangulizi unaopatikana na wenye taarifa nyingi za mfumo wa haki za binadamu ulioanzishwa na Umoja wa Afrika. Mwongozo huu unatoa muhtasari wa maendeleo yanayohusu Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, chombo chake cha usimamizi, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, na Mkataba wa Haki na Ustawi wa Mtoto na chombo chake cha usimamizi, Kamati ya Afrika ya Wataalam wa Haki na Ustawi wa Mtoto. Toleo hili la Mwongozo lilizinduliwa tarehe 27 Juni 1981, kwa kuadhimisha miaka 40 iliyopita, ambapo Mkataba wa Afrika ulipitishwa. Pia, mwaka 2021 ni mwaka wa 15 tangu Mahakama ya Afrika ianze kufanya kazi.

Mwongozo unalenga kuonyesha matukio muhimu ya maendeleo ya kihistoria na kutoa utangulizi wa mfumo wa Afrika wa haki za binadamu, unaopatikana na unaoendelea kurejewa kila wakati. Mwongozo umeandaliwa na Kituo cha Haki za Binadamu, Kitivo cha Sheria, Chuo Kikuu cha Pretoria kikishirikiana na Tume ya Afrika. Matoleo mawili ya Mwongozo yalitolewa mwaka 2011 na 2017.

Kituo cha Haki za Binadamu, ambacho mwaka 2021 kinasheherekea miaka 35 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1986, ni idara ya kitaaluma na pia ni Shirika Lisilo la Kiserikali. Kituo kina hadhi ya uangalizi katika Tume ya Afrika. Kituo kinatoa programu za kitaaluma na kinashiriki katika utafiti, utetezi na mafunzo ya haki za binadamu, kikilenga zaidi Afrika. Progamu zake kuu ni Shahada ya Umahiri katika Haki za Binadamu na Demokrasia katika Afrika na Mashindano ya Mahakama ya Afrika Haki za Binadamu ya Mfano. Kwa taarifa zaidi kuhusu Kituo cha Haki za Binadamu, tembelea www.chr.up.ac.za

Mwongozo huu pia unapatikana katika mfumo wa wazi wa kielektroniki:
www.pulp.up.ac.za

Pretoria University Law Press
PULP
www.pulp.up.ac.za

ISBN: 978-1-991213-04-4
9 781991 213044

# MWONGOZO WA MFUMO WA HAKI ZA BINADAMU WA AFRIKA

***Maadhimisho ya Miaka 40 Tangu Kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu***

***1981 - 2021***

35 1986 2021 Centre for Human Rights UNIVERSITY OF PRETORIA

HAKI ZA BINADAMU ACHPR WAJUIBU WETU SOTE

**Pretoria University Law Press**

**PULP**

2021

***Mwongozo wa Mfumo wa Haki za Binadamu Afrika - Maadhimisho ya Miaka 40 Tangu Kukubalika kwa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu 1981-2021***

**Umechapishwa na:**

Pretoria University Law Press (PULP) ni mchapishaji katika Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Pretoria, Afrika Kusini. PULP inakusudia kuchapisha na kuwezesha upatikanaji wa maandiko ya wasomi yenye ubunifu, wa kiwango cha hali ya juu kuhusu sheria katika Afrika. Pia PULP inachapisha matoleo endelevu ya nyaraka za sheria kuhusiana na sheria ya masuala ya umma katika Afrika, pamoja na vitabu vya kiada kutoka nchi za Kiafrika tofauti na Afrika Kusini.

Kitabu hiki kilipitiwa na wanataaluma kabla ya kuchapishwa.

Kwa maelezo zaidi kuhusu PULP, tembelea www.pulp.up.ac.za

**Kimechapwa na kujalidiwa na:**

Pinetown Printers, Afrika Kusini

**Kuagiza, wasiliana na:**

PULP
Faculty of Law
University of Pretoria
South Africa
0002
pulp@up.ac.za
www.pulp.up.ac.za

**Jalada limebuniwa na:**

Yolanda Booyzen

Mwongozo huu umeandaliwa na Kituo cha Haki za Binadamu, Kitivo cha Sheria, Chuo Kikuu cha Pretoria kwa kushirikiana na Tume ya Afrika.

**ISBN:** 978-1-991213-04-4

# Yaliyomo

Orodha ya Vifupisho iv

Sababu ya Kusheherekea v

A. Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Viwango Vya Ziada 1

B. Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu 15

C. Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu 56

D. Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto 74

E. Kamati ya Afrika ya Wataalam wa Haki na Ustawi wa Mtoto 80

Bibliografia 103

MIAKA AROBAINI YA MKATABA WA AFRIKA

# Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| ACHPR | Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu |
| AHRLR | Sheria za Afrika za Haki za Binadamu |
| AHSG | Mkutano wa Viongozi wa Kitaifa na Serikali |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| AU | Umoja wa Afrika |
| CAL | Muungano wa Wasagaji Afrika |
| CEDAW | Mkataba wa Kukomesha Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake |
| FGM | Ukeketaji wa Wanawake |
| IDP | Watu Waliolazimika Kuhama Makazi Ndani ya Nchini |
| LDA | Sheria ya Uzuizi wa Wagonjwa wa Afya ya Akili |
| LGBTI | Msagaji, Shoga, Mpenda jinsi zote mbili na Huntha |
| NGOs | Mashirika Yasiyo Ya Kiserikali |
| NHRI | Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu |
| OAU | Umoja wa Nchi Huru za Afrika |
| PLHIV | Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika |
| SERAC | Kituo cha Kuendeleza Haki za Kiuchumi na Kijamii |
| UN | Umoja wa Mataifa |
| VVU | Virusi vya UKIMWI |

# Sababu ya Kusheherekea

Mwaka 2021 ni mwaka wa kusheherekea, licha ya mazingira magumu yaliyoletwa na ugonjwa wa UVIKO 19.

Katika mwaka 2021, ni miaka 40 tangu Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika upitishe Mkataba wa Haki za Binadamu na Watu wa Afrika mnamo tarehe 27 Juni 1981, Nairobi, nchini Kenya.

Kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika huwakilisha kupunguzwa kwa kasi ya kanuni ya 'kutoingilia masuala ya ndani ya nchi' kanuni ambayo ilikuwa nguzo ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrka wa mwaka 1963. Wachambuzi wengi wanaona kuandikwa na kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika ni itiko la Afrika kwa ukiukwaji wa haki za binadamu katika miaka ya 1970 katika nchi za Uganda, Guinea Ikweta na Dola ya Afrika ya Kati na kusita kwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika kukosoa viongozi wa mataifa haya au kuingilia kati kwa njia nyingine yoyote. Wakuu wa nchi hizo tatu waliokuwa madarakani walipoteza madaraka mwaka 1979. Wakati huo huo wimbi la pili la Demokrasia lilifika Afrika, Ghana ikiwa mfano (ambapo mwaka 1979 jeshi lilikubali uwepo wa Demokrasia kamili) na Nigeria (ambapo mwaka 1979 Rais Obasanjo alikabidhi madaraka kwa Serikali iliyochaguliwa kidemokrasia, kuanzisha mchakato ambao uliisha kwa kupitishwa kwa Katiba ya mwaka 1979). Kutokana na hali hii, viongozi wa Afrika waliweka Mkataba huo kama kinga dhidi ya kutokea tena kwa ukatili kama huo na njia ya kuhakikisha kuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika hautaacha tena kuchukua hatua wakati wa ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu katika nchi ambazo ni wanachama wake.

Wakati Mkataba umepitishwa miaka 40 iliyopita, mwaka 2021 tuliadhimisha miaka 35 tangu kuanza kutumika. Imechukua zaidi ya miaka mitano kupata idadi ya kura zinazotakiwa kutoka kwa wanachama wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika ili kuwa sehemu ya Mkataba huo na kufungwa na masharti yaliyopo chini ya Mkataba wa Afrika. Kwa sasa, kuna nchi moja tu katika wanachama wa Umoja wa Afrika ambayo haijaridhia Mkataba wa Afrika ambao

umeridhiwa na u na nchi nyingi zaidi katika bara la Afrika. Mkataba wa Afrika ulianza kutumika mnamo tarehe 21 Oktoba 1986 na inaelezwa kuwa ni hatua muhimu kwasababu inatuelekeza katika ahadi ya wanachama isiyotimizwa ya kutekelezwa kwa masharti ya Mkataba katika Sheria za nchi zao na desturi.

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na watu pia inaadhimisha wakati muhimu katika ukuaji wake. Imepita miaka kumi na tano tangu kuteuliwa kwa majaji kwa mara ya kwanza mwaka 2006 na mahakama kuanza kufanya kazi. Tangu kipindi hicho, Mahakama imetoa maamuzi madhubuti.

Kwetu sisi Kituo cha Haki za Binadamu, mwaka huu umekua na umuhimu zaidi sababu tunasheherekea miaka 35 ya kuanzishwa kwetu. Kwa namna tofauti, kituo kimekua sambamba pamoja na mfumo wa haki za binadamu wa bara la Afrika. Kwa miaka hii, tumepewa heshima ya kushirikiana na kuchukua jukumu katika nyanja mbalimbali zinazohusiana na taasisi tatu zinazounda mfumo. Kituo kinafurahia kuwa na hadhi ya uangalizi katika Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Kamati ya Wataalam ya Afrika Kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto. Imekuwa ikiunga mkono nyanja za mamlaka ya mifumo maalum ya Tume ya Afrika, hususan Katibu Maalum wa Haki za Wanawake barani Afrika (kwa kutengeneza miongozo chini ya Itifaki ya Mkataba wa Afrika kuhusu ya Haki za Wanawake barani Afrika, na Maoni ya Jumla) na Katibu Maalum wa Haki ya Uhuru wa Kujieleza na Upatikanaji wa Taarifa katika Afrika (kupitia utengenezaji wa Sheria ya Mfano kuhusu Upatikanaji wa taarifa katika bara la Afrika).

Tangu mwaka 1992, kila mwaka Kituo cha Haki za Binadamu kwa Ushirikiano na chuo kikuu mwenyeji, katika nchi mbalimbali barani Afrika huandaa Mashindano ya Mahakama ya Mfano za Haki za Binadamu za Afrika. Timu za wanafunzi hubishana kwa hoja katika mashauri ya kinadharia mbele ya jopo la wahadhiri wa sheria na wataalam wa haki za binadamu kana kwamba wapo mbele ya Mahakama halisi ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Mwaka huu mashindano haya yameadhimisha miaka thelathini.

Mwongozo huu ni mfano wa shauku yetu na imani ya kudumu katika kuthamini haki za binadamu katika bara la Afrika. Pia inaashiria shukrani zetu kwa uhusiano wa ushirikiano ambao tumefurahia na taasisi hizi tatu. Tunaamini itakua ni nyenzo kwa ajili ya uelewa mkubwa, tathmini na matumizi ya mfumo wa haki barani Afrika.

Huu ni uhuishwaji wa tatu wa Mwongozo huu, ambao ulionekana mara ya kwanza kwenye hafla ya sherehe ya miaka 30 ya kupitishwa kwa Mkataba, mnamo mwaka 2011, ni miaka 10 iliyopita sasa. Mwongozo huu uliohuishwa, kurekebishwa na kufafanuliwa umewezeshwa na michango ya Trésor Makunya Muhindo, Mratibu wa Machapisho katika Kituo pamoja na wanafunzi wa shahada ya umahiri/uzamili katika programu ya Haki za Binadamu na demokrasia katika Afrika (Olum Lornah Afoyomungu, Ruddy Fualefeh Morfaw Azanu na Davina Murden). Kituo kinatambua michango yao pamoja na wengine waliochangia katika matoleo yaliyopita.

Lizette Hermann, Meneja wa Machapisho PULP, ndiye aliyehusika na mpangilio unaovutia na wenye kufaa kazi.

Frans Viljoen
Director, Centre for Human Rights, University of Pretoria
Pretoria

**Mwaka 2021 ni kilele muhimu cha kihistoria katika mfumo wa haki za binadamu Afrika kwa kuwa unaadhimisha kumbukumbu ya miaka 40 ya kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika na kumbukumbu ya miaka 15 ya utendaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.**

**Maoni kuhusu Mahakama ya Afrika, Tume na maamuzi ya Kamati yanaweza kupatikana katika Kitabu cha African Human Rights Year Book, juzuu ya hivi karibuni (Juzuu ya 4) imechapishwa mwaka 2020.**
**Juzuu zote zinaweza kupatikana https://www.ahry.up.ac.za**

# A. Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Viwango Vya Ziada

## Historia

Wazo la kuandaa nyaraka ya kuanzisha mfumo wa wa kulinda haki za binadamu barani Afrika lilifikiriwa kwa mara ya kwanza mapema miaka ya 1960. Katika Kongamano la kwanza la Wanasheria wa Kiafrika, lililofanyika Lagos, Nigeria, mnamo mwaka 1961, wajumbe walipitisha tamko linalojulikana kama 'Sheria ya Lagos' wakitoa wito serikali za Kiafrika kupitisha Mkataba wa Afrika kuhusu haki za binadamu ulio na Mahakama na Tume. Hata hivyo kwa kipindi hicho Serikali za nchi za Afrika hawakuchukua hatua stahiki za kutekeleza wazo hili.

Mkataba wa mwaka 1963 ulioanzisha Umoja wa Nchi Huru za Afrika haukuweka wazi wajibu wa kulinda haki za binadamu kwa wanachama. Mkataba wa kuanzisha Umoja wa Nchi Huru za Afrika uliwataka wanachama kuheshimu haki za binadamu zilizoainishwa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu katika mahusiano ya kimataifa. Licha ya kukosa mamlaka ya kushughulikia masuala haki za binadamu, Umoja wa Nchi Huru za Afrika ulichukua hatua thabiti kushughulikia masuala kadhaa ya haki za binadamu kama vile kuondoa ukoloni, ubaguzi wa rangi, utunzaji wa mazingira na tatizo la wakimbizi. Hata hivyo, Umoja wa Nchi Huru za Afrika haukutiilia maanani ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu uliofanywa na baadhi ya viongozi wa Afrika waliotawala kimabavu dhidi ya raia wao. Kwa kiasi kikubwa hii ilisababishwa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika kutoa kipaumbele katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi na usimamiaji madhubuti wa kanuni ya uhuru wa nchi na kutokuingilia masuala ya ndani ya nchi wanachama.

Katika kikao cha kwanza cha Wanasheria wa Nchi Zinazozungumza Kifaransa kilichofanyika Dakar, Senegal, mwaka 1967, washiriki walifufua tena wazo la Sheria ya Lagos kuhusu umuhimu ya kulinda haki za binadamu barani Afrika. Katika Tamko la Dakar lililopitishwa baada ya mkutano, washiriki waliiomba Tume ya Kimataifa ya Wanasheria kwa kushauriana na taasisi zingine katika bara la Afrika kuangalia uwezekano wa kuanzisha mfumo

wa haki za binadamu wa Afrika.

Umoja wa Mataifa pia uliwezesha mfululizo wa semina na mikutano katika nchi kadhaa za Afrika. Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa iliunda kikosikazi maalum na kupitisha azimio linalomtaka Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kutoa msaada muhimu kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa kikanda wa haki za binadamu wa Afrika. Hata hivyo, majaribio ya kupata ridhaa ya nchi za Afrika kupitisha Mkataba wa Kikanda wa Haki za Binadamu hayakufanikiwa. Katika moja ya mikutano, washiriki waliamua kuunda kamati ya ufuatiliaji iliyopewa mamlaka ya kukutana na Viongozi wakuu wa chi za Afrika na taasisi zingine muhimu kujadili umuhimu/haja ya kuwa na mfumo wa kikanda wa haki za binadamu wa Afrika. Kufuatia ziara ya kamati nchini Senegal, Rais wa kipindi hicho, Léopold Sédar Senghor, aliahidi kuwasilisha pendekezo katika kikao kinachofuata cha Mkutano wa wakuu wa nchi wanachama Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Katika kikao kilichofanyika Monrovia, Liberia mwaka 1979 kwa kauli moja baraza lilimuomba Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi huru za Afrika kuitisha kamati ya wataalam kuandaa Mkataba wa Kanda ya Afrika wa Haki za Binadamu unaofanana na Mikataba ya Haki za Binadamu ya Ulaya na Amerika.



Kéba M'baye
(1924-2007)



Léopold Sédar Senghor
(1906-2001)

Mwaka 1979, mkutano wa wataalam ishirini kutoka bara la Afrika uliandaliwa Dakar, Senegal na uliongozwa Jaji Kéba M'baye (kushoto). Kwa kiasi kikubwa kazi ya Kamati ya Wataalam ulishawishiwa na hotuba ya ufunguzi ya Rais Senghor (kulia) ambaye aliielekeza Kamati kupata msukumo kutoka katika maadili na mila za kiafrika na pia kuzingatia mahitaji halisi ya waafrika, haki ya maendeleo na wajibu wa watu. Katika kipindi ambacho Afrika imesambaratika, kukiwa na baadhi wa wakuu wa nchi waliozoea desturi ya kutawala kimabavu ambayo itadhoofishwa na mkataba wa haki za binadamu mchango wa Rais Senghor ulihamasisha kuandaliwa na hatimaye kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika.

Takribani siku 10 tangu kutolewa kwa uamuzi katika Mkutano wa Dakar, Kamati iliandaa rasimu ya awali ya Mkataba. Kutokana na Serikali kadhaa za Afrika kupinga ulinzi wa haki za binadamu katika kanda ya Afrika, mkutano wa wajumbe wenye mamlaka kamili ulipangwa kufanyika Ethiopia kupitisha rasimu ya mkataba haukuweza kufanyika. Kipindi hiki kilikua ni kipindi cha kushangaza zaidi katika historia ya uandishi wa Mkataba. Ni wazi mpango wa kuandaa Mkataba ulikua katika hatari. Katika kipindi hiki cha mazingira ya shida na katika mualiko wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi huru za Afrika, Rais wa Gambia aliitisha mikutano miwili ya mawaziri, Banjul, Gambia ambapo rasimu ya Mkataba ilimaliziwa na kisha kuwasilishwa katika Mkutano wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Ni kwa jukumu hili la kihistoria la Gambia, Mkataba wa Afrika hutambulika kama Mkataba wa Banjul.

Hatimaye Mkutano wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika ulipitisha Mkataba wa Banjul mnamo tarehe 27 Juni 1981, Nairobi Kenya. Baada ya kuridhiwa na zaidi ya nusu ya nchi wanachama wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika, Mkataba ulianza kutumika mnamo tarehe 21 Oktoba 1986. Katika mikataba yote ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika/ Umoja wa Afrika, Mkataba wa Afrika ni miongoni mwa mikataba iliyoridhiwa zaidi na nchi wanachama. Kufikia mwaka 1999, Mkataba wa Afrika ulikua umeridhiwa na nchi zote wanachama. Taifa jipya la Sudani ya Kusini liliwasilisha hati yake kuridhia mwaka 2016. Mpaka kufikia Juni 2021, ni nchi ya Moroko tu ndiyo haijaridhia Mkataba wa Afrika. Kipindi inajitoa uanachama kutoka Umoja wa Nchi Huru za Afrika, mwaka 1984 ilikua haijaridhia Mkataba wa Afrika. Tangu kujiunga kwake tena na Umoja wa Afrika mwaka 2017 bado haijaridhia Mkataba wa Afrika kwasababu ya kupinga kwake uhuru wa kujitawala ya Watu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi.

## Nchi Zilizoridhia Mkataba wa Afrika



(Nchi 54 zilizoridhia Mkataba wa Afrika zimeonyeshwa kwa kutumia rangi za zambarau)

# Tarehe Muhimu

| | |
|---|---|
| 27 Juni 1981 | Kupitishwa kwa Mkataba Nairobi, Kenya |
| 21 Oktoba 1981 | Kuridhiwa kwa Mkataba wa Afrika kwa mara ya kwanza (Mali) |
| 21 Oktoba 1986 | Mkataba kuanza kutumika |
| 2 Novemba 1987 | Kuanza kwa kikao cha Kwanza cha Kawaida cha Tume |
| 2 Novemba 1987 | Kupitishwa kwa Azimio la Kwanza, kuhusu Makao Makuu ya Tume |
| 28 Aprili 1988 | Kupitishwa kwa Taarifa ya Kwanza Shughuli za Tume |
| 28 Aprili 1988 | Uzinduzi wa Makao Makuu ya Tume Banjul, Gambia |
| 12 Juni 1989 | Tume kupitisha 21 Oktoba kuwa Siku ya Haki za Binadamu |
| 21 Oktoba 1989 | Kikao cha Kwanza Dharura cha Tume |
| 3-14 Juni 1989 | Kupitishwa kwa Itifaki kuhusu Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika |
| 10 Juni 1998 | Kupitishwa kwa Itifaki ya Maputo |
| 11 Julai 2003 | Kuanza kutumika kwa Itifaki ya Mahakama ya Afrika |
| 25 Januari 2004 | Kuanza kutumika kwa Itifaki ya Maputo |
| 25 Novemba2005 | Kuapishwa kwa Majaji wa Mwanzo wa Mahakama ya Afrika |
| 2 Julai 2006 | Kuanza kazi rasmi kwa Mahakama, Addis Ababa |
| 14 Juni 2013 | Uamuzi wa kwanza wa msingi wa shauri (*Mchungaji Christopher R. Mtikila dhidi ya Tanzania*) |
| 31 Januari 2016 | Kupitishwa kwa Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wazee |
| 29 Januari 2018 | Kupitishwa kwa Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu Afrika |

## Sifa kuu za Mkataba wa Afrika

Mkataba una sifa za kipekee zifuatazo:

- Mkataba unatambua kutokugawanyika kwa haki zote: Vizazi vyote vya haki vimetambuliwa. Haki za kijamii na uchumi zinaweza kudaiwa mahakamani.

> 'Ni wazi haki za pamoja, haki za mazingira na uchumi na haki za kijamii ni masuala muhimu ya haki za binadamu Afrika. Tume ya Afrika inatumia haki mbalimbali zilizomo katika Mkataba wa Afrika. Inatumia fursa hii kubainisha wazi kwamba hakuna haki iliyomo katika Mkataba wa Afrika ambayo haiwezi kutekelezwa.' (*SERAC dhidi ya Nigeria*, aya ya 68)

- Hairuhusiwi kushusha hadhi ya haki.

> '[Mkataba wa Afrika hauna kifungu kinachoruhusu kushusha hadhi ya haki. Kwahiyo, mipaka ya haki na uhuru iliyowekwa katika Mkataba haiwezi kuhalalishwa kwa dharura au mazingira maalum. Sababu pekee ya msingi ya mipaka katika haki na uhuru katika Mkataba imeelezwa katika Ibara ya 27(2).' (*Media Rights Agenda v Nigeria*, aya 68 & 69)

- Mkataba unatambua haki za watu kama vile haki ya maendeleo, uhuru wa kuuza rasilimali za asili na haki ya kujiamulia.

> 'Tume ya Afrika inapenda kusisitiza kwamba Mkataba unatambua haki za watu.' (Shauri la *Endrois*)

- Mkataba unaweka wajibu kwa pande zote mbili; nchi.

> 'Kufurahia kwa haki na uhuru pia inamaanisha utekelezaji wa wajibu kwa kila mtu.' (Dibaji ya Mkataba wa Afrika)

Mkataba unabainisha wazi haki za watu kutoka Ibara ya 19 hadi 24.

> 'Watu wote watakua sawa; watapata heshima sawa na watakuwa na haki sawa. Hakuna suala ambalo litahalalisha utawala wa mtu mmoja kwa mwengine.' (Ibara ya 19 ya Mkataba)

## Viwango vya Ziada: Itifaki ya Maputo

Ibara ya 66 ya Mkataba inaruhusu nchi wanachama katika Mkataba kuandaa itifaki maalum au makubaliano pale itakapolazimu ili kuongeza masharti ya Mkataba. Itifaki kadhaa na mikataba imepitishwa kuongeza misingi ya Mkataba.

Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake katika Bara la Afrika (Itifaki ya Maputo) ilipitishwa Maputo, Msumbiji mnamo tarehe 11 Julai 2003 na ulianza kutumika mnamo tarehe 25 Novemba 2005. Itifaki ya Maputo ilihamasishwa na kutambuliwa kwa ulazima wa kuboresha usala-ma duni unaotolewa kwa wanawake chini ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu. Wakati Mkataba wa Afrika unahakikisha na ubaguzi katika msingi wa jinsia, usawa mbele ya sheria, na kukomesha ubaguzi dhidi ya wanawake, Mkataba haujaeleza kwa ufasaha ukiukwaji mahususi wa haki za wanawake unaotokana na ubaguzi.

Itifaki ya Maputo imejitosheleza na inajumuisha haki za kiraia na kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, haki za makundi na kwa mara ya kwanza katika mkataba wa kimataifa, haki za kijinsia na uzazi. Pia ina masharti ya ubunifu ambayo yanaendeleza haki za wanawake kuliko mkataba wowote wa kimataifa wenye nguvu ya kisheria. Kwa mfano, katazo la sheria la kukeketa wanawake limeainishwa vizuri na pia idhini ya utoaji mimba kukiwa na shambulio la aibu, ubakaji, kuzini maharimu, na ikiwa ukuaji wa ujauzito unahatarisha afya ya akili na mwili au maisha ya mama au kijusi. Vilevile, Itifaki hii ni Mkataba wa kwanza wa kimataifa wa haki za binadamu kutaja wazi kuhusu UKIMWI, katika muktadha wa haki za kijinsia na uzazi. Ibara zingine zinaeleza kuhusu ukatili dhidi ya wanawake, mila zenye madhara, ndoa za utotoni, mitala, mirathi, uwezeshaji wa kiuchumi, ushiriki wa wanawake katika siasa na migogoro ya kivita. Itifaki ya Maputo inatambua kwamba baadhi ya wanawake wanaathirika na aina nyingi za ubaguzi na hivyo basi, ukatofautisha ibara kwa ajili ya wajane, wanawake wazee na wanawake wenye ulemavu.

## Nchi 42 zilizoridhia Itifaki ya Maputo hadi Juni 2021



(Nchi 42 ambazo zimeridhia Itifaki ya Maputo zimeoneshwa kwa rangi ya zambarau)

## Itifaki ya Wazee

Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wazee Afrika ilipitishwa mnamo tarehe 31 Januari 2016. Sababu iliyopelekea kupitishwa kwa Itifaki ya Wazee ilikua ni ongezeko la idadi ya wazee na kupungua kwa matunzo na msaada unaotolewa kwa watu masikini katika bara la Afrika.

Itifaki inakamilisha taratibu kuhusu kulinda wazee ambao tayari umewekwa chini ya Mkataba wa Afrika, hususan ibara ya 18(4) ambayo inataka wazee walindwe kwa kuzingatia mahitaji ya 'mwili au maadili'. Pia Itifaki inafungumana na mikataba kadhaa ya Umoja wa Afrika, kwa mfano Mfumo wa Umoja wa Afrika wa Sera na Mpango wa Utekelezaji wa Uzee ambao ulitambua umuhimu wa kuhakikisha kwamba wazee hawabaguliwi, na kwamba nchi inatunga sheria maalum ili kuhakikisha ulinzi wao na kwamba wazee wanashirikiana kwa hiyari baina yao wenyewe ili kuendeleza maslahi yao. Hivyo Itifaki ya Wazee ni kilele cha juhudi za bara la Afrika zilizolenga katika kuboresha hali ya maisha ya wazee ambao wanakabiliwa na baadhi ya desturi zinazofedhehesha na matendo ambayo yana madhara kwa afya zao, usalama na ustawi wao kwa ujumla.

Chini ya ibara ya 3 ya Itifaki, nchi wanachama zinakubali kuondoa ubaguzi dhidi ya wazee. Ubaguzi unaweza kufanyika katika namna mbalimbali ikiwemo, unyanyapaa, kutokujumuishwa katika fursa za ajira, ulinzi wa kijamii na upatikanaji wa huduma za afya kulinGhana na mahitaji yao ya kimwili na kimaadili. Wakati Itifaki inahakikisha haki ambazo wazee wanaweza kupata kwa kutumia nyaraka zingine za kisheria, kwa mfano upatikanaji wa haki, ulinzi sawa mbele ya sheria (ibara ya 4), baadhi ya ibara kadhaa zinaelezea vikwazo malumu. Ibara ya 5 inatoa jukumu kwa nchi kuchukua hatua ili watu wazee waweze kufanya maamuzi kuhusu ustawi wao bila kuingiliwa; desturi zenye madhara dhidi ya wazee (ibara ya 8) na makazi ya wazee ni hiyari na nafuu (ibara ya 11). Hata kama Afrika inafikiriwa kuwa miongoni mwa mabara machanga duniani, Itifaki inaonyesha Afrika inazingatia haki za wazee kwa umakini sana.

## Hadhi ya Uridhiaji

Mpaka mwezi Juni 2021, alama (kidogo) mbili tu za uridhiaji zimerekodiwa kutoka Benin na Lesotho, wakati idadi ya nchi mbazo zilisaini Itifaki ni 17. Jumla ya ridhaa 15 zinatakiwa ili kuhakikisha Itifaki inaanza kutumika.

## Nchi mbili tu zimeridhia Itifaki ya Wazee



(Nchi 2 ambazo zimeridhia Itifaki ya Watu Wazee zimeoneshwa kwa rangi ya zambarau)

## Itifaki ya Haki za Watu wenye Ulemavu Afrika

Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu haki za Watu wenye Ulemavu Afrika ulipitishwa wakati wa Kikao cha Kawaida cha 30 cha Mkutano wa Umoja wa Afrika uliofanyika Ethiopia mnamo Januari 29 mwaka 2018. Uandishi wa Itifaki ulizingatia ulazima wa makubaliano ya kutoa ulinzi maalum wa kisheria kwa watu wenye ulemavu ambao wanazidi kubabiliwa na ubaguzi katika Afrika. Wazo la kuwa na Itifaki lilichochewa na kiwango cha kuogofya cha maisha ya watu wenye ulemavu katika bara la Afrika am-bacho mara nyingi husababisha madhara kama vile umasikini, ujinga na matatizo ya afya.

Sifa kuu za Itifaki ni heshima na utu, ushiriki kamili, fursa sawa kwa watu wenye ulemavu, usawa kati ya wanawake na wanaume, kutoa kipaumbele kwa maslahi ya watoto. Kama mtu mwengine yeyote, wale wanaoathirika kutokana na ulemavu wa mwili au akili wana haki ya kuishi, uhuru, ulinzi, kulindwa dhidi ya mazingira hatarishi kama ilivyotajwa katika ibara ya 12 ya Itifaki ya Watu wenye Ulemavu. Itifaki pia inaju-muisha masharti maalum kwa ajili ya wale wanaofikiriwa kama wapo katika kundi hatarishi na wenye ulemavu. Kwa mfano, Ibara ya 27 ya Itifaki inataja wazi kwamba wanawake wenye ulemavu wanalindwa dhidi ya ukatili wa kingono na kijinsia. Sifa nyingine ya Itifaki ni kuonyesha umuhimu wa watoto wenye ulemavu wanaokabil-iwa na ubaguzi. Itifaki ya Haki za Watu wenye Ulemavu inatusaidia kuelewa mazingira ya watu wenye ulemavu katika bara la Afrika na unatoa suluhisho kwa matatizo yao mengi. Itifaki inawakilisha ufunguo unaofungua watu wenye ulemavu kutoka kwenye uhalisia wa kutengwa na kubaguliwa na inakuza ujumuishwaji wao mkubwa katika jamii. Itifaki inaelewa historia ya Afrika na inajaribu kadri iwezekanavyo kuondoa ubaguzi unaowakabili watu wenye ulemavu huku ikiheshimu desturi za kimataifa.

## Hadhi ya Uridhiaji

Mpaka sasa hakuna nchi ya Afrika iliyoridhia Itifaki. Hii inaweza kuashiria muamko mdogo kukubali wajibu wa nchi za Afrika katika kuboresha hatma ya kundi hatarishi zaidi miongoni mwetu sababu Itifaki ina 'viwango vyenye ubunifu' ambavyo vinaweza kuboresha ulinzi wa watu wenye ulemavu.

## Viwango vingine vya nyongeza

Umoja wa Nchi huru za Afrika umepitisha mikataba kadhaa inayohusu kukuza na kulinda haki za binadamu katika bara la Afrika. Hati hizo zinajumuisha;

| | |
|---|---|
| 1969 | Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika Unaosimamia Masuala Mahususi ya Changamoto za Wakimbizi katika Afrika |
| 1999 | Mkataba wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi |
| 2000 | Sheria ya Uendeshaji wa Umoja wa Afrika |
| 2001 | Itifaki ya Bunge la Umoja wa Afrika |
| 2002 | Itifaki ya Baraza la Amani na Ulinzi |
| 2003 | Mkataba wa Uhifadhi wa Viumbe na Maliasili |
| 2006 | Mkataba wa Vijana wa Afrika |
| 2007 | Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala |
| 2009 | Mkataba wa Umoja wa Afrika Kwa ajili ya Ulinzi na Msaada wa Watu Waliolazimika Kuhama Makazi Ndani ya Nchi (Mkataba wa Kampala) |

Umoja wa Afrika na Tume ya Afrika pia wamepitisha matamko na maamuzi muhimu katika kuelewa na kuendeleza masharti ya Mkataba wa Afrika.

# Athari za Mkataba wa Afrika na viwango vya nyongeza vya haki za binadamu katika Afrika

Tume ya Afrika imejiimarisha kama taasisi ya msingi ya haki za binadamu katika bara la Afrika. Katika kupiga hatua ya kutafsiri Mkataba, Tume imetoa mwongozo kwa nchi kuhusu majukumu yao chini ya Mkataba na ku-tolewa kwa mwongozo kumehamasishwa utungaji wa sheria wa ndani ya nchi.

Katika nchi kadhaa, Mkataba ni sehemu muhimu ya sheria za nchi kutokana na mfumo wa katiba uliopo. Kati-ba ya Benin ya mwaka 1990 inatambua wazi hadhi ya kikatiba ya haki chini ya Mkataba wa Afrika. Hadhi hii imekua muhimu katika kulinda haki za binadamu hususan kwa Mahakama ya Katiba ambayo mara nyingi hutegemea Mkataba wa Afrika. Shauri litasikilizwa kwa muda stahiki, japokuwa Katiba ya Benin haijabainisha moja kwa moja. Haki hii imelindwa na Mkataba wa Afrika. Nigeria wameufanya Mkataba kuwa sehemu ya Sheria zao za ndani kwa kutunga sheria.

Mkataba umekua na matokeo muhimu. Katika maazimio yake ya mada, Tume imeelezea mawanda ya haki na imetoa kipimo kwa ajili ya maendeleo ya sheria za ndani ya nchi hususan katika 'Kanuni na Mwongozo wa Haki ya Uendeshaji wa Mashauri kwa Haki' na 'Kanuni za Uhuru wa Kutoa maoni'. Ilisisitiza nchi kuridhia kusitishwa kwa adhabu ya kifo, hivyo kuunga mkono muelekeo wa kukomesha adhabu ya kifo katika bara la Afrika. Kanuni ya kuwa wazawa ni wamiliki wa haki ilibainishwa wazi katika Mkataba. Katika Ushauri wake ku-husu Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Wazawa Tume ilizungumzia mashaka ya nchi za Afrika kuhusu Tamko hili, na hivyo kuchangia kwa hatma ya upitishwaji wake na nchi nyingi za Afrika. Kupitia ushiriki wake wa kikamilifu katika kupitisha Itifaki ya wanawake, Tume imetoa ufafanuzi kuhusu haki za wanawake katika muktadha wa Afrika, na imetoa mwongozo wenye manufaa makubwa kwa nchi za Afrika. Mnamo mwezi Aprili 2013, Tume ya Afrika pia ilipitisha Sheria ya Mfano kuhusu Upatikanaji wa Habari katika bara la Afrika, sheria ambayo imeziongoza nchi nyingi za Afrika kupitisha sheria ya upatikanaji wa habari.

Vikao vya Tume vinatoa fursa muhimu kwa ajili ya kueleza kwa ufasaha hoja ambazo zinapuuzwa au kunyamazishwa ndani ya nchi. Taasisi zisizo za Kiserikali na Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu zinafaidika na mahusiano haya katika vikao na zinapata taarifa, zinaimarishwa na kujengewa uwezo wa kutekeleza majukumu yao. Ushirikiano na mfumo wa haki za binadamu wa Afrika unasaidia kutengeneza ajenda ya taasisi hizi.

Licha ya kuwa matokeo na taarifa za mwisho za uchunguzi wa Tume hazina nguvu kisheria, nchi huzipa uzito mkubwa. Kwa mfano uamuzi katika shauri la Endorois ulisababisha mjadala makini wa taifa kuhusu makazi ya jamii za wazawa nchini Kenya.

Misheni zinazofanyika katika nchi wanachama huhamasisha na kuunga mkono juhudi zinazoendelea katika ngazi ya taifa ili kuboresha haki za binadamu na kuhamasisha mabadiliko ya sheria au taasisi. Makamishina wanaofanya kazi kama Makatibu Maalum pia hushirikiana na nchi ili kushughulikia madai yanayokuwa ndani ya mamlaka ya Katibu Maalum.

Mfumo wa kushughulikia malalamiko wa Mkataba hutoa nafasi muhimu kwa ajili ya kupata msaada kwa wala-lamikaji ambao hawajapata haki katika ngazi ya taifa. Mara kadhaa maamuzi ya Tume hutekelezwa. Mara nyingi matokeo ya Tume husaidia kukuza uelewa wa kimataifa na mshikamano kama ilivyokuwa nchini

Nigeria wakati wa uongozi wa Abacha.

Mahakama za kitaifa zinazidi kushawishiwa na kutumia Mkataba na maamuzi ya Tume kuwasaidia katika kutafsiri sheria za nchi zao. Mifano maarufu ni ya Mahakama ya Katiba ya Benin, ambayo kama ilivyosemwa hapo awali katika mashauri mengi ilirejea Mkataba wa Afrika na katika baadhi ya mashauri iliutumia Mkataba moja kwa moja. Mahakama ya Katiba ya Afrika Kusini ilitumia Mkataba wa Afrika katika shauri la New Nation Movement NPC na wengine dhidi ya Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini na Wengine kushinikiza ulinzi wa haki ya uhuru wa kushirikiana na wengine. Katika shauri la Molefi Ts'epe dhidi ya Tume Huru ya Uchaguzi Mahakama ya Rufaa ya Lesotho iliuegemea Mkataba wa Afrika pamoja na mikataba mingine ya haki za binadamu za kimataifa.

Maamuzi ya Tume ya Afrika yalitumika katika hukumu za mahakama za kanda (kama vile katika shauri la Campell dhidi ya Zimbabwe, iliyoamuliwa na Mahakama ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika) na hata katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki kwa mfano katika shauri la Diallo (Jamhuri ya Guinea dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo).

Kwa maelezo zaidi kuhusu athari za Tume soma;

Victor Ayeni *The impact of the African Charter and the Maputo Protocol in selected African states* (2016) Pretoria: Pretoria University Law Press (PULP).

Itifaki ya Maputo imehamasisha mabadiliko ya kisheria katika nchi nyingi wanachama, hususan kuhusu utoaji mimba na ukatili wa kijinsia.

# B. Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

## Uanzishwaji

Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu imeanzishwa na Mkataba wa Afrika. Tume ilizinduliwa mnamo tarehe 2 Novemba 1987, Addis Ababa Ethiopia. Sekretarieti ya Tume ipo Banjul, Gambia.

## Muundo

Tume inajumuisha wajumbe 11 waliochaguliwa na Mkutano wa Umoja wa Afrika kutoka kwa wataalam waliopendekezwa na nchi wanachama wa Mkataba. Katika kuchagua wajumbe wa Tume, Baraza huzingatia uwakilishi sawa wa kijiografia na kijinsia. Wajumbe wa Tume huchaguliwa kwa kipindi cha miaka sita na wanaweza kuchaguliwa tena.

Wakishachaguliwa, Makamishina hutumika katika nafasi zao binafsi na siyo kama wawakilishi wa nchi zao husika. Hapo awali, baadhi ya wanachama wa Tume, walikuwa na nafasi za juu za kisiasa katika ngazi ya taifa, hali iliyoathiri uhuru wa Tume. Mnamo Aprili 2005, Tume ya Umoja wa Afrika ilitoa taarifa rasmi (note verbale) kwa nchi wanachama ikiainisha mwongozo kwa ajili ya uteuzi wa wajumbe wa Tume ambao haujumuishi watumishi wa umma na wawakilishi wa kidiplomasia.

## Ofisi

Tume huchagua Mwenyekiti wake na Makamu Mwenyekiti kama Ofisi ya Tume. Wanachaguliwa kwa kipindi cha miaka miwili na huchaguliwa tena kwa muhula mmoja. Ofisi inaratibu shughuli za Tume na kusimamia na kutathmini shughuli za Sekretarieti ya Tume. Aidha, Ofisi imepewa mamlaka ya kufanya maamuzi katika masuala ya dharura wakati wa vikao vya Tume. Hata hivyo, Ofisi inawajibika kuwasilisha taarifa kuhusu dharura hiyo kwa wajumbe katika kikao cha Tume kinachofuata.

Kutokana na kutokuwepo kwa Ibara inayosimamia masuala ya uwakilishi wa kijinsia katika muundo wa Tume, hapo awali wajumbe wote wa Tume walikuwa wanaume. Kamishina wa kwanza mwanamke Vera Duarte Martins (Cape Verde), alichaguliwa mnamo mwaka 1993 na alikua Makamu Mwenyekiti wa kwanza mwanamke mwaka 1997. Ilipofika Novemba 2011, wajumbe wengi walikuwa ni wanawake. Mwaka 2003, Kamishina Salamata Sawadogo alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza mwanamke. Ofisi ya Tume ya Afrika (2019-2021) kwa sasa ina wajumbe wanaume pekee. Hadi sasa Tume imekuwa na Makamu wa Wenyeviti sita wanaume na Wenyeviti saba wanawake. Na imekuwa na Makamu Wenyeviti 12, wawili miongoni mwao walikua Kaimu Makamu Wenyeviti na makamishina wanawake sita tu waliwahi kuwa makamu wenyeviti. Ni dhahiri kwamba Tume ya Afrika imejitahidi kuwa na Ofisi yenye usawa wa jinsia katika miongo miwili ya uwepo wake kuliko ya muongo wa kwanza.

## Sekretarieti

Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika huteua Katibu wa Tume ya Afrika akisaidiwa na wafanyakazi muhimu kwaajili ya kutekeleza majukumu ya Tume kwa ufanisi. Sekretarieti hutoa huduma za utawala, utaalam na utaratibu wa ugavi kwa Tume.

## Mamlaka

Ibara ya 45 ya Mkataba inataja mamlaka ya Tume.

- Ukuzaji wa haki za Binadamu na Watu

Tume inatoa elimu, inahamasisha umma na kusambaza taarifa kupitia semina, makongamano, mikutano na misheni.

- Ulinzi wa haki za binadamu na watu

Tume inahakikisha ulinzi wa haki za binadamu na watu kupitia Utaratibu wa Mawasiliano, njia rafiki za kutatua migogoro, nchi kutoa taarifa (inajumuisha kuzingatia taarifa kivuli za Mashirika yasiyo ya Kiserikali, misaada ya haraka na shughuli zingine za Makatibu Maalum na Kikundi cha Kazi na misheni.

- Tafsiri ya Mkataba

Tume ina mamlaka ya kufasiri ibara za Mkataba baada ya kuombwa na nchi mwanachama, taasisi za Umoja wa Afrika au mtu mmoja mmoja. Hata hivyo hakuna taasisi ambayo imepeleka shauri lolote Tume kwa ajili ya tafsiri ya Mkataba. Tume imepitisha Ushauri mara

moja tu kwa njia iliyo wazi. Ikiwa na Ushauri Kuhusu Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Wazawa (lililopitishwa katika Kikao cha Kawaida cha 41, Mei 2007)

## Kanuni za Utaratibu

Shughuli na taratibu za Tume zinasimamiwa na kanuni zake za utaratibu. Tume ilipitisha Kanuni za Utaratibu za kwanza mwaka 1988 ambazo zilirekebishwa mwaka 1995. Sababu ya uwepo wa Tume ya Haki za Binadamu na Watu ya Afrika, Tume ilipitisha Kanuni za Utaratibu mpya zilizoanza kutumika tarehe 18 Agosti 2010. Mnamo tarehe 4 Machi 2020, Tume ilipitisha Kanuni za Utaratibu mpya.

Kanuni ya 3 ya Kanuni za Utaratibu zinaanzisha uhuru wa Tume na uwezo wake wa kutafsiri Mkataba.

Wajumbe wa Tume wana jukumu la kuheshimu kanuni siri (Kanuni ya 11).

Kanuni ya 63 inaeleza kwamba ingawa maudhui ya Ripoti ya Shughuli yataamuliwa na Tume, ridhaa ya maandishi ya wahusika itaambatishwa katika toleo la ripoti iliyochapishwa.

Tume itaunda kitengo ambacho kitakuwa ni kiungo cha mawasiliano kwa nchi wanachama (Kanuni ya 69).

Kanuni ya 99 inaeleza kwamba ikiwa kuna uvunjifu mkubwa wa haki za binadamu, suala hilo litawasilishwa katika Baraza na pia Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kulinGhana na ibara ya 19 ya Itifaki ya Halmashauri ya Amani na Usalama.

# Wajumbe

## *Makamishina wa Sasa (kama ilivyokuwa hadi Februari 2021)*

**Mwenyekiti**
Solomon Ayele Dersso (2019 - ) Ethiopia

**Makamu Mwenyekiti**
Rémy Ngoy Lumbu (2017 - ) Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

**Makamishina**
Jamesina Essie L King (2015 - ) Sierra Leone
Maya Sahli Fadel (2011 - ) Algeria
Zainabo Sylvie Kayitesi (2007 - ) Rwanda
Marie Louise Abomo (2020 - ) Kameruni
Mudford Zachariah Mwandenga (2020 - ) Zambia
Alexia Amesbury (2020 - ) Shelisheli
Hatem Essaiem (2017 - ) Tunisia
Maria Teresa Manuela (2017 - ) Angola
Ndiamé Gaye (2020 - ) Senegal (Alifariki Machi 2021)

**Wajumbe Waliopita wa Kamisheni**
Yeung Kam John Sik Yuen (2007 - 2019) Mauritius
Lucy Asuagbor (2010 - 2020) Kameruni
Med Kaggwa (2011 - 2017) Uganda
Reine Alapini-Gansou (2005 - 2017) Benin
Lawrence Murugu Mute (2013 - 2020) Kenya
Faith Pansy Tlakula (2011 - 2017) Afrika Kusini
Soyata Maiga (2007 - 2020) Mali
Pacifique Manirakiza (2011 - 2015) Burundi
Mohamed Bechir Khalfallah (2009 - 2015) Tunisia
Mohamed Fayek (2009 - 2011) Misri
Catherine Dupe Atoki (2007 - 2015) Nigeria
Mumba Malila (2005 - 2015) Zambia
Musa Ngary Bitaye (2005 - 2013) Gambia
Sanji Mmasenomo Monageng (2003 - 2013) Botswana
Bahame Tom M Nyanduga (2003 - 2009) Tanzania
Mohamed AO Babana (2003 - 2007) Mauritania
Angela Melo (2001 - 2015) Msumbiji
Salimata Sawadogo (2001 - 2009) Burkina Faso
Yaser Sid Ahmed El-Hassan (2001 - 2009) Sudan
Jainaba Johm (1999 - 2007) Gambia
Andrew R Chigovera (1999 - 2007) Zimbabwe
Vera M Chirwa (1999 - 2005) Malawi
Florence Butegwa (1999 - 2001) Uganda
Nyameko Barney Pityana (1997 - 2003) Afrika Kusini
Kamel Rezzag-Bara (1995 - 2011) Algeria
Julienne Ondziel-Gnelenga (1995 - 2001) Kongo
Victor Oware Dankwa (1993 - 2005) Ghana
Vera De Melo D Martins (1993 - 2000) Cape Verde
Atsu Kofi Amega (1993 - 1999) Togo
Mohammed H Ben Salem (1992 - 2003) Tunisia
Ibrahim Ali B El-Sheikh (1987 - 2011) Misri
Isaac Nguema (1987 - 2001) Gabon
Youssoupha Ndiaye (1987 - 2001) Senegal
Alioune Mahmoud B Beye (1987 - 1998) Mali

U Oji Umozurike (1989 - 1997) Nigeria
Robert Habesh Kisanga (1987 - 1997) Tanzania
Sourahata B S Janneh (1987 - 1995) Gambia
Chama LC Mubanga-Chipoya (1987 - 1993) Zambia
Moleleki D Mokama (1987 - 1993) Botswana
Alexis Gabou (1987 - 1993) Kongo
Ali Mahoud Bouhedma (1987 - 1993) Libya
Grace S Ibingira (1987 - 1989) Uganda

**Kwa mawasiliano zaidi kuhusu shughuli za Kamisheni; wasiliana na:**
Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu
#31, Bijilo Annex Layout
Kombo North District Western Region
PO Box 673 Banjul The Gambia
Simu: (220) 441 05 05; 441 05 06
Faksi: (220) 441 05 04
baruapepe: au-banjul@africa-union.org Tovuti: www.achpr.org

# Vikao

Hadi kufika Juni 2021, Tume ilikua imefanya vikao vya kawaida 68 na vikao maalum 32.

## Vikao vya Kawaida

Tume imefanya vikao vya kawaida kila mwaka. Kwa muda, muda wa kufanya uliongezeka kutoka siku 10 hadi 21. Sehemu ya kwanza ya kikao cha kawaida huwa cha wazi na sehemu ya pili hufanyika kwa faragha.

## Vikao maalum

Tume inaweza kufanya vikao maalum. Vikao maalum huitishwa na Mwenyekiti wa Tume baada ya maombi ya Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika au wajumbe wengi wa Tume. Kwa muda, vikao viwili vya kawaida vimekua vikifanyika kila kwa mwaka.

## Ajenda

Ajenda ya kikao cha kawaida huandaliwa na Sekretarieti ya Tume kwa kushauriana na Ofisi ya Tume. Zaidi ya masuala yaliyopendekezwa katika kikao kilichopita, Mwenyekiti , wajumbe wa Tume, nchi wanachama, taasisi za Umoja wa Afrika , Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu, Taasisi zisizo za Kiserikali na taasisi yoyote inayofanya kazi maalum ya Umoja wa mataifa zinaweza kupendekeza suala la

ziada kwa ajili ya kujumuishwa katika ajenda. Hata hivyo, Ofisi ya Tume ina maamuzi ya mwisho kuhusu masuala ya kuwekwa katika ajenda za awali.Relatório de actividades

## Ripoti za Shughuli za Tume

Tume huwasilisha katika kila Kikao cha Kawaida cha Mkutano wa Umoja wa Afrika ripoti ya shughuli zake wa-kati wa vikao. Halmashauri Kuu huzingatia ripoti kwa niaba ya Baraza. Ripoti huwasilishwa na Mwenyekiti wa Tume au mwakilishi wao. Tume inaweza kuchapisha taarifa kuhusu shuguli zake za kulinda haki (mawasiliano na misheni za ulinzi) mara baada ya ripoti kupitishwa na uchapishaji wake kuidhinishwa na Halmashauri Kuu kwa niaba ya Baraza. Kabla ya kupitishwa kwa Ripoti za Shughuli za Mkutano wa Umoja wa Afrika, kwa kawai-da Tume hutoa taarifa mara moja baada ya kikao.

## Vikao vya Kawaida na Ripoti ya Shughuli za Tume tangu mwaka 1987

| Kikao cha | Tarehe | Nchi Mwenyeji | Ripoti ya Shughuli ya |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 Novemba 1987 | Ethiopia | 1 |
| 2 | 8 - 13 Februari 1988 | Senegal | 1 |
| 3 | 18 - 28 Aprili 1988 | Gabon | 2 |
| 4 | 17 - 26 Oktoba 1988 | Misri | 2 |
| 5 | 3 - 14 Aprili 1989 | Libya | 2 |
| 6 | 23 Okt - 4 Nov 1989 | Gambia | 3 |
| 7 | 18 - 28 Aprili 1990 | Gambia | 3 |
| 8 | 8 - 21 Oktoba 1990 | Gambia | 4 |
| 9 | 18 - 25 Machi 1991 | Nigeria | 4 |
| 10 | 8 - 15 Oktoba 1991 | Gambia | 5 |
| 11 | 2 - 9 Machi 1992 | Tunisia | 5 |
| 12 | 12 - 21 Oktoba 1992 | Gambia | 6 |
| 13 | 29 Machi - 7 Aprili 1993 | Gambia | 6 |
| 14 | 1 - 10 Desemba 1993 | Ethiopia | 7 |
| 15 | 18 - 27 Aprili 1994 | Gambia | 7 |
| 16 | 25 Okt - 3 Nov 1994 | Gambia | 8 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17 | 13 - 22 Machi 1995 | Togo | 8 |
| 18 | 2 - 11 Oktoba 1995 | Cape Verde | 9 |
| 19 | 26 Machi - 4 Aprili 1996 | Burkina Faso | 9 |
| 20 | 21 - 31 Oktoba 1996 | Mauritius | 10 |
| 21 | 15 - 24 Aprili 1997 | Mauritania | 10 |
| 22 | 2 - 11 Novemba 1997 | Gambia | 11 |
| 23 | 20 - 29 Aprili 1998 | Gambia | 11 |
| 24 | 22 - 31 Oktoba 1998 | Gambia | 12 |
| 25 | 26 Aprili - 5 Mei 1999 | Burundi | 12 |
| 26 | 1 - 15 Novemba 1999 | Rwanda | 13 |
| 27 | 27 Aprili - 11 Mei 2000 | Algeria | 13 |
| 28 | 23 Okt - 6 Nov 2000 | Benin | 14 |
| 29 | 23 Aprili - 7 Mei 2001 | Libya | 14 |
| 30 | 13 - 27 Oktoba 2001 | Gambia | 15 |
| 31 | 2 - 16 Mei 2002 | Afrika Kusini | 15 |
| 32 | 17 - 23 Oktoba 2002 | Gambia | 16 |
| 33 | 15 - 29 Mei 2003 | Niger | 16 |
| 34 | 6 - 20 Novemba 2003 | Gambia | 17 |
| 35 | 21 Mei - 4 Juni 2004 | Gambia | 17 |
| 36 | 23 Nov - 7 Des 2004 | Senegal | 18 |
| 37 | 27 Aprili - 11 Mei 2005 | Gambia | 18 |
| 38 | 21 Nov - 5 Dez 2005 | Gambia | 19 |
| 39 | 11- 25 Mei 2006 | Gambia | 20 |
| 40 | 15 - 29 Novemba 2006 | Gambia | 21 |
| 41 | 16 - 30 Mei 2007 | Ghana | 22 |
| 42 | 15 - 28 Novemba 2007 | Jamhuri ya Kongo | 23 |
| 43 | 7 - 22 Mei 2008 | Swaziland | 24 |
| 44 | 10 - 24 Novemba 2008 | Nigeria | 25 |
| 45 | 13 - 27 Mei 2009 | Gambia | 26 |
| 46 | 11- 25 Novemba 2009 | Gambia | 27 |
| 47 | 12 - 26 Mei 2010 | Gambia | 28 |
| 48 | 10 - 24 Novemba 2010 | Gambia | 27 |
| 49 | 28 Aprili - 12 Mei 2011 | Gambia | 30 |
| 50 | 24 Out - 5 Nov 2011 | Gambia | 31 |
| 51 | 18 Aprili - 2 Mei 2012 | Gambia | 32 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 52 | 9 - 22 Oktoba 2012 | Côte d'Ivoire | 33 |
| 53 | 9 - 22 Aprili 2013 | Gambia | 34 |
| 54 | 22 Oktoba - 5 Nov 2013 | Gambia | 35 |
| 55 | 28 Aprili - 12 Mei 2014 | Angola | 36 |
| 56 | 21 Aprili - 7 Mei 2015 | Gambia | 38 |
| 57 | 4 - 18 Novemba 2015 | Gambia | 39 |
| 58 | 6 - 20 Aprili 2016 | Gambia | 40 |
| 59 | 21 Oktoba - 4 Nov 2016 | Gambia | 41 |
| 60 | 8 - 22 Mei 2017 | Niger | 42 |
| 61 | 1 - 15 Novemba 2017 | Gambia | 43 |
| 62 | 25 Aprili - 9 Mei 2018 | Mauritania | 44 |
| 63 | 24 Oktoba - 13 Nov 2018 | Gambia | 45 |
| 64 | 24 Aprili - 14 Mei 2019 | Misri | 46 |
| 65 | 21 Oktoba - 10 Nov 2019 | Gambia | 47 |
| 66 | 13 Julai - 7 Agosti 2020 | Gambia | 48 na 49 |
| 67 | 13 Nov - 3 Dez 2020 | Gambia | 48 & 49 |
| 68 | 14 Aprili - 4 Mei 2021 | Gambia | - |

## Vikao Maalum vya Tume

| Kikao maalum cha: | Tarehe | Nchi Mwenyeji | Ripoti ya Shughuli ya |
|---|---|---|---|
| 1 | 13 - 14 Juni 1989 | Gambia | 2 |
| 2 | 18 - 19 Desemba 1995 | Uganda | 9 |
| 3 | 18 - 19 Setembro 2004 | Afrika Kusini | 18 |
| 4 | 17 - 23 Februari 2008 | Gambia | 24 |
| 5 | 21 - 29 Julai 2008 | Gambia | 25 |
| 6 | 30 Machi - 3 Aprili 2009 | Gambia | 26 |
| 7 | 5 - 12 Oktoba 2009 | Senegal | 27 |
| 8 | 22 Fev - 3 Machi 2010 | Gambia | 28 |
| 9 | 23 Fev - 3 Machi 2011 | Gambia | 30 |
| 10 | 12 - 16 Desemba 2011 | Gambia | 31 |
| 11 | 21 Februari - 1 Machi 2012 | Gambia | 32 |
| 12 | 30 Julai - 4 Agosti 2012 | Algeria | 33 |
| 13 | 18 - 25 Februari 2013 | Gambia | 34 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 14 | 20 - 24 Julai 2013 | Kenya | 35 |
| 15 | 7 -14 Machi 2014 | Gambia | 36 |
| 16 | 20 - 29 Julai 2014 | Rwanda | 37 |
| 17 | 19 - 28 Februari 2015 | Gambia | 38 |
| 18 | 29 July - 7 Agosti 2015 | Kenya | 39 |
| 19 | 16 - 25 Februari 2016 | Gambia | 40 |
| 20 | 9 - 18 Juni 2016 | Gambia | 41 |
| 21 | 23 Fev - 4 Machi 2017 | Gambia | 42 |
| 22 | 29 July - 7 Agosti 2017 | Senegal | 43 |
| 23 | 13 - 22 Februari 2018 | Gambia | 44 |
| 24 | 30 Julai - 8 Agosti 2018 | Gambia | 45 |
| 25 | Februari - 5 Machi 2019 | Gambia | 46 |
| 26 | 16 - 30 Julai 2019 | Gambia | 47 |
| 27 | 19 Fev - 4 Machi 2020 | Gambia | 48 na 49 |
| 28 | 29 Juni - 1 Julai 2020 | Gambia | 48 na 49 |
| 29 | 2 - 5 Oktoba 2020 | Gambia | 48 na 49 |
| 30 | 11 - 19 Desemba 2020 | Gambia | 48 na 49 |
| 31 | 19 - 25 Februari 2021 | Gambia | - |
| 32 | 12 Mei 2021 | Gambia | - |

## Mawasiliano

Mawasiliano (malalamiko) ni moja ya njia zinazotumika na Tume kuhakikisha utekelezaji wa nchi wanachama wa haki za binadamu zillizopo kwenye Mkataba. Tume inaweza kupokea malalamiko toka kwa nchi moja dhidi ya nchi nyingine (nchi dhidi ya nchi) chiniya ibara ya 48 na 49 ya Mkataba. Mpaka sasa Tume imemaliza mawasiliano ya nchi moja tu. Tume pia hushughulikia mawasiliano kutoka kwa mtu na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali dhidi ya nchi moja au zaidi (malalamiko ya mtu) kuhusu malalamiko ya uvunjaji wa haki za binadamu kwa mujibu wa mamlaka yake na ibara ya 55 ya Mkataba wa Afrika. Hadi mwezi Machi 2021, mawasiliano 547 ya watu binafsi yalikua yamepokelewa tangu Tume ilipoanzishwa mwaka 1987.

## Mawasiliano baina ya nchi

Mawasiliano ya nchi ya kwanza na ya pekee ambayo Tume imeyakamilisha yaliamuliwa baada ya kusikilizwa mwaka 2003.

> **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo dhidi ya Burundi, Rwanda na Uganda**
> **(2004) AHRLR 19 (ACHPR 2003)**
>
> Mawasiliano haya yaliwasilishwa na Jamhuri ya Muungano wa Kongo dhidi ya Jamhuri ya Burundi, Rwanda na Uganda. Jamhuri ya Kongo iliituhumu Burundi, Rwanda, na Uganda (Wajibu mawasiliano) kufanya uvunjivu mkubwa wa haki za binadamu na watu katika majimbo ya Kongo kupitia makundi ya waasi ambayo mleta mawasiliano anatuhumu yalikua yakiungwa mkono na wajibu mawasiliano.

Ikipata msukumo toka kanuni za ujumla za sheria ya kimataifa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa na maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Tume ilisema kuwa vitendo vya wajibu mawasiliano kukalia ardhi ya nchi inayolalamika vinavunja haki ya watu wa Kongo ya kujitambua na inajumuisha hatari katika amani na usalama wa taifa na kimataifa.

Tume ilitamka kwamba vitendo vya ukatili vilivyooneshwa na nchi zinazojibu mawasiliano katika ardhi ya mlalamikaji ni kashfa kwa maadili ya kiungwana ya mila za kiafrika. Aidha, Tume ilibaini kwamba kwa kusimamia rasilimali mbalimbali zinazozalishwa katika nchi inayolalamika, nchi zinazojibu malalamiko zinawanyima watu wa Kongo haki ya kuuza rasilimali zao kwa uhuru. Hivyo Tume ilihitimisha kwamba nchi zinazojibu mawasiliano zimevunja masharti mbalimbali ya Mkataba wa Afrika na kuwasihi kuchukua hatua ili kufuata wajibu wao chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa, Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika na Mkataba wa Afrika na pia kulipa fidia ya kutosha kwa waathiriwa wa uvunjifu huo.

Tume ilipata shauri lililokubaliwa la nchi dhidi ya nchi *Djibouti dhidi ya Eritrea*; Uamuzi wake kuhusu kusikilizwa bado.

## Ni Nani anayeweza kuwasilisha mawasiliano ya mtu binafsi?

Mtu yeyote na au Shirika Lisilo la Kiserikali linaweza kuwasilisha

mawasiliano mbele ya Tume. Mkataba hauja-eleza suala la kufika mbele ya Tume na Kanuni za Utaratibu wa Tume hazijaweka masharti kwa ajili ya hitaji la mwathiriwa.

Mawasiliano yanaweza kuwasilishwa na mwathiriwa (waathiriwa) kwa niaba yao. Mtu binafsi au Shirika Lisilo la Kiserikali inayowasilisha mawasiliano kwa niaba ya mtu zinahitaji kupata ridhaa kutoka kwa mwathiriwa. Shirika Lisilo la Kiserikali pia linafurahia hadhi ya uangalizi kwenye Tume. Mtu mmoja mmoja au Shirika Lisilo la Kiserikali halihitaji kuwa raia au kusajiliwa katika nchi ambayo inalalamikiwa.

## Mawasiliano yanaweza kuwasilishwa dhidi ya nani?

Mawasiliano yanaweza kuwasilishwa dhidi ya nchi tu ambayo imeridhia Mkataba wa Afrika.

## Msaada wa Kisheria

Tume kwa uamuzi wake yenyewe au baada ya kupokea ombi kutoka kwa mwandishi wa mawasiliano wanawe-za kuwezesha upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa mwandishi wa mawasiliano. Katika kufikia uamuzi huu, Tume lazima iwe imeshawishika kwamba mwandishi hana kipato cha kutosha kulipa gharama zote au baadhi za mawasiliano na msaada wa kisheria ni muhimu kuhakikisha usawa pande mbili za wahusika wa malalamiko kwa ajili ya kutimiza inavyostahiki.

## Vigezo vya Kupokea Mawasiliano (ibara ya 56 ya Mkataba)

Kabla Tume haijatamka kama inapokea mawasiliano yoyote ni lazima mawasiliano hiyo ikidhi masharti yote yafuatayo:

- Mawasiliano yanapaswa kuonesha mwandishi (waandishi).
- Mawasiliano yanapaswa yaendane na Sheria ya Uendeshaji wa Umoja wa Afrika na Mkataba wa Afrika.
- Mawasiliano hayapaswi kuandikwa kwa lugha ya dharau au matusi.
- Mawasiliano hayapaswi kutokana na ripoti za vyombo vya habari tu.

- Nafuu za ndani ya nchi ni lazima ziwe zimeombwa isipokuwa kama zinacheleweshwa sana.
- Mawasiliano yanapaswa kuwasilishwa ndani ya muda stahiki.
- Hoja zilizoibuliwa katika mawasiliano hazipaswa kuwa zile zilizosuluhiswa chini ya taratibu wa Umoja wa Afrika au Umoja wa Mataifa.

## Kutumia nafuu zote ndani ya nchi

Kutumia nafuu zote ndani ya nchi ni miongoni mwa masharti ya kupokea shauri katika Tume ya Afrika na taasisi zingine za kimataifa za haki za binadamu. Hii ni kwa sababu ya kushirikiana kwa mfumo wa kimataifa wa utatuzi wa mashauri. Mantiki ya sharti la kutumia nafuu za ndani ya nchi ni kuijulisha serikali kuhusu uvunjifu hivyo basi kuipa serikali nafasi ya kutoa nafuu na kuzipa mahakama za ndani ya nchi nafasi ya kuamua shauri.

Nafuu zinazotakiwa kuombwa ni zile zinazopatikana, zinazofaa katika kurekebisha kosa lililotokea. Nafuu inapatikana ikiwa upatikanaji wake hauna vikwazo vyovyote, una ufanisi ikiwa inatoa uwezekano wa mafanikio, na inatosha ikiwa unaweza kurekebisha kosa.

Mlalamikaji hahitajiki kutumia nafuu za ndani ya nchi ikiwa mlalamikaji yupo katika makundi yafuatayo:

- Ikiwa muathiriwa ni masikini (*Purohit dhidi ya Gambia*).
- Ikiwa malalamiko yanahusisha ukiukaji mkubwa wa haki (*Free Legal Assistance Group dhidi ya Zaire*)
- Ikiwa sheria ya ndani ya nchi zinaondoa mamlaka ya mahakama za taifa (*Media Rights Agenda dhidi ya Nigeria*).
- Ikiwa haki zinazodaiwa hazijawekwa katika sheria za ndani ya nchi (*SERAC dhidi ya Nigeria*)
- Ikiwa ni hatari kwa mlalamikaji kurudi katika nchi iliyofanya ukiukaji kwa ajili ya kutumia nafuu za ndani ya nchi (*Jawara dhidi ya Gambia*; *Abubarkar dhidi ya Ghana*).
- Kama mlalamikaji anahusisha 'idadi kubwa' ya watu wanaoweza kuwa walalamikaji muhimu (*African Institute for Human Rights and Development dhidi ya Guinea*).
- Ikiwa utaratibu wa kupata nafuu za ndani ya nchi unaweza kucheleweshwa kwa muda mrefu (ibara 56 (5) ya Mkataba wa Afrika)
- Ikiwa haileti maana kuweka sharti la kutumia nafuu za ndani ya nchi.

## Utaratibu wa Mawasiliano

| | |
|---|---|
| Usajili wa mawasiliano kwa Sekretarieti ya Tume | • Uwasilishaji wa mawasiliano<br>• ugawaji wa namba ya faili<br>• utambuzi wa mawasiliano na Sekretarieti |
| Kusitishwa kwa mawasiliano na watu binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (Kanuni ya 115) | • Kuonyesha jina, taifa na saini ya mtu anayewasilisha mawasiliano au jina na saini ya mwakilishi (wawakilishi) wa Shirika Lisilo na Kiserikali.<br>• Mlalamikaji ataonyesha kama anapenda kubaki hajulikani<br>• Anuani ya mawasiliano<br>• Kueleza vizuri suala au hali inay-olalamikiwa (mahali, tarehe na asili ya ukiukwaji)<br>• Kuonyesha jina lamuathirika kama ni tofauti na mlalamikaji<br>• Kuonyesha taasisi yoyote ya umma ambayo imetambua suala au hali inayolalamikiwa<br>• Jina la nchi inayodaiwa kuhusika na uvunjifu |
| Nchi mwanachama inayohusika inajulishwa kuhusu mawasiliano | |
| Invitation for comme Mwaliko kwa nchi mwanachama na mwandishi wa mawasiliano kutoa maoni (ndani ya muda wa miezi mitatu) | |
| Tume inafanya maamuzi kuhusu kukubaliwa | |
| Kama malalamiko yanakubaliwa pande husika zinatakiwa kutuma maoni yao kuhusu hoja za msingi kutoa maoni yao | |
| Kama pande husika zipo tayari Tume itateua katibu kwa ajili usuluhishi wa malalamiko. | |
| Kama usuluhishi hautafanikiwa, Tume itaamua mawasiliano kwa kusik-iliza msingi wa shauri. | |
| Tume inatoa maoni yake ya mwisho kwa nchi | |
| Ikiwa Tume imeona ukiukwaji wa haki, Sekretarieti inatuma barua ya(za) ufuatiliaji ikihoji utekelezaji wa mapendekezo. | |

## Hatua za muda

Mara baada mawasiliano kupokelewa, Tume inaweza kuelekeza nchi husika kuchukua hatua moja au zaidi za muda kusubiri maamuzi ya mwisho ya mawasiliano. Hatua za muda ni muhimu

kuzuia madhara yasiyorekebishika anayofanyiwa mwathiriwa wa ukiukwaji unaodaiwa kufanyika. Iwapo nchi itashindwa kutekeleza maombi ya Tume ya kupitisha hatua za muda baada ya muda ulioainishwa, Tume chini ya Kanuni ya 130 ya Kanuni za Utaratibu za mwaka 2020 inaweza kupeleka mawasiliano katika Mahakama ya Afrika.

## Usuluhishi

Kanuni za Utaratibu za Tume zinakuza utatuzi wa migogoro kwa usuluhishi kati ya pande husika. Kabla ya maamuzi hayajafikiwa, ni lazima masharti yakubaliwe na pande zote mbili. Ni lazima usuluhishi uzingatie kanuni za haki za binadamu.

## Maamuzi na mapendekezo

Ikiwa Tume imebaini ukiukwaji wa haki za binadamu, Tume inaweza kutamka kwamba nchi imekiuka haki za binadamu. Katika mazingira mengine Tume inaweza kujumuisha katika matokeo yake mapendekezo yenye matokeo zaidi. Kwa mfano, inaweza kupendekeza nchi ichukue hatua muhimu kuendana na Mkataba ikiwemo kulipa fidia kwa waathiriwa.

## Ufuatiliaji wa mapendekezo ya Tume

Utaratibu wa Tume wa kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yake katika maamuzi ya msingi wa shauri uliwe-kwa katika Kanuni Utaratibu za Tume za mwaka 2010 ambazo zilihuishwa mwaka 2020 katika Kanuni za Utaratibu.

Kanuni za Utaratibu za Tume ya Afrika za mwaka 2020 zilianza kutumika mnamo tarehe 2 Juni 2020.

Kwa mujibu maelezo ya Tume ya Afrika katika taarifa kwa vyombo vya habari, Kanuni mpya zilipitishwa kwa lengo la kuhakikisha ufanisi zaidi katika kutekeleza majukumu ya Tume ya Afrika chini ya Mkataba wa Afrika. Kanuni mpya zinaleta kipengele kipya katika:

- Mamlaka na hadhi ya Tume ya Afrika. Kanuni ya 3 imerudia hali ya kujitegemea wa Tume ya Afrika na mamlaka yake ya kutafsiri Mkataba wa Afrika na maamuzi yake yenyewe na kuhakikisha utendaji wa Sekretarieti yake.

- Jukumu la Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu. Kanuni ya 79 inalenga kuongeza jukumu la Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu katika kufuatilia mapendekezo ya Tume. Inaeleza kwamba Hitimisho la Maoni kuhusu Ripoti ya Nchi litasambazwa kwa Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu pamoja na Serikali.
- Vikao vya Tume: Kanuni ya 28 inaeleza kuhusu Tume kufanya mikutano minne kwa mwaka na hivyo kuzifanya kanuni ziwe sawa na desturi ya sasa.
- Utaratibu wa mawasiliano ya Tume ya Afrika. Walalamikaji wanatakiwa kuwasilisha 'mawasilisho yao ya msingi na kukubaliwa' kwa pamoja, ndani ya siku 60 tangu kupokea uamuzi wa kusitishwa. Nchi itapewa siku 60 za kujibu kuhusu hoja na kupokelewa ikiwa baada ya mlalamikaji kuwa na nafasi ya kuwasilisha majibu.

## Baadhi ya maamuzi ya kihistoria ya Tume

- ***SERAC dhidi ya Nigeria* (2001) AHRLR 60 (ACHPR 2001)**

Katika shauri hili Serikali ya Nigeria kupitia shirika lake linalalomilikiwa na Serikali la Kampuni ya Taifa ya Pe-troli Nihgeria (Nigera National Petroleum Corporation) na kampuni ya kimataifa, Shell Petroleum Development Corporation, ilidaiwa wamesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira kwa watu wa Ogoni. Ardhi na vyanzo vya maji vilichafuliwa kama matokeo ya kuchimba mafuta, hivyo kusababisha kilimo na uvuvi (njia mbili kuu za msingi za kiuchumi za kuingiza kipato kwa watu wa Ogoni) kushindikana. Pia mlalamikaji alidai kuwa Serikali ya Nigeria imedharau uvunjifu uliofanyika pamoja na kuwepo kwa maombi kadhaa, serikali ilishindwa kuitaka kampuni za mafuta kufanya tathmini ya athari ya mazingira na jamii ya shughuli zake.

> 'Serikali zinajukumu la kuheshimu wananchi wake, sio tu kwa kupitia sheria inayofaa na utekelezaji wake ila pia kwa kuwalinda kutokana na shughuli zenye madhara ambazo zinafanywa na makampuni binafsi.' (shauri la *SERAC*, aya 57)

Jamii pia hazikutoa maoni kabla ya kampuni haijaanza kufanya kazi. Vikosi ya usalama viliachiliwa kushambulia, kuchoma na kuharibu vijiji vyao, makazi na mashamba kila walipojaribu kuandamana. Walalamikaji walidai kuwa shughuli hizi za serikali ya Nigeria, zinakiuka haki ya watu wa ogoni kupata haki ya kufurahia hali bora inayoweza kupatikana ya afya njema ya kimwili na kiakili, mazingira safi, kumiliki mali, maliasili na makazi ya kutosha.

> 'Haki ya kupata chakula imeunganishwa na haiwezi kutenganishwa na utu wa binadamu na hivyo ni muhimu kwa kufurahia na kutimiza haki zingine kama afya, elimu,kazi na kushiriki katika siasa…Kiwango cha chini cha haki ya chakula kinataka kwamba …serikali isiharibu au kuchafua chanzo cha chakula.' (Shauri la *SERAC*, aya ya 65)

Tume ilibaini kuwa Serikali ya Nigeria ilikiuka Mkataba wa Afrika. Iliiagiza Serikali iache kuzishambulia jamii za Ogoni, kuhakikisha fidia ya kutosha inalipwa kwa waathiriwa wa uvunjifu wa haki na pia kufanya tathmini inayofaa ya mazingira na jamii kwa ajili ya maendeleo ya uchimbaji mafuta.

- ***Centre for Minority Rights Development (Kenya) na Minority Rights Group International kwa niaba ya Endorois Welfare Council dhidi ya Kenya* (2009) AHRLR 75 (ACHPR 2009)**

Katika shauri hili serikali ya Kenya iliwaondoa jamii ya wazawa wa Endorois kwa nguvu kutoka kwenye ardhi za mababu zao karibu na ziwa Bogoria bila mashauriano au kuwalipa fidia. Hivyo watu wa Endrois walishindwa kufika katika maeneo ya kuabudu yaliyopo katika ziwa Bogoria. Walalamikaji walidai kuwa huu ni ukiukwaji wa Mkataba wa Afrika.

Katika uamuzi huu mpya na wa aina yake, Tume iliamua kuhusu haki ya maendeleo katika Mkataba wa Afrika. Mkataba ni wa Afrika ni mkataba pekee wa kimataifa wenye nguvu kisheria unaotambua haki hii. Tume pia ilielezea haki za wazawa katika bara la Afrika.

> 'Haki ya maendeleo ni kipimo chenye pande mbili… ni muhimu kama njia na matokeo. Ukiukwaji wa kipengele chochote kile kiwe cha utaratibu au msingi ni ukiukaji wa haki ya maendeleo.
>
> …sio tu hali ya kutoa, kwa mfano, makazi ya watu, maendeleo ni badala ya kutoa ni kuwajengea watu uwezo wa kuchagua sehemu ya kuishi. '(Shauri la *Endrois*, aya ya 277 na 288)

Tume ilibaini kuwa utamaduni, dini na maisha ya kimila ya watu wa Endrois unaingiliana kwa kiasi kikubwa na ardhi za mababu zao. Ilibainika Serikali ya Kenya imekiuka haki na ilihimizwa kuiruhusu jamii ya Endrois kwenda Ziwa Bogoria na sehemu zinazolizunguka ziwa kwa ajili ya shughuli za kidini na kimila na kulipa fidia ya

kutosha kwa jamii kwa madhara waliyopata, kulipa mirahaba kwa jamii ya Endrois kutoka kwenye shughuli za kiuchumi zilizopo na kutoa ripoti kwa Tume kuhusu utekelezaji wa mapendekezo haya.

- ***Jawara dhidi ya Gambia* (2000) AHRLR 107 (ACHPR)**

Katika mawasiliano haya, Tume iilpitia kwa kina Ibara ya 56 ya Mkataba wa Afrika ambao unaweka kanuni kwa ajili ya upokeaji wa mawasiliano. Mawasilaino yaliletwa na Rais wa zamani wa Gambia (Bwana Dawda Kairaba Jawara) ambaye alifukuzwa katika jeshi. Mawasiliano yaliletwa dhidi ya jeshi la serikali ya Gambia ambayo ililalamikiwa kwa ukiukwaji wa Mkataba wa Afrika. Mawasiliano hayo yalidai matumizi mbaya ya dhahiri ya madaraka ya serikali inayojibu mawasiliano vilevile kutokufuata utaratibu wa sheria kwa kwa nchi inayojibu mawasiliano kwa ukamataji wa kibaguzi na vifungo holela, mauaji ya maafisa wa zamani, na wanaoiunga mkono serikali ya mlalamikaji bila kufuata sheria. Aidha mawasiliano yanadai kwamba serikali ya mjibu mawasiliano kwa kupitia amri walioondoa mamlaka za mahakama na kudharau mahakama dhahiri. Mjibu mawasiliano alipinga kupokelewa kwa mawasiliano kwa kigezo kuwa hayakuendana/hayakukidhi vigezo viwili chini ya ibara ya 56 ya mkataba.

Katika uamuzi wake, Tume ilitamka kwamba, haitakuwa na tija kutumia nafuu zinazopatikana ndani ya nchi kama mazingira yanafanya ishindakane kutumia nafuu hizo. Katika kutathmini endapo mtu binafsi ametumia nafuu zote ndani ya nchi kuhusiana na ukiukwaji aliofanyiwa, masuala matatu lazima yazingatiwe ambayo ni upatikanaji, ufanisi na matokeo yanayotarajiwa ya nafuu. Nafuu inapatikana ikiwa inaweza kufuatiliwa bila kizuizi, ina matokeo yanayotakiwa ikiwa kuna matumaini ya kushinda na inatosha ikiwa kurekebisha manung'uniko kwa kiasi cha kutosha. Tume ilihitimisha kwamba hali ya Gambia kwa wakati huo ilikua inazuia upatikanaji wa nafuu za ndani ya nchi. Tume pia ilibaini kwamba sehemu ya taarifa ya mawasiliano ilitokana na ripoti za vyombo vya habari hivyo kupelekea isikubaliwe.

> Nafuu ambayo upatikanaji wake hauna uhakika haiwezi kuombwa na nchi kwa hasara ya malalamijkaji (Shauri la *Jawara*, aya ya 34)

Kuhusu kiini cha shauri, Tume ilitamka kwamba kwa kusitisha haki za binadamu katika Katiba ya Gambia, serikali ya kijeshi imekiuka haki zilizowekwa katika Mkataba na kulindwa chini ya Katiba. Muhimu zaidi, Tume ilitamka kwamba serikali ya kijeshi kwa

kupitia mapinduzi ya kijeshi imekiuka haki ya watu wa Gambia ya kujitawala kwa kuwanyima wananchi haki ya kuchagua serikali yao kwa uhuru. Tume imebaini serikali ilikiuka haki za binadamu na ilihimiza kurekebisha sheria zake ziendane na masharti ya Mkataba.

- ***Purohit na Mwenzake dhidi ya Gambia* (2003) AHRLR 96 (ACHPR 2003)**

Katika mawasiliano haya, Tume ilishughulikia pamoja na masuala mengine haki ya afya na matibabu ya watu wenye ugonjwa wa afya ya akili. Mawasiliano yaliwasilishwa na walalamikaji kwa niaba ya wagonjwa walio-zuiliwa kizuizini katika Kitengo cha Tiba ya Magonjwa ya Afya ya Akili cha Hospitali ya Royal Victoria nchini Gambia. Mawasiliano yanadai kuwa masharti ya Sheria ya Uzuizi wa Wagonjwa wa Afya ya Akili haitoshi na imeshindwa kutafsiri nani ni mgonjwa wa afya ya akili na haijabainisha masharti ya kulinda haki wakati wagonjwa wanachunguzwa na kuwekwa kizuizini. Vile vile, mawasiliano yalidai kuwa hali katika kizuizi haifai na inakiuka haki za wagonjwa. Walalamikaji walieleza kwamba mfumo haukutoa uchunguzi wowote huru wa kiutawala katika kitengo au vituo vilivyopo. Sheria haijaweka sharti lolote la msaada wa kisheria kwa waliowe-kwa kizuizini na haijaleza kuhusu fidia kwa wagonjwa kama kukiwa na ukiukwaji wa haki zao. Mawasiliano vilevile yalidai kwamba wagonjwa wananyimwa haki zao za kupiga kura.

Katika uamuzi wake, Tume ilisisitiza kwamba utu wa binadamu ni haki ya asili ambayo lazima iheshimiwe wa-kati wote bila kujali uwezo wa akili wa mtu au watu na watu wenye ugonjwa wa afya ya akili wana haki ya ku-wa na maisha bora kama watu wengine. Watu hao hawatakiwi kunyimwa haki zao za huduma ya afya am-bayo ni muhimu kwa ajili ya kuendelea kuishi katika jamii na wanatakiwa kupewa matibabu maalum ku-wawezesha kufikia kiwango cha juu cha afya. Ni lazima nchi iweke masharti kuwezesha watu ambao wamewekwa kizuizini kimakosa na ambao haki zao zimekiukwa kupata msaada wa kisheria na kutafuta nafuu.

> 'Haki ya utu ni haki ya asili ya msingi ambayo binadamu wote bila kujali uwezo wao wa akili au ulemavu wao kama mazingira yatakavyokuwa wanastahiki kuipata bila ubaguzi' (Shauri la *Purohit*, aya ya 57)

Tume ilieleza kwamba haki ya afya ni muhimu kwa ajili ya kufurahia haki zote nyingine na inajumuisha haki ya kufikia vituo vya huduma za afya na huduma za afya bila ubaguzi. Aidha, Tume pia iliikumbusha

nchi kama zinajukumu la kuhakikisha kwamba wagonjwa wa afya ya akili wanapewa matibabu maalum kwa hali yao.

Nchi pia ina wajibu wa kuchukua hatua 'thabiti na zenye malengo' kuhakikisha upatikanaji kamili wa haki ya afya. Tume ilibaini kwamba serikali ilikiuka Mkataba na iliihimiza kufuta sheria ya uzuizi wa wagonjwa wa afya ya akili na kutoa matibabu ya kutosha na huduma ya vifaa kwa ajili ya watu wenye ugonjwa wa afya ya akili.

- ***Open Society Justice Initiative dhidi ya Côte d'Ivoire (Mawasiliano Na. 318/06)***

Mawasiliano yaliwasilishwa na Open Society Justice Initiative dhidi ya nchi ya Côte d'Ivoire. Katika malalamiko ilidaiwa kwamba kuanzishwa kwa dhana ya 'ivoirité' na Rais Henri Konan Bédié kuna maanisha utaifa wa Côte d'Ivoire unaweza kupatikana tu kwa watu ambao wamezaliwa Ivory Coast/ Côte d'Ivoire na wazazi wawili wa Ivory Coast/Côte d'Ivoire. Sera hii iliathiri asilimia 30 ya idadi ya watu na ikijumuisha ambao wamezaliwa Ivory Coast/Côte d'Ivoire na ambao wamekua na kuishi nchini kwa kipindi chote cha maisha yao. Hii ilisababisha kutengwa kisiasa na kijamii kupitia zuio la upatikanaji wa ardhi, kupiga kura na kushika ofisi ya umma. Kwa mujibu wa mawasiliano, sheria za kibaguzi zilisababisha kunyimwa haki ya utaifa, na mara nyingi kutokuwa na utaifa au kuwa katika hatari ya kutokuwa na utaifa hivyo kuzuia kutambuliwa hadhi ya kisheria kwa maelfu ya wa-ivory, kupoteza fursa za ajira na ukiukaji wa haki ya kumiliki mali.

Katika kupitisha tafsiri ya hali ya kutokuwa na utaifa kama ilivyotafsiriwa katika ibara ya 1 ya Mkataba kuhusu Hadhi ya Watu wasiokuwa na Utaifa wa mwaka 1954, Tume ilihitimisha kwamba nchi ina wajibu wa kuwapa utaifa watu wanaodai kuzaliwa katika ardhi yake, isipokuwa kama nchi haiwezi kuthibitisha kwamba mtu husika tayari anautaifa au anastahiki kupata utaifa wa nchi nyingine. Tume ilisisitiza kwamba utaifa una dhana mbili; hadhi ya utaifa kutokana na mazingira au hali ya muda mfupi (de facto) na hadhi ya utaifa kwa mujibu wa sheri (de jure) ili mtu aelewe lazima atumie lenzi ya kijamii na kisiasa. Pia Tume ilieleza kwamba, utaifa katika muktadha wa kisheria maana yake ni ushirikishaji wa kisheria wa mtu kwa jamii ikijumuisha nchi au hadhi ya mtu anayeishi katika nchi kutokana na uhusiano wake wa kisiasa na kisheria.

Tume ilikuwa na maoni kwamba masharti ya sheria kwa ajili ya mtu kupata utaifa hayana mantiki na hivyo hayaendani na haki ya

utaifa inayolindwa na ibara ya 5 ya Mkataba. Pia Tume ilizingatia kwamba haki zingine zinalizolindwa na Mkataba zina uhusiano wa hali ya juu na zinategemeana na haki ya utu.

Vilevile, Tume ilieleza kwamba kuwa mhamiaji asiye na nyaraka hutambuliwa kama ni miongoni mwa hadhi ya chini ya utambulisho katika mfumo wa sheria, siasa na jamii. Tume ilihitimisha kwamba sheria na hati za nchi zinakiuka masharti ya ibara ya 5 ya Mkataba kuhusu haki ya utu wa binadamu. Ilibainika nchi inayojibu mawasiliano imekiuka haki ya maendeleo, ajira na usawa.

- ***Institute for Human Rights and Development na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Mawasiliano Na. 393/10 (2016)***

Shauri hili lililetwa mbele ya Tume ya Afrika na taasisi tatu zisizo za kiserikali kwa niaba ya watu binafsi na familia zaidi ya saba zilizolalamikia ukiukwaji wa haki za binadamu zinazolindwa na Mkataba wa Afrika. Ukiukwaji huu ulifanyi-ka katika muktadha wa shughuli za kijeshi. Kikosi cha Wanajeshi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (The Armed Forces of the Democratic Republic of Congo) kinalalamikiwa kwa ukamataji holela, uporaji, utesaji, unyanyasaji na udhalilishaji, mauaji ya kinyama na mauaji ya nje ya mfumo wa sheria wakati wa makabiliano ya kijeshi na kikundi cha waasi katika mji wa Kilwa. Cha kushangaza, wadai walidai kwamba Kampuni ya kimataifa ya uziduaji ya Anvil Mining ya Australia, walihamasisha ukiukwaji huo kwa kulisaidia jeshi la serikali katika kuking'oa kikundi cha waasi kilichokuwepo Kilwa.

Katika uamuzi wake, Tume ilibaini kwamba Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ilishindwa kuhakikisha kwamba mawakala wake, jeshi la taifa na kam-puni ya kimataifa, inaheshimu Mkataba. Mkataba unaipa wajibu nchi kuchukua hatua zinazofaa kuhakikisha ulinzi wa watu binafsi dhidi ya ukiukwaji uliofany-wa na watendaji wasio serikali. Hatua hizi, kama Tume ilivyobaini, zingeju-muisha zile ambazo Serikali ingezichukua kuiadhibu kampuni ya kimataifa na jeshi lake pia kuhakikisha kwamba waathiriwa wa ukiukwaji wa haki za binadamu wanalipwa fidia. Hoja kwamba kampuni za kimataifa siyo wahusika katika Mkataba wa Afrika ingeweza kusababisha Tume kutotamka bayana kwamba Kampuni ya Uchimbaji ya Anvil imekiuka haki kadhaa chini ya Mkataba wa Afrika. Hata hivyo, Tume ilirudia msimamo wake wa awali kwamba kampuni inayojihusisha katika sekta ya uziduaji inawajibika kuheshimu haki za wazawa katika kutekeleza shughuli zake. Hii inazuia wazi kampuni kujihusisha moja kwa moja na kukiuka haki

za jamii za wazawa na kufanya hivyo kwa namna nyingine kwa kuwaunga mkono au kuhamasisha wanaokiuka haki hizo.

Hakuna mkataba wa kimataifa unaotoa majukumu ya wazi ya kuheshimu haki za binadamu kwa kampuni. Wakati mchakato wa kufanya hivyo unakuja katika ngazi ya dunia, ufafanuzi wa Tume unaongeza suala la uendeshaji wa shughuli ambao unaendana na viwango vya msingi vya haki za binadamu kati-ka kundi la mila zisizo na nguvu ya kisheria.

Tume pia ilizungumzia masuala yanayohusika na haki ya maendeleo ambayo waleta maombi walilalamika imekiukwa na Serikali. Haki ya maendeleo ni miongoni mwa ubunifu wa msingi wa Mkataba wa Afrika. Japo kuwa haki ya maendeleo huhusishwa na dhana ya haki za watu ambayo ndiyo msingi mkuu wa Mkataba wa Afrika, Tume inaonesha kwamba haki ya maendeleo inaweza kufurahiwa na watu binafsi. Uwili huu 'ya mtu binafsi' na 'ya makundi' ni kipengele cha haki ya maendeleo katika ibara ya 22 ikijumuisha vipengele vya maendeleo ya kiuchumi na kiutamaduni. Katika mazingira haya Tume ilibaini kwamba haki ya maendeleo ya kiuchumi ya watu wa Kilwa imekiukwa kwa ubomoaji wa miundombinu binafsi na ya jamii kama vile shule, vituo vya afya ambavyo viliingiza kipato kwa ajili ya watu binafsi au vilitumika kwa ajili ya ustawi wa jamii. Kipengele cha utamaduni katika haki ya maendeleo pia kilikiukwa wakati watu wanazikwa katika makaburi ya pamoja, wanakosa mazishi yenye heshima na familia zao zinashindwa kufanya matambiko ya kiutamaduni zao kama inavyotambulika katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

- ***Kevin Mgwanga Gunme na Wenzake dhidi ya Kameruni* (Mawasiliano Na. 266/03)**

Mawasiliano haya yaliletwa na watu binafsi 14 kwa niaba ya Watu wa Kusini ya Kameruni. Ukiukwaji haki unaolalamikiwa ulianza kipindi baada ya Kamer-uni kupata uhuru. Kwa sababu Kusini ya Kameruni ilikua eneo lililo chini ya Dhamana ya Umoja wa Mataifa likitawaliwa na Uingereza tofauti na sehemu ya Francophone ya Kameruni, wakati wa kura ya maoni ya Umoja wa Mataifa mwaka 1961 walipewa "njia mbadala mbili". Njia hizi zilikua ni kuamua kujiunga na Nigeria au Kameruni na walichagua Kameruni. Walalamikaji wanadai kuwa walinyimwa njia mbadala ya tatu ambayo ilikuwa ni kupata uhu-ru, taifa na uhuru wa kujiamulia. Wanadai kwamba haki za binadamu za wakameruni zimekua zikikiukwa na nchi inayojibu mawasiliano, pamoja na ukamataji holela, kuwekwa kizuizini kuteswa na kuuawa kwa watu ambao wa

wanatetea uhuru wa Kameruni ya Kusini.

Katika uamuzi wake wa Tume ilibaini kwamba Kameruni imeshindwa kutatua changamoto za biashara za wakameruni ya Kusini chini ya Mkataba wa Kulin-ganisha Sheria za Biashara za Afrika ambao ulitaka katiba ya kampuni kuwa katika lugha ya kingereza. Hii ilipelekea ukiukwaji wa ibara ya 2 ya Mkataba wa Afrika. Aidha, Tume pia ilibaini kwamba nchi inayojibu mawasiliano ime-kiuka haki ya kuishi, misingi isiyokiukwa ya binadamu na utu wa mtu. Haki ya kuteswa, adhabu na utendewaji wa kikatili, kinyama na kudhalilisha pia ulibain-ikia umekiukwa.

Hata hivyo Tume ilijizuia kutoa maamuzi juu ya suala la kura ya maoni za Umoja wa Mataifa mwaka 1961, kuhusu matukio yaliyofanyika Oktoba 1961 na 1972 kwasababu yalifanyika kabla Mkataba haujanza kutumika. Wakati Tume inasita kutafsiri dhana ya 'haki za makundi 'ilitamka kwamba lengo la haki za makundi ni sawa na lengo za haki za watu binafsi na zinahitaji kulindwa. Hivyo ilihitimisha kwa kwamba watu wa Ka-meruni ya Kusini wanaweza kudai kuwa wao ni kundi la watu kwasababu wanaonesha sifa kadhaa na undugu ikijumuisha historia inayofanana, lugha na mila.

Tume ilibaini kwamba Mkataba wa Afrika hauwezi kutumiwa na mlalamikaji kutishia uhuru na uadilifu wa nchi mwanachama. Hivyo basi ilieleza kwamba ili kuwe na ukiukwaji wa uhuru wa kujiamulia chini ya Mkataba wa Afrika ni lazima kuwe na ushahidi wa kutosha wa haki za binadamu kiasi kwamba uadilifu katika nchi uwe ni changamoto na nchi mwanachama sambamba na kuwanyima watu haki yao ya kushiriki katika serikali kama inavyolindwa na ibara 13(1). Aidha, Tume iliamua kwamba ukiukwaji wa uhuru wa kujiamulia inabidi ukidhi masharti mawili chini ya ibara ya 20 (2) ambayo ni ukandamizaji na utawala.

## Uwasilishaji wa ripoti ya nchi

Uwasilishaji wa ripoti ya nchi ni moja wapo ya njia za kupima utekelezaji wa wajibu wa Serikali chini ya Mkataba. Ibara ya 62 ya Mkataba unazitaka nchi kuwasilisha ripoti yake ya muhula kwa Tume. Katika kutekeleza ibara hiyo ya Mkataba, mwezi Oktoba mwaka 1988 Tume ilipitisha mwongozo wa jumla kuhusu muundo na maudhui ya ripoti ya nchi. Mwaka 1998 Tume ilitoa Mwongozo mfupi wa Kuandaa Ripoti ya Muhula.

Ibara ya 26 ya Itifaki ya Wanawake pia inazitaka nchi wanachama wa Itifaki kujumuisha katika ripoti yake ya muhula kwa Tume kwa mujibu wa ibara ya 62 ya mkataba, ripoti kuhusu kutunga sheria na hatua zingine zilizochukuliwa katika kutekeleza masharti ya Itifaki. Hivyo, ripoti ya nchi wanachama katika mkataba na Itifaki ya Wanawake lazima itakua na sehemu mbili, sehemu ya kwanza (Sehemu A) inahusu Mkataba na ya pili (Sehemu B) ya Itifaki. Mwaka 2009, Tume ya Afrika ilipitisha Mwongozo kwa ajili ya Kuwasilisha Taarifa kuhusu Itifaki ya Wanawake na mwaka 2010 Mwongozo kwa ajili ya Kuwasi-lisha Ripoti ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni.

Sehemu C ya ripoti ya nchi ya Kameruni inaelezea utekelezaji wa haki zilizoelezwa katika Mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu ulinzi na Msaada wa Watu waliolazimika Kuhama makazi ndani ya nchi (Mkataba wa Kampala).

- Kameruni ilichukua hatua ya kutunga sheria kuhakikisha ulinzi wa kisiasa kwa wananchi wake. Hii inajumuisha , pamoja na masuala mengine, Sheria Na. 96/12 ya tarehe 5 Agosti mwaka 1996 kuweka mfumo wa utunzaji wa mazingira nchini Kameruni, Sheria Na. 86/16 ya tarehe 6 Disemba 1986 kuandaa upya ulinzi wa haki za kiraia nchini Kameruni.
- Kuhusu fedha zilizotengwa kusimamia watu waliohamishwa, Serikali ilipata kiasi cha fedha kipatacho 'Yuro' 3,587,786,25 kupitia mshikamano wa kitaifa kuelekea bajeti ya Serikali.
- Aidha, Kameruni ilichukua hatua za kuzuia uhamishaji wa ndani ya nchi kupitia kukuza mazingira yanayofaa kwa ajili ya shughuli za haki za binadamu katika nchi, serikali pia ilianzisha mfumo wa tahadhari kuwezesha mashirika ya wazawa kugundua hatari zinazosababishwa na asili na binadamu. Kituo cha Taifa cha Uendeshaji cha Dharura kilianzishwa huko Yaoundé ili kufanya kazi kama kituo mbadala cha Kituo cha Taifa.
- Kameruni imechukua hatua mahususi katika kuzuia uhamaji wa ndani ya nchi kupitia kwa mfano, uhamaji wa ndani ya nchi kwa ajili ya mabadiliko ya hali ya hewa yanayotarajiwa, serikali imechukua hatua za kisheria na ki-taasisi kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa yanayohusu athari za mazingira katika njia endelevu.

Utaratibu wa uwasilishaji wa ripoti ya nchi unatumika kama jukwaa la majadiliano yenye tija. Utaratibu huu unaiwezesha Tume kusimamia utekelezaji wa Mkataba na kutambua changamoto zinazokwamisha kufikiwa kwa malengo ya Mkataba. Nchi zinaweza kutathmini mafanikia yao na changamoto katika Mkataba

Mkataba unazitaka nchi kuwasilisha aina mbili za ripoti: ripoti za awali na ripoti za muhula. Ripoti za awali zinatakiwa kuwasilishwa

na nchi miaka miwili tangu kuridhia au kukubali Ripoti za muhula zinatakiwa kuwasi-lishwa kila baada ya miaka miwili, baada ya kuwasilisha ripoti ya awali.

## Maudhui ya Ripoti ya Nchi kuhusu Mkataba wa Afrika

Ripoti ya nchi inayowasiliswa na nchi mwanachama lazima ieleze yafuatayo:

- Hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza masharti yaliyomo katika mkataba
- Maendeleo yaliyopatikana hadi wakati huo
- Changamoto zinazoathiri utekelezaji wa Mkataba na nyaraka nyingine za nyongeza zinazohusika

Nchi zinatakiwa kuwasilisha taarifa chini ya Mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu Ulinzi na Msaada wa Watu Waliolazimika Kuhama Makazi Ndani ya Nchi (ibara ya 14 (4) ya Mkataba wa Kampala). Nchi ambazo zim-eridhia Mkataba wa Afrika na Itifaki ya Maputo zinatakiwa kuwasilisha ripoti yenye sehemu tatu, kila sehemu moja ikihusika na mkataba mmoja. Mpaka sasa ni nchi ya Kameruni tu imefanya hivyo.

Nchi inatakiwa kueleza utekelezaji wa masharti ya Itifaki ya Maputo kama imeridhia kulingana na Mwongozo wa Tume wa kwa ajili ya nchi kuwasilisha taarifa chini ya Itifaki ya Maputo.

## Faida ya uwasilishaji wa ripoti ya nchi katika Itifaki ya Maputo

- Uwasilishaji ripoti huisaidia Tume kutimiza jukumu lake la uangalizi wa kusimamia utekelezaji wa Itifaki.
- Uwasilishaji wa Ripoti za nchi huipa nafasi nchi mwanachama kuonesha hatua zilizochukuliwa kutekeleza itifaki, pamoja na sababu na changamoto zinazozuia utekelezaji wa Itifaki wenye ufanisi.
- Mchakato wa kuwasilisha unaiwezesha Tume kukusanya taarifa na uzoefu uliojitokeza katika nchi nyingi kutoka nchi kuhusu haki za wanawake katika Afrika.
- Baada ya kuzingatia ripoti hizi, Tume ya Afrika hutoa hitimisho na mapendekezo ambayo nchi wanachama wanatarajiwa kuyatekeleza ili kuboresha upatikanaji wa haki za wanawake.
- Uwasilishaji ripoti wa nchi hutoa namna ambayo Tume hupata taarifa za kuaminika na taswira ya kuaminika ya hali ya haki za binadamu katika nchi.

- Uwasilishaji wa ripoti ya nchi huisaidia Tume katika mazungumzo yake na mijadala na nchi wanachama kuhusu kuzingatia ripoti.

## Baadhi ya hatua na mifumo iliyopitishwa na nchi

Katika kutekeleza haki zilizotajwa katika Itifaki ya Maputi, katika ripoti yake ya muhula ya Mei 2015 hadi Machi 2019 Malawi inaonyesha ilichukua hatua zifuatazo:

- Sheria ya Usawa wa Kijinsia ilipitishwa kufanya udhalilishaji wa kijinsia kuwa kosa la jinai na mtu akikutwa na hatia atahukumiwa kifungo cha hadi miaka mitano jela na kutoa fidia.
- Katika ngazi ya sera, Mpango wa Taifa wa Kupambana na Ukatili wa Kijinsia (2014-2020) ulipitishwa
- Malawi ilianzisha kituo kimoja kwa ajili ya kusaidia waathiriwa wa ukatili wa kijinsia kwa kutoa ushauri nasaha, matibabu na mahitaji ya kisaikolojia na ya kijamii.
- Mwaka 2016 kulikua na hukumu iliyotokana na kosa la kudhuru kinyume na kifungu cha 5 cha Sheria ya Usawa wa Kijinsia.

Katika ripoti yake ya awali chini ya Itifaki ya Maputo (2015), Afrika Kusini ilionesha kwamba ilichukua hatua zifuatazo:

- Kuhusu haki ya kuishi, uadilifu na usalama wa mtu, serikali imepitisha mfumo wa sheria unaolenga kupambana, kuzuia, kuondoa na kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake. Hii inajumuisha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (1997), Sheria Dhidi ya Unyanyasaji Majumbani (1998) ambayo ililenga kuwalinda wanawake kwa kuongeza mawanda ya nini kinajumuisha mahusiano ya nyumbani na vitendo vya unyanyasaji majumbani, Sheria ya Ulinzi dhidi ya Unyanyasaji ya mwaka 2011, ambayo inalenga kuwaweka huru waathiriwa wote wa unyanyasaji kutoka sehemu za umma au binafsi.
- Katika nia ya kukuza haki ya elimu na mafunzo, Afrika Kusini ilipitisha Sheria ya Sera ya Taifa ya Elimu ya mwaka 1996 na Sheria ya Shule za Afrika Kusini ya mwaka 1996, kukuza upatikanaji wa elimu kwa wote. Sheria ya Shule za Afrika Kusini ilifanya kusoma kuwa lazima kwa watoto wa kuanzia miaka saba hadi 15.
- Majibu ya serikali yanajumuisha mpango wa kuunda upya mfumo wa huduma ya afya kwa kuboresha vita dhidi ya UKIMWI na Kifua Kikuu na magonjwa mengine yasiyoambukizwa, kuratibu gharama na kufanya huduma ya afya kuwa nafuu kwa wote.
- Serikali pia inafanyia kazi uboreshaji wa upatikanaji na matumizi za dawa za uzazi wa mpango kwa wanawake. Kutokana na hali hii, Sera ya Taifa ya a Uzazi wa Mpango na Uzazi Salama iliyohuishwa iliidhinishwa na Halmas-hauri ya Taifa ya Afya mwaka 2012/2013.
- Hatua zifuatazo zilichukuliwa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kutekeleza haki zilizotolewa chini ya Itifaki ya Maputo:

- Sambamba na kukuza na kulinda haki za kichumi na kijamii, Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo imepitisha sheria kadhaa kuhakikisha ulinzi wa haki za wanawake kwa mfano Sheria Na. 015/2002 ya tarehe 16 Oktoba 2002, kuhusu Kanuni za Kazi ambayo ina masharti muhimu kwa ajili ya kulinda wanawake walioajiriwa.
- Hatua nyingine za kisheria ni Amri ya Sheria ya mwaka 1961 ambayo ilirekebishwa ili kuanzisha kuanzisha mfumo wa hifadhi ya jamii.
- Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo imepitisha sera na programu kwa ajili ya hatua za kitawala na kutunga sheria kukuza ustawi wa wanawake kama vile; Sera ya Taifa ya Jinsia, Sera ya Taifa ya Ajira na Mafunzo ya Ufundi Stadi ya mwaka 2015, Sera ya Taifa ya Vijana na Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Kupambana na aina mbaya zaidi za Ajira ya Mtoto ya mwaka 2011 pamoja na nyinginezo.
- Kuhusu utoaji wa huduma za afya ya uzazi ikijumuisha kupunguza idadi ya vifo vya wanawake na watoto wakati wa kujifungua, Serikali ya Jamhuri ya Kongo, kupitia Wizara ya Afya, imeanzisha programu ya Taifa ya afya ya Uzazi iliyopewa jukumu la kutekeleza Sera ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kuhusu afya ya uzazi.

## Changamoto za uwasilishaji wa ripoti ya nchi

Kwa Tume ya Afrika

- Kutokujibu kwa nchi. Hakuna adhabu/motisha kwa nchi kuwasilisha taarifa zake. Nchi sita wanachama wa Mkataba wa Afrika hawajawahi kuwasilisha taarifa za nchi zao kwa Tume ya Afrika.
- Ingawa utaratibu wa nchi kuwasilisha ripoti unaruhusu Tume kutumia mamlaka yake ya usimamizi, mara kadhaa nchi wanachama wanasita kutoa taarifa wanazoombwa ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Mara nyingi Tume hurudia ombi lake kwa ajili ya taarifa za ziada na ufafanuzi kutoka kwa nchi.
- Tume pia inakabiliwa na changamoto ya kiutendaji kwa kukosa mamlaka ya kutosha ya kutekeleza maoni na mapendekezo yake sababu havina nguvu ya kisheria. Nchi pia zinaweza kuamua kutokutekeleza maoni na mapendekezo haya ikiwa kuna utashi duni wa kisiasa.

Kwa nchi wanachama:

- Nchi zinakosa rasilimali za kitaasisi na kifedha kutekeleza mapendekezo kutoka hitimisho linalojumuishwa katika ripoti ya serikali/ripoti ya nchi. Ukosefu wa uratibu ndani ya wizara za serikali, maana yake ni kwamba utekelezaji wa baadhi ya mapendekezo ya serikali utachukua muda kabla ya utekelezaji na baadhi ya nchi zinahitaji ushauri toka wizara mbalimbali kabla sheria haijafutwa.
- Katika kutoa baadhi ya mapendekezo na maoni ya kuhitimisha, Tume mara chache huzingatia changamoto za kisiasa na kipindi ambacho kinaweza hitajika.

## Utaratibu wa nchi kuwasilisha ripoti

Uwasilishaji wa ripoti hupitia hatua zifuatazo:

Nchi kuwasilisha ripoti kwa Sekretarieti ya Tume ya Afrika.

Sekretarieti huweka ripoti katika tovuti ya Tume, ikionesha wakati gani ripoti hiyo itashughulikiwa.

Nakala za ripoti zinasambazwa kwa makamishina na taasisi zisizo za kiserikali zinazohusika.

Wadau wanaotaka kuchangia uchunguzi wa ripoti huwasilisha michango yao ikiwemo ripoti kivuli kwa Sekretarieti ya Tume angalalu siku 60 kabla ya tarehe iliyopangwa kwa ajili ya uchunguzi wa ripoti hiyo.

Sekretarieti wanaweza kuwaalika taasisi maalum kuwasilisha taarifa inayohusiana na ripoti.

Sekretarieti inaweza kuandaa maswali kutokana na ripoti.

Kuwasilisha maswali kwa makamishina wote.

Tume inawasilisha maswali kwa kwa nchi inayowasilisha taarifa (barua ya kuiomba nchi kutuma wawakilishi wake kuhudhuria ikiambatishwa).

Tume inachunguza ripoti ya nchi katika kikao cha wazi kama ilivyopangwa: uwasilishaji ripoti na mwakilishi wa nchi, maswali kutoka kwa makamishina, majibu ya maswali kutoka kwa ujumbe wa nchi (wakati mwengine hongezewa na majibu ya maandishi), (muhtasari, na hitimisho na mwenyekiti wa Tume).

Kisha Tume itapitisha hitimisho (katika kikao cha faragha).

## Maoni ya Kuhitimisha

Mwaka 2001, Tume ilianza kupitisha hitimisho baada ya kujadili ripoti ya nchi. Hitimisho huzungumzia athari chanya na hasi ambazo zimejitokeza kupitia mjadala wa ripoti. Hitimisho hubainisha hatua ambazo nchi itazichukua kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa.

# Viziduo vya maoni ya hitimisho ya Ripoti ya Muhula wa Kwanza ya Jamhuri ya Afrika Kusini (imetolewa katika kikao cha 38 cha Tume mwaka 2005):

> 'Tume ya Afrika inapendekeza kwamba Serikali ya Afrika Kusini:
>
> 28. Ihakikishe kwamba masharti ya Mkataba wa Afrika yanajulikana na kueleweka na watu wazima na watoto maeneo yote ya mijini na vijijini.
>
> 29. Kufikiria kuondoa iliyofanywa katika ibara ya 6(d) ya Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu Kuhusu Haki za Wanawake katika Afrika.
>
> 35. Kutoa Tamko chini ya Ibara ya 34 (6) ya Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Uanzishaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.
>
> 38. Kuijulisha Tume ya Afrika, katika ripoti yake ya mhula unaofuata, hatua ilizochukua kutatua changamoto, na pia namna ilivyotekeleza mapendekezo yote katika hitimisho hili.

## Ufuatiliaji

Ni jukumu la makamishina kama sehemu yao ya kukuza mamlaka kuhakikisha ufuatiliaji wa mapendekezo yanayotokana na Hitimisho. Pia hupeleka kwa Bunge la Umoja wa Afrika hitimisho lake likiambatishwa na nakala za ripoti za nchi zilizowasilishwa kwa Tume pamoja na majibu ya maswali ya nchi zilizowasilisha ripoti yaliyoulizwa wakati wa kujadili ripoti.

Endapo wawakilishi wa nchi husika hawawezi kutoa majibu ya kuridhisha kuhusu swali moja au zaidi yaliyoulizwa kwao na Tume wakati wa kushughulikia ripoti yao, Tume huandika barua

ya ufuatiliaji kwa nchi husika kuomba taarifa za nyongeza kuhusu swali hilo (maswali hayo).

Kanuni za Utaratibu za Tume ya Afrika Kuhusu Haki za Binadamu na Watu za mwaka 2020 zinaweka utaratibu wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maoni ya Hitimisho chini ya Kanuni ya 83:

- Tume itaainisha hoja ambazo zinahitaji umakini maalum kwa upande wa Nchi Mwanachama katika Maoni ya Hitimisho.
- Tarehe Nchi Mwanachama kuwasilisha Ripoti ya Muhula itajumuishwa pia katika Hitimisho.
- Wajumbe wa Tume wana mamlaka ya kuhakikisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo kutoka katika hitimisho ndani ya mfumo wao wa kukuza shughuli kwa Nchi Mwanachama inayohusika.
- Wanachama wanaweza kuomba au kuzingatia michango ya wahusika wenye maslahi au taasisi zilizoalikwa, kwa kadri ambavyo mapendekezo hayo yametekelezwa.
- Tume inaweza kurejea Hitimisho lolote katika Ripoti ya Shughuli zake kwa Baraza.

### Kupitia ripoti bila uwakilshi wa nchi

Katika mazingira ambayo nchi imeshindwa kutuma mwakilishi yeyote baada ya kutaarifiwa mara mbili, Tume inaweza kuendelea na upitiaji wa ripoti na kupeleka maoni yake kwa nchi.

### Kutokuwasilisha ripoti

Ni wajibu wa Katibu kuijulisha Tume kuhusu kutokuwasilishwa kwa ripoti na nchi mwanachama. Ukumbusho hutumwa kwa nchi mwanachama yoyote inayohusika kila miezi mitatu na orodha nchi ambazo hazijawasilisha ripoti huambatishwa katika Ripoti ya Shughuli za Tume.

## Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Tume ya Afrika

Tume ina uhusiano mzuri sana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Ibara ya 45 (1) ya Mkataba inazitaka Tume kushirikiana na taasisi zingine za kimataifa za Afrika zinazohusika na kukuza na kulinda haki za binadamu na watu. Kuanzia mwaka 1988, Tume imekua ikitoa hadhi ya uangalizi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Mwaka 1999, Tume ilipitisha uamuzi kuhusu vigezo kwa ajili ya kutoa hadhi ya uangalizi. Mnamo mwaka 2016, Azimio Namba 361

kuhusu Vigezo kwa ajili ya Kutoa na Kutunza Hadhi ya Uangalizi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofaya kazi za Haki za Binadamu na Watu katika Afrika lilipitishwa kuanzisha uwezo kuamua mamlaka ya Tume kama ilivyoelezwa chini ya ibara ya 45 ya Mkataba wa Afrika.

Hadi kufikia Juni 2021, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 535 yalikuwa yamepewa hadhi ya uangalizi na Tume.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu muhimu katika shughuli za Tume. Huijulisha Tume kuhusu ukiukwaji wa Mkataba, kupeleka mawasiliano kwa niaba ya watu binafsi, kusimamia nchi wanachama kutekeleza mkataba, na kusaidia kuongeza uelewa kuhusu shughuli za Tume kwa kuandaa mikutano na shughuli nyingine. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hushiriki katika mikutano ya Tume na kuhusika katika utaratibu wa kuwasilisha tipoti kwa kuwasilisha ripoti kivuli na kueneza hitimisho. Mashirika yasiyo ya kiserikali yenye hadhi ya uangalizi yanaweza kupewa nafasi wakati wa vikao vya wazi wote. Pia watakiwa kuwasilisha ripoti ya shughuli zao za mwaka katika kila miaka miwili.

Mahusiano kati Mashirikia yasiyo ya kiserikali na Tume huratibiwa na kuongozwa na Jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambalo hufanyika kabla ya kila kikao cha Tume kuamua na kuandaa ripoti kuhusu mada na hali katika kanda ya Afrika. Jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali huandaliwa na *Banjul based African Center for Democracy and Human Rights Studies*, linatumika kama njia ambayo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hupatata uzoefu kuhusu shughuli za Tume. Mashirikia Yasiyo ya Kiserikali pia mara nyingi hujadiliwa na makamishina wakati wa hotuba ya ufunguzi ya kila kikao.

**Vigezo vya kutoa hadhi ya uangalizi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

Kupewa hadhi ya uangalizi Shirika Lisilo la Kiserikali hutakiwa kuwa na vigezo vifuatavyo:

(i) Malengo ya Shirika Lisilokuwa la Kiserikali lazima yaendane na kanuni za Sheria ya Uendeshaji ya Umoja wa Afrika na Mkataba wa Afrika;

(ii) Shirika lisilo la kiserikali lazima liwe linafanya kazi katia masuala ya haki za binadamu

(iii) Maombi kwa njia ya maandishi kwa sekretariati lazima yaambatishwe na:

- Ushahidi kama ipo kisheria, orodha ya wanachama, vitengo vya shirika na chanzo cha mapato
- Tamko la vyanzo vya mapato
- Taarifa ya fedha ya mwisho

## Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu na Tume ya Afrika

Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu ni taasisi za kisheria zinazoanzishwa na serikali katika bara la Afrika na kupewa jukumu la kukuza na kulinda taasisi zinazohusika na haki za binadamu katika nchi zao. Uanzishaji na utendaji wa taasisi hii lazima uendane na Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusiana na Hadhi na Utendaji wa Taasisi za Kitaifa kwa ajili ya Kukuza na Kulinda Haki za Binadamu ambazo pia huitwa 'Kanuni za Paris'.

Uhusiano kati ya Tume na Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu yalianza mwaka 1998 ambapo Tume ilipitisha Azimio kuhusu Kutoa Hadhi ya Kushirikishwa kwa Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu. Azimio lilitoa vigezo kwa ajili ya kutoa hadhi ya kushirikishwa kwa Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu.

**Kupewa hadhi ya kushirikishwa ni lazima Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu ikidhi vigezo vifuatavyo:**

- Ni lazima iwe Taasisi ya kitaifa ya haki za binadamu katika nchi mwanachama kwenye Mkataba.
- Lazima iwe imeanzishwa kwa mujibu wa sheria.
- Lazima ishabihiane na Kanuni za Paris.
- Lazima iombe rasmi kwa Tume hadhi ya kushirikishwa.

Msingi wa uhusiano kati ya Tume na Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu yanatokana na ibara za 26 na 45 (1) za Mkataba wa Afrika. Utoaji wa hadhi ya ushirikiano kwa Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu imekuza ushirikiano wa pamoja kati ya Tume na Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu. Ingawa haki na wajibu wa Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu shirikishi zinafana katika baadhi ya masuala na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yenye hadhi ya uangalizi, Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu vile vile zinatakiwa kuisaidia Tume kukuza haki za binadamu katika ngazi ya taifa. Kwa mfano, Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu zimehimiza nchi zao kuridhia mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu. Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu zina dhima muhimu katika kuongeza uelewa wa shughuli za Tume za kukuza na kulinda haki za binadamu. Taasisi za haki za binadamu za taifa zenye ushirikiano na Tume zinastahili kuhudhuria na kushiriki katika vikao vya wazi vya Tume. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanatakiwa kuwasilisha ripoti kuhusu shughuli zake kwa Tume kila baada ya miaka miwili. Kanuni ya 79 ya Kanuni za Utaratibu wa Tume ya Afrika zinaeleza kwamba hitimisho la ripoti za nchi litapelekwa Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu pamoja na serikali.

> Hadi mwezi Juni 2021, Tume ilikuwa imetoa hadhi ya ushirikiano kwa Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu 30. Orodha ya Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu zenye hadhi ya ushirikiano na Tume inapatikana katika https://www.achpr.org/sessions/info?id=367

## Mifumo maalum ya Tume

Kwa miaka mingi Tume imeanzisha mfumo maalum unaojumuisha makatibu maalum na Vikosi-Kazi. Wakati Tume haina mamlaka iliyoeleza dhahiri ya kuanzisha mifumo hii, mamlaka yake ya kufanya hivyo, inatokana na mamlaka yake pana ya kukuza haki za binadamu (katika ibara ya 45 ya Mkataba) na mamlaka yake ya kutumia njia yoyote ya uchunguzi inayofaa katika kutekeleza majukumu yake (chini ya ibara ya 46 ya Mkataba). Mifumo maalum ya kuchunguza ukiukwaji wa haki za binadamu, utafiti wa masuala ya haki za binadamu na kutekeleza shughuli za kukuza haki za binadamu kupitia ujumbe. Ripoti zao zinaunda msingi wa baadhi ya maazimio ya Tume. Makatibu Maalum huteuliwa miongoni mwa wajumbe wa Tume, wakati wanafanya kazi Vikosi-Kazi hujumuisha wajumbe wa Tume pamoja na wataalam huru.

## Mifumo maalum chini Mfumo wa Afrika wa haki za binadamu

| Mwaka | Mfumo |
| --- | --- |
| 1996 | • Katibu Maalum wa Wafungwa, Hali za Magereza na Sera katika Afrika |
| 1999 | • Katibu Maalum wa Haki za Wanawake |
| 2000 | • Kikosi -Kazi kuhusu Jamii za Wazawa katika Afrika |
| 2004 | • Katibu Maalum wa Uhuru wa Kujieleza na Kupata Habari<br>• Katibu Maalum wa Watetezi wa Haki za Binadamu<br>• Katibu Maalum wa Wakimbizi, Wahamiaji na Watu Waliolazimika Kuhama Makazi Ndani ya Nchi<br>• Kamati ya Kuzuia Mateso katika Afrika<br>• Kikosi -Kazi cha Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni |
| 2005 | • Kikosi- Kazi kuhusu Adhabu ya Kifo na Nje ya Utaratibu wa Kisheria, Muhtasari wa Mauaji Holela katika Afrika |
| 2007 | • Kikosi- Kazi kuhusu Haki za Wazee na Watu wenye Ulemavu |
| 2009 | • Kikosi -Kazi cha Sekta ya Uziduaji, Mazingira na Ukiukwaji wa Haki za Binadamu. |
| 2010 | • Kamati ya Ulinzi wa Haki za Binadamu na Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi na Walio Katika Mazingira Hatarishi na Walioathirika na Virusi vya Ukimwi |

## Changamoto Zinazoukabili Mfumo Maalum

- Makamishina hufanya kazi pia kama Makatibu Maalum. Inalalamikiwa kwamba jukumu hili la nyongeza huwapunguzia makamishina uwezo wa kutekeleza mamlaka yao yote kwasababu ya changamoto ya muda.
- Rasilimali hazitoshi kufanya shughuli zote zinazotakiwa.
- Idhini ya nchi inahitajika katika kutembelea nchi hata hivyo mara nyingi huwa haitolewi.

# Misheni zinazofanywa na Tume

Jukumu kuu la Tume ni kukuza na kulinda haki za binadamu katika bara la Afrika na kuhakikisha nchi wanachama zinatekeleza wajibu wake chini ya Mkataba. Tume pia huandaa hadidu za rejea kwa kila misheni ya kukuza haki za binadamu.

Tangu kuanzishwa kwake Tume imefanya misheni za aina mbili. Misheni hizi ni za kukuza na kulinda haki za binadamu. Pia Makatibu maalum hufanya misheni wakilenga ukiukwaji wa haki za

binadamu ulio ndani ya mamlaka yao.

- Misheni ya kukuza (utetezi) wa haki za binadamu.

Ziara au misheni za kukuza haki za binadamu hufanywa na Tume au mfumo wake wake maalum kuraghibisha nchi kuhusu nafasi ya Mkataba wa Afrika, kuhimiza nchi ambazo bado hazijaridhia mikataba muhimu kuhusu haki za binadamu kuiridhia, au kuzishawishi nchi ambazo haziwasilishi ripoti kutimiza majukumu yao ya kuwasilisha ripoti. Kwa madhumuni ya ziara za kukuza haki za binadamu, nchi wanachama 54 zinagawanywa miongoni mwa makamishina. Misheni za kukuza haki za binadamu zimekua zikifanyika kwa nchi nyingi za Afrika.

- Misheni za kulinda haki za binadamu ('misheni za utafutaji taarifa katika eneo la tukio au kufanya uchunguzi')

Misheni za utafutaji taarifa katika eneo la tukio mara nyingi hufanyika katika nchi ambayo mawasiliano kadhaa yamewasilishwa dhidi yake na ikiwa idhini kutoka kwa nchi imepatikana kufanya ziara. Kusudi la kufanya misheni hii mara nyingi huwa ni kutafuta fursa ya kufanya usuluhishi au kuchunguza maelezo maalum kuhusu mawasiliano. Tume pia inaweza kufanya misheni ya utafutaji taarifa pale ambapo kuna madai ya kawaida au kuenea kwa ripoti za ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya nchi mwanachama. Misheni ya kutafuta taarifa haihitaji mawasiliano yoyote ya awali kuwasilishwa kwa Tume kabla misheni haijaanza. 'Kufanya uchunguzi kunaweza kujumuisha utafutaji taarifa na ziara za eneo la tukio.

Tume ilifanya misheni yake ya kwanza ya utafutaji taarifa mwaka 1996 nchini Senegal kufuatia madai ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu huko Kaguitt, Casamance ikihusisha jeshi na waasi huko Casamance. Kisha Tume imefanya misheni kadhaa za kulinda haki za binadamu katika Afrika, hususani katika nchi ambazo madai kuendelea kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu kama vile Sudan na Nigeria. Mwaka 1997, Tume ilifanya misheni nchini Nigeria kutathmini hali ya 'Ogoni 19' (kundi la wanaharakati wa Niger Delta walioshikiliwa kuhusiana na Ken Saro-Wiwa) ambaye alishikiliwa kwa kupinga uharibifu wa mazingira na kutokuwa na maendeleo katika mkoa wao.

Mwaka 2004, Tume ilifanya misheni ya utafutaji taarifa (pamoja na ziara eneo la tukio) katika mkoa wa Darfur, Sudan kuhakikisha madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu na makosa ya jinai ya kimataifa na kupendekeza suluhisho la kutatua hali hiyo.

Baada ya siku za kufanya ziara eneo la tukio na mahojiano, misheni ilibaini kwamba kulikuwa na aina za ukiukwaji wa haki za binadamu uliofanywa na pande zote zilizokuwa kwenye vita ikiwemo serikali na kutoa mapendekezo yake. Misheni kama hizo zilifanyika nchini Mali, Mauritania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Saharawi na Zimbabwe.

### Wajibu wa nchi wakati wa misheni za kulinda haki za binadamu

Nchi mwanachama inalazimika:

- Kutochukua hatua za kulipiza kisasi dhidi ya mtu yeyote au taasisi yoyote iliyotoa taarifa, ushuhuda au ushahidi kwa misheni.
- Kuhakikisha uhuru wa kutembea wa wajumbe wa misheni ikiwemo idhini yoyote muhimu ndani ya nchi.
- Kutoa taarifa yoyote au nyaraka ambayo misheni inaona ni muhimu kwaajili ya kuandaa taarifa yake.
- Kuchukua hatua za kuilinda misheni.

### Jukumu la Asasi za kiraia wakati wa misheni

Asasi za kiraia huwezesha uamuzi wa Tume kufanya misheni kwa kutoa taarifa kuhusu ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Mara nyingi huambatana na Tume wakati wa ziara na wanafahamika kwa kuwa na nafasi ya mshiriki katika majadiliano.

## Maazimio, mwongozo na Maoni ya Jumla

Ibara ya 45 ya Mkataba inaipa mamlaka Tume 'kuandaa na kuweka kanuni na masharti' zinazolenga katika kutatua matatizo ya kisheria yanayohusu haki za binadamu na watu. Kwa mujibu wa ibara hii, Tume inapitisha maazimio yakutatua masuala mbalimbali ya haki za binadamu. Kwa ujumla maazimoi haya yanaweza kugawanywa katika makundi matatu: mada, nchi –maalum na utawala.

### Maazimio ya mada, mwongozo, maoni ya jumla na sheria ya mfano

Azimio la Mada linafafanua kwa maelezo ya kutosha mada za haki maalum au haki ya msingi iliyoelezwa katika Mkataba. Ina

fasili wajibu wa nchi kuhusu haki maalum na inaelezea kiwango kilichowekwa na mkataba. Tume imepitisha maazimio mengi ya mada, wakati mwengine hurejewa kama mwongozo, ikijumuisha mada mbalimbali ikiwemo adhabu ya kifo, haki ya watu wazawa, hali ya wanawake na watoto, haki ya za kijamii na kiuchumi, VVU/UKIMWI, UVIKO 19, mchakato wa uchaguzi, utawala bora, magereza, uhuru wa kushiriki, na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu. Tume imepitisha Maoni ya Jumla sita kwa mfano katika ibara za Itifaki ya Maputo na kuhusu haki ya kuishi. Pia imepitisha miongozo kadhaa ambayo ina ufafanuzi zaidi kuliko maazimio na maoni ya ujumla na sheria ya mfano kuhusu upatikanaji wa habari katika Afrika.

**Azimio Na. 449** kuhusu Haki za Watu na Binadamu kama nguzo ya msingi ya majibu yenye mafanikio kwa UVIKO 19 na ahueni kutokana na athari zake za kijamii na kisiasa. Tume inatoa wito kwa nchi wanachama kuhakikisha khaki ya afya na maisha chini ya ibara ya 16 na 4 za Mkataba wa Afrika kwamba:
Tume ilitoa kipaumbele katika matumizi ya hatua za afya ya jamii ikiwa pamoja na ulazima wa kuvaa barakoa, kuweka vitakasa mikono sehemu za umma, kukusanyika sehemu za wazi, kuzingatia umbali wa kijamii wakati wa kushiriki shughuli za kiuchumi; hatua maalum zinachukuliwa kuwalinda walipo katika mazingira hatarishi katika kuambukizwa UVIKO 19 kama vile wazee na watu wenye magonjwa sugu yasiyoambukiza ikijumuisha kuwaelimisha wanafamilia wao, vituo vya uangalizi na majirani, kuhusu kuyakinga makundi hayo ya watu na kutokaa karibu na watu wanaojihusisha katika maisha ya kijamii na kiuchumi (Tarehe 7 Agosti 2020)

**Azimio la 470** kuhusu ulinzi wa wakimbizi, watafuta hifadhi na wahamiaji katika mapambano dhidi ya mlipuko wa/ kuenea kwa UVIKO 19 katika Afrika: Tume inakumbusha nchi wajibu wake na ahadi walizotoa kwa kukubali viwango na sera za Umoja wa Afrika kuhusu ulinzi wa wanaotafuta hifadhi , wakimbizi na wahamiaji katika bara la Afrika, hususan Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika Unaosimamia Masuala Mahsusi ya Changamoto za Wakimbizi katika Afrika wa mwaka 1969 na Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Ulinzi na Msaada wa Watu Waliolazimika Kuhama Makazi Ndani ya Nchi katika Afrika (Mkataba wa Kampala), hulaani ukiukwaji wote wa haki za binadamu ambazo watafuta hifadhi, wakimbizi na wahamiaji wanastahiki katika muktadha wa usimamizi wa janga la UVIKO -19 katika nchi wanachama wa Mkataba wa Afrika na Itifaki zake.

**Azimio kuhusu hadhi ya wanawake katika Bara la Afrika (lilipitishwa mwaka 2005)**
Tume kupitia Azimio hili imetoa wito kwa nchi wanachama kuridhia na kuweka masharti ya mkataba katika sheria za kitaifa, Itifaki ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za wanawake katika bara la Afrika, kuongeza ushiriki wa wanawake katika operesheni ya kutunza amani, kutekeleza hatua za dhati na kuheshimu ahadi zao chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake na Jukwaa la Utekelezaji la Beijing.

## Maazimio Maalum ya Nchi

Maazimio maalum ya nchi hushughulikia masuala ya haki za binadamu katika nchi wanachama. Aina hii ya Azimio imethibitika ni muhimu sana wakati wowote kukiwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika nchi mwanachama lakini hakuna mtu binafsi aliyewasilisha mawasiliano yoyote kwa tume kuhusu uvunjifu huo. Tume imepitisha maazimio maalum kushughulikia hali ya haki za binadamu katika nchi za Sudan, Uganda, Zimbabwe, Ethiopia, Eritrea, Somalia, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Côte d'Ivoire, Komoro, Libya, Tunisia, Guinea Bissau, Liberia, Burundi, Rwanda na nchi nyingine nyingi.

**Azimio kuhusu hali ya haki za binadamu Gambia (limepitishwa mwaka 2008)**
Azimio hili lilipitishwa kama matokeo ya suala ambalo Tume ililiita 'kuzorota kwa hali ya haki za binadamu nchini Gambia'. Azimio lililaani kukamatwa kwa watu kinyume na sheria, uendeshaji wa mashauri bila na haki, utesaji, unyongaji wa watu wanaodaiwa kupanga njama za kupindua serikali, waandishi wa habari na watetezi wa haki za binadamu bila kufuata utaratibu wa sheria.

Tume iliitaka Serikali ya Gambia kuwaachia mara moja wafungwa wote wa kisiasa na iliiomba Gambia kuchunguza madai yote ya unyongaji wa watu bila kufuata utaratibu wa sheria na utesaji wa watu walio kizuizini. Pia iliiagiza Serikali kutekeleza hukumu ya mahakama ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi ya tarehe 8 Juni 2008 inayohusu ukiukwaji wa haki za Binadamu nchini Gambia.

**Azimio la 469 kuhusu hali ya haki za binadamu katika Shirikisho la Kidemokrasia la Ethiopia (lilipishwa mwaka 2020)**
Pamoja na kulaani matumizi ya nguvu yaliyofanywa na serikali ya Shirikisho ya Jamhuri ya Gambia katika mkoa wa Tigray, Tume iliiagiza Serikali kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu za waethiopia wote hususan katika mkoa wa Tigray kulingana n/kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu iliyoridhiwa na Ethiopia.
Serikali ilihimizwa kufanya uchunguzi wa haraka, bila upendeleo na wenye ufanisi kuhusu vifo vya raia na ukiukwaji mwengne wa haki za binadamu uliofanywa wakati wa vita, kuwawajibisha waliofanya ukiukwaji huo na kulipa fidia inayotosha kwa familia zao.

## Maazimio ya kiutawala

Maazimio ya kiutawala yanahusika na utaratibu wa Tume, mifumo ya ndani na uhusiano kati ya Tume na taasisi zingine za Umoja wa Afrika, vyombo vya kiserikali, Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu, na Mashirika Yasiyo Kiserkali.

Baadhi ya maazimio ya Tume ya kiutawala ni pamoja na uteuzi na mamlaka ya makatibu maalum na vikosi-kazi, maazimio kuhusu vigezo vya kutoa hadhi ya uangalizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na hadhi ya ushirikiano kwa Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu na azimio kuhusu ulinzi wa jina, kifupisho na nembo ya Tume.

# Mafanikio na changamoto za Tume ya Afrika

## Mafanikio ya Tume

- ***Maendeleo ya kutafsiri***

Tume haijatafsiri tu ibara za haki za kiraia na kisiasa lakini pia haki nyinginezo zilizomo katika Mkataba kama vile haki ya kulinda lugha, haki ya amani na usalama wa kitaifa na kimataifa, ulinzi wa maisha ya familia, haki ya maendeleo, haki ya kuishi, haki ya makazi na kujiamulia. Tume kupitia nadharia ya 'haki zisizotamkwa' wametafsiri haki ya maisha na afya kujumuisha haki ya chakula. Aidha, Tume kupitia nadharia hii imetafsiri haki ya makazi kutoka haki ya mali na ulinzi wa familia.

> 'Ingawa haki ya makazi au makao haijatajwa bayana katika Mkataba wa Afrika, matokeo ya muunganiko wa ibara inayolinda haki ya kumiliki mali na ulinzi unaopewa familia inakataza uharibifu mbaya wa makazi kwasababu makazi yakiharibiwa mali, afya na maisha ya familia yataathiriwa vibaya…Muunganiko wa athari za ibara ya 14,16 na 18 inasomeka katika Mkataba haki ya malazi au makazi.' (*SERAC v Nigeria*, aya ya 60)

- ***Kuendeleza Haki za Wanawake***

Tume imechukua hatua za kuendeleza hali za wanawake katika Afrika. Mbali na mafanikio yake katika suala hili, imepitisha Itifaki ya Wanawake, imepitisha maazimio kuhusu masuala maalum yafuatayo ya wanawake: hadhi ya wanawake katika Afrika (2005); wanawake na wasichana waathiriwa wa ukatili wa kingono (2007); Vifo vya mama na watoto katika Afrika (2008).

Uteuzi wa Katibu Maalum kuhusu Haki za Wanawake katika Afrika mwaka 1998, umechangia sana maendeleo haya na mwenye-mamlaka mtambuka anaendelea kukuza utekelezaji wa Itifaki ya Wanawake na kuhudumu kama Afisa kiungo wa Tume kwa ajili ya kukuza na kulinda haki za wanawake katika Afrika.

- ***Uhusiano imara na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu***

Tume ina uhusiano mzuri na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hutoa taarifa wakati wa kikao cha wazi cha Tume na wanawakilishwa na

Vikosi -Kazi vilivyoanzishwa na Tume.

- ***Kukuza haki za wazawa***

Tume imekua mstari wa mbele katika kukuza haki za wazawa katika Afrika. Tume imetoa matamko muhimu kuhusu haki za wazawa maarufu miongoni mwa hayo ni shauri la Endrois. Aidha, Tume ilianzisha Kikosi-Kazi kuhusu idadi na jamii za wazawa katika Afrika. Ripoti ya Kikosi-Kazi imepitishwa na Tume.

> 'Tume ya Afrika …inatambua kwamba kutokana na michakato ya zamani na ya sasa wazawa, wamekua wakitengwa katika nchi zao wenyewe na wanahitaji utambuzi na ulinzi wa haki zao za binadamu na uhuru wa msingi. (Shauri la *Endrois*, aya ya 148)

- ***Kanuni ya haki ya kufika na kusikilizwa mbele ya Tume***

Mtu binafsi yeyote au Shirika Lisilo la Kiserikali lolote linaweza kuwasilisha mawasiliano mbele ya Tume. Mwandishi wa mawasiliano hatakiwi kuwa muathiriwa wa ukiukwaji unaodaiwa.

> 'Ibara ya 56 (1) ya Mkataba inataka kwamba mtu yeyote anayewasilisha Tume mawasiliano kuhusu haki za binadamu lazima atoe utambulisho wake. Hawahitajiki kuwa waathiriwa wa ukiukwaji huo au wanafamilia' (*Malawi African Association dhidi ya Mauritania*, aya ya 78).

Tume imetafsiri 'masharti zuizi' katika mkataba kwa upana

> 'Kwa mujibu wa ibara ya 9(2) ya Mkataba, usambazaji maoni unaweza kuzuiwa na sheria. Hii haimainishi kwamba sheria ya nchi inaweza kuweka kando haki ya mtu kutoa na kusambaza maoni yake; hii ingefanya ulinzi wa haki ya mtu kutoa maoni isiwe na ufanisi. Kuruhusu sheria ya nchi kuwa juu ya sheria ya kimataifa ya Mkataba kutazuia madhumuni ya haki na uhuru uliowekwa katika Mkataba. Viwango vya kimataifa vya haki za binadamu lazima zitawale wakati wote juu ya sheria ya kitaifa yenye ukinzani. Kizuizi chochote cha haki katika Mkataba kitapaswa kuzingatia masharti ya Mkataba.' (*Media Rights Agenda* na Wenzake dhidi ya Nigeria, aya 66)

## Changamoto zinazoikabili Tume

- ***Changamoto za Tume na Sekretarieti***

Muda kati ya kuwasilisha malalamiko na maamuzi ya mwisho ya Tume ni mrefu. Hii inaathiri matokeo ya maamuzi ya Tume. Licha ya Tume kuwa na mrundikano wa mawasiliano, Tume haijaonesha shauku kubwa ya kupeleka rufaa kwa Mahakama. Tume pia inachelewesha ripoti kupitishwa na Makatibu Maalum. Tume haina mfumo wa kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yake.

Changamoto kubwa inayoikabili Tume ni kupata namna ya kuweka uwiano unaofaa katika kutekeleza mamlaka zake za kukuza na kulinda haki.

Kuingiliwa kisiasa na ukosefu wa uhuru wa Tume. Mnamo tarehe 8 Agosti 2018, Tume iliondoa hadhi ya uangalizi kwa Muungano wa Wasagaji wa Kiafrika kufuatia uamuzi wa Baraza la Utendaji la Umoja wa Afrika ambalo liliitaka Tume kuzingatia 'maadili ya Afrika' inapokuwa inapitia maombi ya hadhi ya uangalizi.

- ***Changamoto za nchi***

Nchi nyingi ziko nyuma katika kutekeleza wajibu wao wa kuwasilisha ripoti za nchi chini ya Mkataba, hivyo kuinyima Tume fursa ya kawaida ya kupitia rekodi ya haki za binadamu ya nchi. Nchi hazina utashi wa kisiasa ya kufuata mapendekezo ya Tume.

- ***Changamoto zinazohusu Umoja wa Afrika***

Taasisi za kisiasa za Umoja wa Afrika hazitoi msaada kwa Tume na wakati mwingine huzuia kazi za Tume mfano kwa kuzuia kuchapishwa kwa Ripoti ya Shughuli zake.

Pia kuna ukosefu mkubwa wa uratibu kati taasisi au vyombo vyenye mamlaka yanayohusu haki za binadamu, ingawa Umoja wa Afrika unajitahidi kutatua changamoto hii kwa kupitia Usanifu wa Utawala wa Afrika.

# C. Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

## Uanzishwaji

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama ya Afrika) imeanzishwa kupitia Itifaki ya Mkataba wa Afrika. Itifaki kuhusu Uanzishaji wa Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu Afrika (Itifaki ya Mahakama) ilipitishwa Ouagadougou, Burkina Faso, tarehe 9 Juni 1998 na ilianza kutumika tarehe 25 Januari 2004. Mahakama ilianzishwa ili kukamilisha mamlaka ya ulinzi wa haki za binadamu ya Tume. Maamuzi yake ni ya mwisho na yana nguvu za kisheria kwa nchi wanachama ambazo zimeridhia Itifaki.

## Kanuni za Utaratibu

Shughuli za mahakama na taratibu zinaratibiwa na Kanuni za Utaratibu. Kanuni za awali na za muda zilitengenezwa mwaka 2008 baada ya ulinganifu na kanuni za Tume. Baadaye kanuni zilibadilishwa mwaka 2010. Katika kikao cha kawaida cha 58 cha Mahakama mwaka 2020, Kanuni za Utaratibu mpya zilipitishwa kuchukua nafasi ya zilizopita kwa lengo la kuongeza ufanisi na umadhubuti wa Mahakama.

## Muundo

Mahakama inaundwa na Majaji 11 waliochaguliwa Mkutano wa Umoja wa Afrika kutoka kwenye orodha iliyopendekezwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika. Majaji huchaguliwa kwa uwezo wao binafsi lakini hakuna majaji wawili wanaohudumu watakaotoka nchi moja. Uwakilishi wa kijinsia na kijiografia pia huzingatiwa. Majaji huchaguliwa kwa muhula wa miaka sita na wanastahili kuchaguliwa tena kwa muhula mmoja tu. Rais wa Mahakama atahudumu katika nafasi yake kwa muda wote. Majaji wengine 10 hufanya kazi kwa muda. Kanuni za mwaka 2020 zimeanzisha kada ya Mkuu wa Majaji, ambayo inafasiliwa kama 'Jaji aliyehudumu kwa muda mrefu zaidi ambaye si mwanachama wa ofisi'. Majaji wa kwanza wa Mahakama waliapishwa kushika ofisi mnamo tarehe 1

Julai mwaka 2006. Mahakama huketi Arusha, Tanzania.

## Ofisi

Ofisi inaundwa na Rais na Makamu wa Rais kila mmoja ana mamlaka ya muhula wa miaka miwili ambao unaweza kuongezwa mara moja. Ibara ya 10(2) ya Kanuni mpya za Mahakama zilizorekebishwa za mwaka 2020 zimeanzisha uzingatiaji wa usawa wa jinsia katika muundo wa ofisi. Mnamo Juni 2021, Jaji Aboud alichaguliwa kama Jaji wa pili mwanamke kuwa Rais wa Mahakama.

## Masijala

Masijala inaundwa na Msajili na Naibu Msajili na wafanyakazi ambao Mahakama inaweza kuwahitaji kwa ajili ya utekelezaji majukumu wenye ufanisi. Katika kuweka sawa uwiano wa historia ya kikanda, mila za kisheria na lugha, Kanuni ya 16 (2) ya Kanuni za Mahakama zilizorekebishwa mwaka 2020 vilevile ilianzisha uzingatiaji wa lugha, ukanda na usawa wa kijinsia katika uchaguzi wa wajumbe wa Masijala.

## Wajumbe

### *Majaji wa sasa (Juni 2021)*

**Ofisi ya Mahakama Rais wa Mahakama**
Imani Daud Aboud (2018 - ) Tanzania

**Makamu wa Rais**
Blaise Tchikaya (2018 - ) Jamhuri ya Kongo

**Majaji Wengine**
Ben Kioko (2012 - ) Kenya
Mh. Rafaâ Ben Achour (2014 - ) Tunisia
Mh. Ntyam Ondo Mengue (2016 - ) Kameruni
Mh. Marie Thérèse Mukamulisa (2016 - ) Rwanda
Mh. Tujilane Rose Chizumila (2017 - ) Malawi
Mh. Bensaoula Chafika (2017 - ) Algeria
Mh. Stella Isibhakhomen Anukam (2018 - ) Nigeria
Mh. Dumisa Buhle Ntsebeza (Juni 2021 - ) Afrika Kusini
Mh. Sacko Modibo (Juni 2021 - ) Mali

**Majaji Waliopita**
Mh. Gérard Niyungeko (2006 - 2012) Burundi
Mh. El Hadji Guissé (2006 - 2012) Senegal
Mh. Solomy Balungi Bossa (2014 - 2020) Uganda
Mh. Augustino S. L. Ramadhani (2010 - 2017) Tanzania
Mh. Elsie Nwanwuri Thompson (2010 - 2016) Nigeria

Mh. Fatsah Ouguergouz (2006 - 2016) Algeria
Mh. Duncan Tambala (2010 - 2016) Malawi
Mh. Sophia A. B. Akuffo (2006 - 2014) Ghana
Mh. Jean Mutsinzi (2006 - 2012) Rwanda

Mh. Bernard Makgabo Ngoepe (2006 - 2013) Afrika Kusini
George W Kanyeihamba (2006 - 2008) Uganda
Jean Emile Somda (2006 - 2008) Burkina Faso
Kelello Justina Mafoso-Guni (2006 - 2010) Lesotho
Hamdi Faraj Fanoush (2006 - 2010) Libya
Githu Muigai (2008 - 2009) Kenya
Joseph N Mulenga (2008 - 2012) Uganda
Kimelabalou Aba (2013 - 2014) Togo
Sylvain Ore (2016 - Juni 2021) Côte d'Ivoire
Jaji Ângelo Vasco Matusse (2014 - Juni 2021) Msumbiji

Katika mkutano wa kawaida wa 34 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mwezi Februari 2021, majaji wawili wapya walichaguliwa (Jaji Dumisa Buhle wa Afrika Kusini na Jaji Sacko Modibu wa Mali). Walichukua nafasi ya Jaji Sylvain Oré na Jaji Ângelo Vasco Matusse kuanzia Juni 2021 walipoanza kazi katika kikao cha 61 cha kawaida cha Mahakama.

**Kwa mawasiliano zaidi kuhusu shughuli za Mahakama, wasiliana na:**
Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu
Mwalimu Julius Nyerere Conservation Centre, Barabara ya Dodoma
S.L.P 6274 Arusha, Tanzania
Simu: (255) 27 2970430
Faksi: (220) 441 05 04
Baruapepe: registrar@african-court.org
tovuti: www.african-court.org

# Vikao vya Mahakama

Mahakama inafanya vikao vyote vya kawaida na maalum. Kufikia Februari 2021, Mahakama ilikua imefanya vikao vya kawaida 60 na vikao maalum 10. Vikao vyote vya Mahakama hufanyika katika Mahakama au katika nchi moja wapo mwanachama wa Umoja wa Afrika, kama Mahakama itaamua au vifanyike kwa njia ya mtandao kutokana na mazingira.

## Vikao vya Kawaida vya Mahakama

Vikao vya Mahakama vya Kawaida hufanyika mara nne kila mwaka kwa muda wa angalau wiki nne tarehe ya kikao cha Mahakama hupangwa na Mahakama wakati ikikaa au Rais akishauriana na Majaji wengine.

## Vikao maalum vya Mahakama

Mahakama inaweza kuitisha vikao maalum vya mahakama. Vikao maalum vya Mahakama huitishwa na Rais wa Mahakama kwa uamuzi wake mwenyewe au baada ya kuombwa na Majaji wa Mahakama walio wengi.

## Vikao kwa njia ya mtandao

Pamoja na changamoto ya kuenea kwa UVIKO 19 katika ulimwengu, uwezekano wa kufanya vikao kwa njia ya mtandao uliimarishwa na Kanuni ya 89 na 90 za Kanuni za Mahakama za mwaka 2020.

Mnamo Mei mwaka 2020 wakati wa kipindi cha UVIKO 19 Majaji wa Mahakama walifanya kikao kwa njia ya mtandao kuamua hatua za kuchukua wakati wa janga hilo la UVIKO 19, kwa ajili ya uendeshaji mzuri wa Mahakama na usalama wa wafanyakazi. Kufuatia uamuzi wa kikao hicho, mkutano Mahakama wa kawaida wa 57 ulifanyika kwa njia ya mtandao.

# Mamlaka

## Mamlaka katika masuala yanayobishaniwa

- Mamlaka binafsi

Mamlaka ya Mahakama inatumika tu kwa nchi ambazo zimeridhia Itifaki ya Mahakama. Mahakama inaweza kusikiliza mashauri na migogoro kuhusu tafsiri na matumizi ya Mkataba wa Afrika, Itifaki ya Mahakama na mkataba wowote wa haki za binadamu ambao nchi husika imeridhia.

Watu binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wanaweza kuwasilisha mashauri katika Mahakama moja kwa moja dhidi ya mwanachama tu ambaye ametoa tamko chini ya ibara ya 34(6). Mahakama ina mamlaka binafsi ya kisheria juu ya waombaji hawa.

- Mamlaka ya kimkataba

Mahakama ina mamlaka juu ya mikataba ya haki za binadamu ya Umoja wa Afrika na mikataba mingine ya haki za binadamu iliyoridhiwa na nchi husika. Katika kutumia mamlaka haya ya kisheria katika mikataba, mtizamo wa Mahakama haujawahi kuwa sawa. Kwa upande mmoja, katika shauri la Mtikila, Mahakama baada

ya kuzingatia madai ya ukiukwaji wa haki chini ya ibara husika za Mkataba wa Afrika haikuchukulia kama ni lazima kuzingatia matumizi ya mikataba mingine (Mtikila dhidi ya Tanzania, aya ya 123). Kwa upande mwengine, kama ilivyoonekana katika shauri la Zongo), Mahakama ilibaini ukiukwaji wa haki ya uhuru wa kujieleza chini ya Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa. Katika shauri la Mango dhidi ya Tanzania, Mahakama ilibaini ukiukwaji wa haki za binadamu chini ya Mkataba wa Afrika na Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (Tamko la kimataifa) kwa msingi kwamba Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu ni sehemu ya sheria ya kimila za kimataifa, isipokuwa iliamua kwamba haina mamlaka kuhusu hoja ya kisheria za ndani ya nchi au mikataba ya kimataifa ambayo haina nguvu za kisheria kwa nchi mwanachama inayojibu mawasiliano.

- Mamlaka ya muda

Mamlaka ya muda ya Mahakama inaanza muda ambao Itifaki ya Mahakama ilianza kutumika kwa nchi fulani, isipokuwa katika mazingira ambayo ukiukwaji unaendelea. Katika shauri la Mtikila dhidi ya Tanzania, Mahakama ilibaini kwamba mjibu mawasiliano anawajibika kwasababu wakati wa madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu, Tanzania ilikua imesharidhia Mkataba wa Afrika na ilikua inawajibika na masharti ya Mkataba huo. Pia Mahakama iliamua kuwa, kizuizi cha mgombea huru, ambacho kilikua kinalalamikiwa kilikua ni kitendo endelevu kilidumu hadi itifaki ya Mahakama ilipoanza kutumika. Katika shauri la Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu dhidi ya Kenya, Mahakama iliamua kwamba ina mamlaka hata kama Mkataba wa Afrika ulikua haujaanza kutumika wakati wa ukiukwaji wa haki za binadamu. Iliamuliwa kwamba shauri hili lilikua linahusu 'ukiukwaji wa haki za binadamu endelevu za wazawa wa jamii ya Ogiek msitu wa Mau nchini Kenya.

## Mamlaka ya kutoa ushauri

Mahakama inaweza pia kutoa ushauri kuhusu suala lolote ambalo lipo katika mamlaka yake. Ushauri wa Mahakama unaweza kuombwa na Umoja wa Afrika, nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, mashirika ya Umoja wa Afrika na taasisi yoyote inayotambuliwa na Umoja wa Afrika (Ibara ya 4(1) ya Itifaki ya Mahakama).

Katika Ombi la Ushauri lililoletwa na Umoja wa Wanasheria wa Afrika (PALU), kuhusu kushabihiana kwa sheria za uzururaji (2020), Mahakama katika kuzingatia kwamba kama sheria zinashabihiana

na Mkataba wa Afrika ilibaini kwamba sheria hizi zinawaadhibu walionyimwa haki za msingi za kijamii kwa kutumia nafasi za wazi kupata kipato hivyo kusababisha hali za kiuchumi na kijamii za watu hao kwa kukiuka haki zao chini ya sheria hizi. Aidha, Mahakama ilizingatia kushabihiana kwa Sheria za Uzururaji na Mkataba wa Haki za Watoto na ilibaini kwamba uhamishwaji wa lazima kutoka maeneo yao ya makazi na kuwakamata na kuwaweka kizuizini watoto ili kutekeleza sheria za uzururaji kunasababisha ukiukaji wa haki za watoto.

Vilevile, Mahakama ilizingatia kushabihiana kwa sheria za uzururaji na Itifaki ya Maputo na kutoa tamko kwamba sababu sheria hizi zinaruhusu idhini ya kumkamata mwanamke bila hati, inawaathiri wanawake zaidi kwasababu mara nyingi hawawezi kulipia ada za dhamana hivyo wanakua katika hatari ya kukaa kizuizini kwa kipindi kirefu suala ambalo linakiuka ibara ya 24 ya Itifaki ya Maputo.

Katika Ombi la ushauri la Kamati ya Afrika ya Wataalam wa Haki na Ustawi wa Mtoto (2014), Mahakama iliamua kwamba Kamati ina mamlaka ya kutoa ushauri inapoombwa lakini sio kupeleka suala lenye ubishani wa kisheria mbele yake.

Katika Ombi la Ushauri la Kituo cha Haki za Binadamu, Chuo Kikuu cha Pretoria na Shirikisho la Wasagaji Afrika (Ombi la Ushauri) (2017), Mahakama iliamua kwamba haina mamlaka ya kutoa ushauri kwa shirika Lisio la Kiserikali ambalo halitambuliwi na Umoja wa Afrika. Hata hivyo Kituo cha Haki za Binadamu kina hadhi ya uangalizi katika Tume ya Afrika na Shirikisho la Wasagaji Afrika lilisajiliwa kama taasisi nchini Afrika Kusini. Mahakama iliamua kwamba hawakuwa katika tafsiri ya ibara ya 4 (1) ya Itifaki inayoanzisha Mahakama kuhusu watu wanaoweza kuwasilisha ombi la ushauri kwa Mahakama.

## Ufikiwaji wa Mahakama

Watu binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaweza kuifikia mahakama kwa njia isiyo ya moja kwa moja, kwanza kwa kuwasilisha mawasiliano kwa Tume ya Afrika. Hii inatumika kwa nchi zote ambazo zimeridhia Itifaki ya Mahakama. Tume ina haki ya kuwasilisha shauri katika Mahakama. Kama Tume ikihitimisha shauri baada ya kulisikiliza, ikabaini kuna ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya nchi mwanachama wa Itifaki, inaweza kupeleka

shauri katika Mahakama kama nchi itashindwa kuzingatia uamuzi wa Tume.

## Ufikiwaji wa Mahakama kwa njia nyingine




Taasisi zifuatazo zina uhalali wa kisheria wa kuwasilisha mashauri katika Mahakama: Tume ya Afrika, nchi wanachama wa Itifaki ya Mahakama na vyombo vya kiserikali vya Afrika.

## Kuifikia Mahakama moja kwa moja

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yenye hadhi ya uangalizi mbele ya Tume na watu binafsi wanaweza kuwasilisha mashauri moja kwa moja kwa Mahakama, iwapo nchi imetoa tamko chini ya ibara ya 34(6) ya Itifaki inayoanzisha Mahakama.

Nchi wanachama ambazo zimetoa tamko la kukubali watu binafsi kuifikia Mahakama moja kwa moja chini ya ibara ya 34(6) ni: Burkina Faso, Malawi, Mali, Ghana, Tunisia na Gambia.

Nchi wanachama zifuatazo zilitengua matamko yake:

- Tanzania: 14 Novemba 2019
- Rwanda: 24 Februari 2016
- Benin: 24 Machi 2020
- Côte d’Ivoire: 28 Aprili 2020




### Maombi ya nchi wanachama zilizokubali kuifikia Mahakama moja kwa moja (Juni 2021)

| **Nchi inayojibu mawasiliano** | **Rekodi** |
|---|---|
| Jamhuri ya Benin | 35 |
| Jamhuri ya Burkina Faso | 8 |
| Jamhuri ya Gambia | 5 |
| Jamhuri ya Ghana | 4 |
| Jamhuri ya Rwanda | 16 |
| Jamhuri ya Tunisia | 6 |
| Jamhuri ya Mali | 28 |
| Jamhuri ya Malawi | 4 |
| Jamhuri ya Ivory Coast | 36 |
| Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 156 |
| **Jumla** | **316** |

## Uhusiano kati ya Mahakama na Tume

Uhusiano kati ya Mahakama na Tume unasimamiwa na Itifaki inayoanzisha Mahakama. Itifaki hii inaonyesha uhusiano wa Mahakama na Tume kama ifuatavyo:

- Mahakama inakamilisha mamlaka ya ulinzi wa haki za binadamu ya Tume
- Mahakama inaweza kuhamisha shauri lililo mbele yake kwenda

Tume. Katika mashauri ambayo yalifikishwa Mahakamani, Kanuni ya 36 (4) ya Mwaka 2020 inaainisha kwamba Mahakama inaweza kuiomba Tume kufanya uchunguzi kutafuta taarifa au kufanya uchunguzi katika eneo la tukio endapo Tume siyo mhusika katika shauri. Hii inasaidia kupunguza mrundikano wa kazi katika Mahakama na kuhakikisha kiwango cha uhuru wa Mahakama katika kufanya uchunguzi.

- Tume kwa uamuzi wake yenyewe inaweza kuwasilisha mawasiliano kuhusu ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, Kwa mfano angalia shauri la Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu dhidi ya Libya (2011) 1 AfCLR 17, kuhusu ombi la kuchukuliwa kwa hatua za awali kuhusu ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu nchini Libya, Aidha, shauri la Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu dhidi ya Kenya ("013) 1 AfCLR 193.
- Tume inaweza, katika hatua yoyote kushughulikia mawasiliano, kuisimamisha Mahakama kufanya uchunguzi wa mawasiliano.
- Tume inaweza kuwasilisha mawasiliano Mahakamani kwasababu ya nchi kushindwa au kutokuwa tayari kuzingatia uamuzi wake au kuchukua hatua za muda.
- Mahakama inaweza kuomba maoni ya Tume pale ambapo inaamua kuhusu hoja za kupokea shauri.
- Mahakama inaweza kutoa ushauri baada ya kuombwa na Tume
- Katika kuandaa kanuni zake, Mahakama inatakiwa kushauriana na Tume kadri inavyofaa.

## Libya Hatua za awali zilizoamriwa dhidi ya Libya

Kutokana na uwepo wa madai kadhaa ya ukiukwaji wa haki za binadamu katika nchi ya Libya, mapema mwaka 2011, Tume ya Afrika kwa mara ya kwanza ilipeleka shauri Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu. Tume iliamuru hatua za awali kuchukuliwa, ambazo Libya ilitakiwa kujibu ndani ya siku 15.

> 'Endapo, kwa maoni ya Mahakama, kuna ukiukwaji wa haki uliokithiri kwa kiwango cha juu na uharaka, vilevile kuna madhara yasiyorekebishika kwa watu ambao wameleta maombi, hususan, kuhusu haki ya kuishi na utu wa mtu kama zilivyohakikishwa katika Mkataba… Kwa sababu hizi, Mahakama kwa kauli moja iliamuru kwamba lazima Libya iache kitendo chochote ambacho kitapelekea kupoteza uhai/maisha au kukiuka utu wa mtu , ambayo inaweza kuwa ukiukwaji wa masharti ya Mkataba au Mkataba mwengine wa kimataifa wa haki za binadamu ambao Libya ni seheumu ya Mkataba huo.. (Tume ya Afrika dhidi ya Libya, aya ya 22 na 25)

## Vigezo vya kupokea mashauri yanayowasilishwa na mtu binafsi au Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Kuhusiana na mashauri yanayowasilishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na watu binafsi, ibara ya 34(6) ya Itifaki ya Mahakama inaeleza kwamba nchi mwanachama inayohusika ambayo ilitoa tamko la kukubali uwezo wa mahakama wa kisheria wa kupokea mashauri kutoka kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na watu binafsi. Hili ni sharti kwa ajili ya kuanzisha mamlaka binafsi ya Mahakama kuhusu masuala husika. Ibara yake ya 6 ya itifaki ya Mahakama inaitaka Mahakama kuweka masharti kwa ajili ya kupokea mawasiliano kama ilivyoanishwa katika ibara ya 56 ya Mkataba wa Umoja wa Afrika, ambayo inajumuisha kutumia nafuu za ndani ya nchi, muda stahiki na ushahidi unaotokana na madai.

### Kutokutumia kikamilifu nafuu za ndani ya nchi

Katika shauri la Diakité Couple dhidi ya Mali, Mahakama iliamua kwamba haina mamlaka ya kusikiliza shauri kwasababu nafuu za ndani ya nchi hazikuombwa, ikizingatiwa kwamba polisi hawakufanya uchunguzi wa kutosha wa shauri. Kwa misingi hiyo hiyo Mahakama pia ilifuta shauri la Mulindahabi dhidi ya Rwanda.

### Marekebisho mengine muhimu katika Kanuni za Mahakama za mwaka 2020

Kanuni za Mahakama mpya za mwaka 2020 zimefanya mabadiliko mazuri ambayo yanastahiki kuelezwa. Chini ya Kanuni ya 40(5), muombaji ambaye hana uwezo wa kuwasilisha nakala halisi ya maombi yake kwa Msajili anaweza kuwasilisha nakala iliyothibitishwa, iliyochanganuliwa au za kieletroniki. Hata hivyo ni lazima wahakikishe wamewasilisha nakala halisi kabla ya siku iliyopangwa na Mahakama kwa ajili ya usikilizaji. Kwa Kanuni ya 40 (7), Masijala inaruhusiwa kumjulisha mhusika katika shauri kuhusu maudhui yoyote inayokosekana katika faili na hivyo kuomba ufafanuzi husika.

Endapo shauri limeletwa dhidi ya nchi, nchi inayojibu shauri ilikuwa na siku 60 za kujibu, wakati hakukua na muda maalum uliotolewa kwa ajili ya muombaji kuwasilisha majibu kinzani. Kwa

sasa chini ya Kanuni Mahakama mpya, Kanuni ya 44 inaongeza muda hadi siku 90 kwa mleta maombi kujibu. Mahakama inaweza kutoa ongezeko la siku kwa kuzingatia tu mazingira maalum ya shauri hilo. Kanuni za 46 na 47 zinaainisha zaidi kwamba hati za shauri zitachukuliwa kuwa zimefungwa ikiwa baada ya kipindi cha siku 45, mleta maombi anashindwa kuwasilisha majibu kinzani yoyote. Hii husaidia kuweka uhakika zaidi na kuisaidia Mahakama katika kutimiza majukumu yake, ukizingatia kwamba Kanuni za zamani hazikueleza kuhusu suala hili kiasi ambacho Mahakama ilikua ikiwakumbusha wahusika katika shauri mara nyingi kabla ya kufunga Hati za Shauri. Endapo hati za shauri zitafungwa, marekebisho yoyote na pande husika za shauri yanaweza kufanywa tu baada ya Mahakama kuidhinisha na kukiwa na sababu ya msingi.

Kwa ajili ya kusimamia haki inavyostahilli, kwa sasa Kanuni ya 63 inaruhusu pande husika katika shauri ambao wamepokea hukumu ya difoti kuomba hukumu hiyo kutenguliwa ikiwa watawasilisha ombi ndani ya muda wa mwaka moja tangu hukumu itolewe na pia watatoa sababu nzuri.

Miongoni mwa marekebisho yanayostahili kusifiwa katika Kanuni ni kuanzishwa kwa utaratibu wa hukumu ya mfano, chini ya Kanuni ya 66. Imetafsiriwa katika Kanuni kama 'hukumu ya Mahakama ambayo inashughulikia kundi la mashauri yanayofanana ambayo yanatokana na sababu za madai au matatizo yenye asili ya kimfumo au kimuundo yanayofanana'. Inajumuisha mashauri ambayo idadi ya malalamiko inaonyesha ukiukwaji wa kimfumo au kimuundo ambao umewasilishwa dhidi ya Mlalamikiwa yuleyule (walalamikiwa walewale). Msajili anatakiwa kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya Mahakama na Mahakama itaamua kuhusu utaratibu wa hukumu ya mfano baada ya kuomba ridhaa kwa wahusika. Kisha shauri litapewa kipaumbele na hivyo Mahakama inaweza isiendelee na hitajio la kusikiliza kila shauri la mtu binafsi dhidi ya mjibu (wajibu) mawasiliano husika tofauti. Katika kuamua hukumu ya mfano, Mahakama inaruhusiwa kukubali usuluhishi baina ya wahusika. Endapo hii itashindikana au ikiwa Nchi inayojibu mawasiliano inashindwa kuheshimu masharti yaliyopo ya hukumu ya mfano basi Mahakama itaendelea kuamua kufanya uamuzi unaojitegema wa kila shauri ambalo liliahirishwa, kama vile hakuna hukumu iliyopitishwa.

## Baadhi ya maamuzi yaliyofanywa kwa kusikiliza msingi wa shauri

Tangu ianze kufanya kazi mwaka 2006, Mahakama imeamua baadhi ya mashauri kwa kusikiliza msingi wake. Maamuzi hayo zimeonyeshwa hapa chini:

- ***Mtikila dhidi ya Tanzania* (14 Juni 2013)**

Waleta maombi katika shauri hili wanadai kwamba baadhi ya ibara katika Katiba ya Tanzania vinavyozuia mgombea huru kugombea nafasi za uchaguzi vinakiuka uhuru wa wananchi wa kushirikiana na wengine, haki dhidi ya kutokubaguliwa, na haki ya kushiriki katika shughuli za umma na za serikali za nchi. Mahakama ilibaini kwamba kulikua na ukiukwaji wa haki zilizohakikishwa chini ya ibara ya 2, 3, 10 na 13(1) Mkataba wa Afrika.

- ***Zongo na Wenzake dhidi ya Burkina Faso* (28 Machi 2014)**

Katika shauri la Zongo waleta maombi walidai kwamba Burkina Faso imeshindwa kuchunguza na kuwafungulia mashtaka waliohusika na kifo cha Norbet Zongo na wenzie watatu, kwa ajili ya uchunguzi wao wa uandishi wa habari, na kwamba hii iliwaweka katika hatari ya kufanya kazi katika hofu na vitisho. Mahakama ya Afrika ilibaini kuwa kushindwa kwa serikali kuchunguza na kuwashitaki wahalifu ilikua ni ukiukwaji wa haki ya kujieleza na haki ya mtu kusikilizwa na mahakama za kitaifa chini ya ibara ya 7 na 9 ya Mkataba (ikisomwa pamoja na ibara ya 66(2)(c) cha Mkataba wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi uliofanyiwa marejeo.

- ***Konaté dhidi ya Burkina Faso* (5 Disemba 2014)**

Katika shauri la Konaté, mleta maombi alishtakiwa kwa kosa la kukashifu chini ya sheria ya Burkinabe, alipewa adhabu ya kifungo na kuamriwa kulipa faini, kulipa faini kubwa, uharibifu na gharama, kufuatia makala mbili alizochapisha katika gazeti zikimhusisha mwendesha mashtaka wa serikali. Katika hukumu yake, Mahakama ilibaini kwamba adhabu ya kifungo kuhusu kosa la kukashifu chini ya sheria za mujibu mawasiliano zilikuwa zinaingilia haki ya kujieleza ya mleta maombi hivyo ukiukwaji wa Mkataba wa Afrika, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa na Mkataba wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi uliofanyiwa marejeo.

- ***Thomas v Tanzania* (20 November 2015)**

Katika shauri hili, mleta maombi alishtakiwa na hukumiwa bila

kuwepo Mahakama Kuu ya Tanzania, akiwa amelazwa hospitali kwa ugonjwa sugu. Mahakama ya Rufani ilithibitisha hatia yake na jaribio lake la kuomba mapitio ya kimahakama lilishindikana. Mahakama ya Afrika ilibaini kwamba haki ya kusikilizwa ya mleta maombi ambayo inajumuisha haki ya kujitetea ilikiukwa.

- ***Onyango dhidi ya Tanzania* (18 Machi 2016)**

Katika shauri la Onyango, waleta maombi walidai kwamba kukaa kwao kizuizini kwa muda mrefu na kucheleshwa kwa shauri lao ilikua ni ukiukwaji wa haki yao ya kusikilizwa kikamilifu ndani ya muda stahiki. Mahakama iliamua kwamba nchi mjibu maombi ulikua unakiuka ibara ya 7(1) (d) ya Mkataba wa Afrika ambayo inahakikisha haki ya kushitakiwa ndani ya muda stahiki.

- ***Abubakari dhidi ya Tanzania* (3 Juni 2016)**

Mleta maombi alihukumiwa kwa kosa la wizi wa kutumia silaha na alikua anatumikia kifungo cha miaka 30. Alidai kuwa wakati anakamatwa na kushitakiwa hakupewa fursa wala kuwezeshwa kujitetea. Mahakama ilibaini kwamba nchi ilikiuka ibara ya 7 ya Mkataba wa Afrika. Pia Mahakama ilibaini kwamba Mahakama iliyosikiliza shauri haikuzingatia ipasavyo utetezi wa mleta maombi na mwendesha mashtaka alikua na mgongano wa kimaslahi na muathirika wa shitaka linalodaiwa, utetezi wake wa kutokuwepo eneo la tukio wakati wa tukio, na vile vile kukutwa kwake na hatia kulitokana na ushahidi unaokinzana wa shahidi mmoja bila gwaride la utambuzi ilikuwa ukiukwaji wa ibara ya 7 ya Mkataba.

## Mada katika mashauri mengine

- ***Mamlaka (kujitoa)***

*Ingabire Victoire Umuhoza dhidi ya Rwanda* (3 Juni 2016)

Katika shauri hili, mjibu mawasiliano (Rwanda) alitoa hoja kwamba Mahakama haina mamlaka ya kuamua shauri kuhusu tamko lake la kujitoa (chini ya ibara ya 34(6) ya Itifaki ya Mahakama, ikiruhusu watu binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuweza kuwasilisha malalamiko moja kwa moja) mara tu ilipowasilishwa Tume. Inadaiwa kwamba kutokana na hilo, Mahakama haikuweza kuendelea kusikiliza msingi wa shauri lenyewe. Katika kuamua endapo mjibu maombi ana haki ya kujitoa na athari ambazo pande husika katika shauri zitapata, Mahakama iliamua kwamba ilikua na mamlaka katika masuala yote yanayohusu Itifaki ya Mahakama kwa mujibu wa ibara ya 3 (1) na (2) ya Itifaki ikijumuisha suala la kujitoa. Pia iliamua kwamba ili kuhakikisha 'usalama wa mahakama kwa

kuzuia kusimamishwa ghafla kwa haki ambazo zinaathiri (wahusika wa tatu)', kujitoa kunaweza kuanza tu baada ya mwaka.

- ***Adhabu ya Kifo***

Ingawa Mahakama haioni matumizi ya adhabu ya kifo na nchi kama kosa la asili, hata hivyo imeweka msimamo mkali katika matumizi yake, na imebatilisha hukumu za mahakama za kitaifa ambazo zilishindwa kukidhi vigezo. Katika shauri la Rajabu na Wenzie dhidi ya Tanzania, Mahakama ilifuata hoja za Tume katika mashauri yaliyopita kama vile Interights na Wenzake (kwa niaba ya Bosch) dhidi ya Botswana, na International Pen na Wengine (Ken Saro-Wiwa) dhidi ya Nigeria ambapo sharti la kutoa adhabu ya kifo ilielezwa inajumuisha: uwepo wa kifungu cha sheria, kutolewa na mahakama yenye mamlaka, na kufuata utaratibu unaofaa. Katika shauri la Ally Rajabu, Mahakama iliamua kwamba ulazima wa kutoa adhabu ya kifo kwa kosa la mauaji chini ya kifungu cha ya 197 ya Kanuni za Adhabu za Tanzania, ni ukiukwaji wa haki ya kuishi ya mleta maombi chini ya ibara ya 4 ya Mkataba wa Afrika.

Hii ilikuwa katika sababu kwamba masharti ya adhabu yanaweka wajibu kwa mahakama ulio wa moja kwa moja na usio wa moja kwa moja. Haimpi nafasi mtuhumiwa kutoa ushahidi wowote wa kupunguza adhabu wala haiipi nafasi mahakama ya kutumia sheria kutokana na msingi wa kila shauri. Mahakama ilikuwa na mtazamo kwamba huu ni ukiukwaji holela wa haki ya kuishi na usikilizaji wa shauri kwa ukamilifu.

Katika mashauri mengi yanayohusisha adhabu ya kifo, Mahakama imepitisha hatua za muda zinazozitaka nchi husika kusitisha adhabu iliyopitishwa na Mahakama ya kitaifa mpaka Mahakama itakapoamua msingi wa shauri ili kuzuia madhara yasiyorekebishika.

- ***Matendo ya ukatili, unyama na udhalilishaji***

*Nguza dhidi ya Tanzania* (23 Machi 2018)

Katika shauri hili, waleta maombi walishatakiwa, walikutwa na hatia na kuhukumiwa kwa kosa la kubaka na kulawiti. Walileta malalamiko wakidai mwenendo wa shauri usio wa haki uliokiuka utaratibu ikiwemo haki ya kutofanyiwa vitendo vya kikatili, kinyama na kidhalilishaji. Ingawa Mahakama iliamua kwamba waleta maombi hawajatoa ushahidi wa kutosha wa kuthibitisha kwamba mwenendo wa utaratibu katika mahakama ya kitaifa ulikiukwa, ila kulikua na ushahidi kwamba waleta maombi walizuiwa kurejea maelezo ya mashahidi na kuhojiwa kwa mashahidi. Vile vile,

Mahakama ilibaini kwamba kulikua na ukiukwaji wa haki chini ya Mkataba wa Afrika na wajibu mawasiliano kwa kushindwa kufanya kipimo cha uhanithi kama mleta maombi alivyodai na kutokuwepo eneo la tukio wakati wa tukio katika madai hayo.

- ***Ulinzi sawa mbele ya Sheria***

*Evarist dhidi ya Tanzania* (21 Septemba 2018)

Mleta maombi alikutwa na hatia na kuhukumiwa miaka 30 jela na alikua anadai mapungufu katika mwenendo wa shauri la jinai ikiwemo uwakilishi wa kisheria katika kupata msaada wa kisheria. Mahakama ilibaini ukiukwaji wa haki za binadamu chini ya ibara ya 7 ya Mkataba wa Afrika, ikionyesha kwamba 'msaada wa kisheria unaotolewa bure na unafangamana na haki ya usikilizwaji kwa ukamilifu.

- ***Kuondolewa Utaifa***

*Anudo dhidi ya Tanzania* (22 Machi 2018)

Katika shauri hili mleta maombi alizaliwa Tanzania, aliponyan'ganywa uraia alifukuzwa kwenda Kenya. Kenya ilimfukuza kurudi Tanzania lakini bahati mbaya hakuweza kuingia Tanzania na hivyo akabaki Sirari (ardhi isiyo ya mtu) mpaka wa Tanzania na Kenya. Mahakama ilibaini kwamba Mleta maombi alifukuzwa nchini Tanzania kiholela na kulikua na ukiukwaji wa haki ya utaifa chini ya ibara ya 15 (2) ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu.

## Takwimu za mashauri katika Mahakama ya Afrika

| **Mwaka** | **Maombi Yaliyo-pokelewa** | **Amri zilizo-tolewa** | **Hukumu/ Maamuzi** |
|---|---|---|---|
| 2020 | 48 | 34 | 26 |
| 2019 | 66 | 33 | 28 |
| 2018 | 33 | 4 | 17 |
| 2017 | 37 | 4 | 8 |
| 2016 | 59 | 23 | 8 |
| 2015 | 33 | 2 | 3 |
| 2014 | 3 | 1 | 6 |
| 2013 | 7 | 5 | 6 |
| 2012 | 7 | 0 | 4 |
| 2011 | 14 | 2 | 9 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2008 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **310** | **108** | **115** |
| **Jumla Kuu** | **533** | | |

Maelezo yote yanayohusu mashauri yanaweza kupatikana katika (African Court Law Reports) Juzuu mbili zimechapishwa mpaka sasa. Juzuu ya Kwanza (mwaka 2006-2016) na Juzuu ya pili (mwaka 2017-2018).

## Mafanikio na Changamoto ya Mahakama ya Afrika

### Mafanikio

Mahakama ya Afrika imekuwa na jukumu kubwa kukuza fasihi ya haki za binadamu katika Afrika. Tangu kuanzishwa kwake, Mahakama imeshughulikia maombi zaidi ya 300, ikionyesha kukubalika kwake na ufikiwaji wake kwa ujumla. Kwa miaka mingi imeongoza sayansi ya falsafa ya sheria kuhusu masuala kama adhabu ya kifo, uhuru wa kujieleza, haki za jamii za wazawa, na haki za mazingira na maendeleo. Mara nyingi hii imekuwa na athari ya kugeuza maamuzi ya mahakama za ndani ya nchi nyingi na kutoa fasiri mpya au pana kuhusu baadhi ya haki na kuhamasisha mabadiliko katika mifumo ya ndani iliyosanifu na ya utaratibu.

Katika mashauri ya *Norbert Zongo na Wengine dhidi ya Burkina Faso* na *Lohé Issa Konaté dhidi ya Burkina Faso*, kwa mfano, Mahakama ilitoa jukumu kubwa kwa maafisa wa umma katika kuheshimu haki na uhuru wa kujieleza kwa waandishi wa habari. Kufuatia mashauri haya Burkina Faso ilifanya marekebisho katika sheria yake katika kosa la kukashifu, na ilipanga upya utaratibu wa kimahakama ili kuboresha usahihi wa matokeo ya mashauri na uamuzi wa mahakama zake za ndani ya nchi. Pia mahakama katika nchi ya Kenya na Lesotho mara kwa mara zimekua zikitaja hoja zilizojadiliwa na Mahakama ya Afrika katika shauri la Konaté.

Marekebisho ya Kanuni za Mahakama ya mwaka 2020, yamesaidia Mahakama kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na imeangazia matamanio ya Mahakama katika kufanya maendeleo ya kila wakati kwa mahitaji ya sasa na mahitaji ya wadaawa

watarajiwa. Hii imefanya Mahakama ifikiwe kiurahisi zaidi. Hali hii imeoneshwa zaidi katika ushiriki wake katika vikao kwa mtandao (kama ilivyotumika wakati wa mlipuko wa UVIKO 19) ambapo bado ilijitahidi kuamua mashauri na kutoa hukumu.

Pia ukubwa wa mamlaka umeifanya Mahakama iwe taasisi muhimu ya kimaamuzi ya kikanda. Uwezo wake wa kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi, kufanya hukumu ya mfano, (chini ya kanuni ya 66 ya Kanuni za Mahakama za mwaka 2020) na mamlaka yake mapana ya kutoa ushauri imewezesha mahakama kujenga sayansi ya falsafa ya sheria na kuendeleza wigo mpana wa kulinda haki za binadamu ndani ya bara la Afrika.

Vilevile, uhuru wa Majaji unaongeza mafanikio ya Tume, ingawa uteuzi unatoka kwa nchi wanachama, majaji huchaguliwa kwa kupigiwa kura. Majaji hawaruhusiwi kusikiliza mashauri ambayo yanazihusisha nchi walizotoka na wabunge au watendaji hawawezi kuwa Majaji kwa wakati mmoja.

## Changamoto

Sio wanachama wote wa Umoja wa Afrika wameridhia Itifaki ya Mahakama (nchi 30 tu zimeridhia mpaka Juni 2021) na kumeendelea kuwepo kwa kasi ndogo katika kuridhia. Hii imesababisha malalamiko kutoka nchi hizo kupelekwa Tume tu.

Nchi wanachama chache zimetoa tamko chini ya ibara ya 34(6) ya Itifaki ya Mahakama kuruhusu mtu mmoja mmoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kufikia Mahakama. Baadhi ya nchi wanachama wametengua matamko yao kama ilivyojadiwa awali, wakilalamika kwamba fursa hii inadhoofishwa na inatumika kinyume na lengo la awali la uanzishaji wake. Baadhi ya nchi kama Benin wametoa wito wa marekebisho ya mfumo wa Mahakama. Hali hii imesababisha kupunguza uwezekano wa kufikiwa kwa Mahakama, na kupunguza nafasi ya Mahakama kama taasisi ya uamuzi inayoaminika katika kanda.

Pia kuna kukosekana kwa uelewa kuhusu Mahakama katika bara la Afrika, bado kuna uelewe usio sahihi kwamba Mahakama sio moja ya taasisi za Mahakama katika mfumo wa Umoja wa Afrika.

Ni Rais wa Mahakama tu anayefanya kazi kwa muda wote na majaji mengine wameajiriwa katika nchi zao na wanafanya kazi na

Mahakama kwa muda. Hii ina maana wanasikiliza mashauri mara chache wakati wa vikao vya Mahakama. Hii inachelewesha baadhi ya majukumu ya Mahakama kwa ajili ya kuamua mashauri kwa haraka.

## Mustakabali wa Mahakama ya Afrika

Mahakama ya Afrika inaweza kwa wakati ujao, ikaanzisha mfumo wa mahakama wa vyumba viwili vya majaji (ikiwa na nyongeza ya kitengo kinachoshughulikia migogoro kawaida baina ya nchi) au katika mfumo wa vyumba vitatu vya majaji (ikiwa na nyongeza ya kitengo kinachoghulikia uwajibikaji binafsi na wa kampuni katika jinai kwa makosa ya kimataifa na yanayovuka mipaka yanayohusisha nchi zaidi ya moja.




Mpaka Juni 2021, nchi nane tu zilikuwa zimeridhia Itifaki ya Mahakama Afrika ya Haki na Haki za Binadamu.

Mpaka kipindi hicho Itifaki ya Malabo ilikuwa haijaridhiwa na nchi yoyote.

# D. Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto

Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (Mkataba wa Afrika wa Watoto) ni kipimo muhimu cha mfumo wa haki za binadamu wa Afrika. Mkataba huo ulihamasishwa na masuala kadhaa ya kikanda yanayoihusu bara la Afrika ambayo hayakutajwa katika Mkataba wa Afrika wa mwaka 1981. Masuala yenye umuhimu hasa yalikuwa masuala yanayohusu usafirishaji haramu wa watoto, utumiaji wa watoto kama askari katika vita, mila na utamaduni wenye madhara pamoja na desturi nyingine katika maeneo mengi ya nchi za Afrika ambazo ni kinyume na haki za binadamu. Masuala haya, ambayo hayajaelezwa kwa ufasaha katika Mkataba wa Afrika na katika mikataba ya kimataifa na a kikanda ya haki za binadamu, ilionesha hitaji la kanuni inayoongozwa na muktadha maalum kwa ajili ya kukuza na kulinda hazi za binadamu na ustawi wa mtoto wa Afrika.

Aidha, Mkataba wa Afrika wa Watoto umeanzisha Kamati ya Afrika ya Wataalam wa Haki na Ustawi wa Mtoto (Kamati) ndani ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika kukuza na kulinda haki zilizotajwa katika Mkataba wa Afrika wa Watoto. Kwahiyo, Mwongozo huu unatoa muhtasari wa Mkataba wa Afrika wa Watoto na unaonyesha shughuli za Kamati , mfumo wake wa ufanyaji kazi, mafanikio na athari zake kwa haki za watoto katika bara la Afrika.

## Historia ya Mkataba wa Afrika wa Watoto

Mkataba wa Afrika wa Watoto ulipitishwa mnamo tarehe 11 Julai mwaka 1990, miaka tisa baada ya kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika. Mkataba wa Afrika pamoja na mikataba mingine ya haki za binadamu kwa wakati huo haikufafanua haki za watoto. Badala yake, marejeo ya haki za watoto yalikuwa kwa kiwango kidogo tu na katika muktadha wa haki za wanawake. Kwa mfano, ibara ya 18 (3) ya Mkataba wa Afrika unaeleza kwamba nchi itahakikisha uondoaji wa kila aina ya ubaguzi dhidi ya wanawake na pia itahakikisha ulinzi wa haki za wanawake na mtoto kama ilivyoainishwa katika Tamko na mikataba ya kimataifa. Hakuna ibara nyingine ya Mkataba

wa Afrika inayoshughulikia masuala pekee ya haki za binadamu yanayomkabili mtoto wa kiafrika.

Umoja wa Mataifa uliongoza njia kwa maendeleo ya mikataba ya kimataifa kuhusu haki za mtoto. Mwaka 1959, Umoja wa Mataifa ulipitisha Tamko la Haki za Mtoto. Baadae Nchi za Afrika zilipitisha Tamko la Haki na Ustawi wa Mtoto wa Afrika (Tamko) mnamo mwaka 1979. Tamko linatambua haja ya kuchukua hatua zote zinazofaa kukuza na kulinda haki na ustawi wa mtoto wa Afrika.

Mnamo 20 Novemba 1989, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto ulipitishwa. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto ulianza kutumika tarehe 2 Septemba 1990 kama mkataba wa kimataifa wa kwanza unaoelezea haki za watoto za kiraia, kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Ikiwa na nchi wanachama 196 hadi tarehe 21 Oktoba 2016, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto ni mkataba wa haki za binadamu ulioridhiwa zaidi katika historia. Nchi nyingi za Afrika ziliridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto katika hatua za awali za kuanza kwake kutumika. Hata hivyo, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto, haukugusa baadhi ya matatizo ya Afrika kama vile watoto wanaoishi chini ya ubaguzi wa rangi, unyanyasaji wa kijinsia, unyanyasaji wa kingono wa watoto wa kike, watoto ambao ni wanajeshi, ndoa za utotoni, wakimbizi watoto na mila zenye madhara. Kwa hivyo, kulikuwa na mahitaji katika bara la Afrika kuwa na mkataba tofauti wa kanda kuhusu haki za watoto, ambao ungeakisi changamoto mahususi za Afrika. Kikosi-Kazi cha Wataalam wa Afrika kuhusu haki na ustawi wa watoto kiliundwa mnamo mwaka 1979 ili kuandika Mkataba wa Afrika wa Watoto.

Mkataba wa Afrika wa Watoto unajumuisha maadili ya watu wote wakati ikiandaa dhana zake katika muktadha wa utamaduni wa Afrika. Mkataba huu hususan unazingatia urithi wa kiutamaduni, historia na maadili ya ustaarabu wa kiafrika. Kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika wa Watoto unaendana na utambuzi wa Umoja wa Mataifa wa ushirikishaji wa kikanda katika masuala ya haki za binadamu. Katika Azimio lake Na. 45/167, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa umesisitiza kwamba mipango ya kikanda ya kulinda na kukuza haki za binadamu inaweza kuwa na mchango mkubwa katika 'upatianaji wa haki za binadamu'. Kwa hivyo, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto na Mkataba wa Afrika wa Watoto haikinzani bali inaendana.

Mkataba wa Afrika wa Watoto ni mkataba wa kwanza wa kikanda ambao unatumia Mkataba Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto katika muktadha wa Afrika. Tangu kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika wa Watoto mwaka 1990, nchi wanachama wa Umoja wa Afrika 47 wameshauridhia (hadi kufikia Juni 2021).

## Estados-parte da Carta da Criança Africana



(Nchi 47 ambazo zimeridhia Mkataba wa Afrika wa Watoto zimeoneshwa katika rangi ya zambarau)

## Tarehe Muhimu

| | |
|---|---|
| 1 Julai1990 | Kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika wa Watoto Addis Ababa, Ethiopia |
| 13 Februari 1992 | Mkataba wa Afrika wa Watoto unaridhiwa kwa mara ya kwanza, (Shelisheli) |
| 29 Novemba 1999 | Mkataba wa Afrika wa Watoto unaanza kutumika |
| 11 Julai 2001 | Wajumbe 11 wa kwanza wa Kamati walichaguliwa |
| 29 Aprili- 2 Mei 2002 | Kikao cha kwanza cha kawaida cha Kamati |
| 22 Machi 2011 | Uamuzi wa Kamati katika shauri la Watoto wenye Asili ya Kinubi nchini Kenya |

# Sifa za kipekee za Mkataba wa Afrika wa Watoto

Mkataba unatoa viwango bora vya ulinzi kwa watoto kuliko Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto katika kujaribu kushughulikia baadhi ya changamoto katika bara la Afrika. Baadhi ya sifa zake za kipekee zimeonyeshwa hapa chini:

## Muktadha wa utamaduni

Katika dibaji yake Mkataba huu unafafanua kwamba urithi wa kiutamaduni, historia ya maadili ya ustaarabu wa kiafrika yanaoneshwa katika dhana ya haki na ustawi wa mtoto.

## Fasili ya mtoto (ibara ya 2)

Mtoto maana yake ni 'kila binadamu ambaye ana umri chini ya miaka 18. Tofauti na Mkataba wa Haki ya Mtoto hakuna mipaka, masharti au utofauti katika fasili ya mtoto. Badala yake, fasili husaidia kuongeza wanufaika wa ulinzi kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo.

## Maslahi bora ya mtoto (ibara ya 4)

Maslahi bora ya mtoto ni zingatio la msingi ambalo hupima hatua zote, sheria na sera zinazoathiri watoto. Tofauti na maelezo ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto kwamba maslahi bora ya mtoto ni msingi mkuu, Mkataba wa Afrika wa Watoto unafafanua viwango vya tathmini vya masuala yote yanayohusu

haki na ustawi wa mtoto.

## Jina na utaifa (ibara ya 6)

Kila mtoto ana haki ya kuwa na jina kuanzia anapozaliwa na pia ana haki ya kupata utaifa. Vilevile, kila mtoto anastahili kusajiliwa mara moja baada ya kuzaliwa. Nchi zinatakiwa kuhakikisha kwamba katika katiba za nchi zao watoto wanapata utaifa wao ikiwa wamezaliwa katika nchi husika na hakuna nyingine linawapa utaifa.

> 'Ingawa nchi hudumisha uhuru wake wa kuthibiti utaifa, kwa mtazamo wa Kamati ya Afrika, busara za nchi ni lazima ziwekewe ukomo na viwango vya haki za binadamu za kimataifa, katika mazingira haya Mkataba na mila ya sheria za kimataifa na kanuni za jumla za sheria ambazo zinalinda watu dhidi ya vitendo holela vya nchi. Hususan, nchi zinazuiwa katika busara zake za kutoa utaifa kwa wajibu wake wa kuhakikisha ulinzi sawa na kuzuia, kuepuka na kupunguza kukosa utaifa.' (Shauri la Watoto wenye asili ya Kinubi waliopo nchini Kenya, aya ya 48).

## Ulinzi dhidi ya desturi za kijamii na kiutamaduni zenye madhara (Ibara ya 21)

Mkataba wa Afrika wa Watoto unatoa jukumu kwa nchi kuchukua hatua zote muhimu za kukomesha desturi za kijamii na kiutamaduni zinazoathiri utu, ustawi, ukuaji wa kawaida na maendeleo ya mtoto. Mkataba unakataza ndoa za watoto na unaainisha umri wa chini wa kufunga ndoa uwe miaka 18 katika sheria za kitaifa.

> 'Kamati inapendekeza nchi wanachama watoe elimu kwa umma kuhusu kuacha desturi za kijamii na kiutamaduni na tabia nyingine zenye madhara kwenye haki na ustawi wa mtoto. Pia Kamati inapendekeza kuongezwa kwa vituo vya kulea watoto kwa ajili ya watoto wadogo maeneo ambayo wasichana wanalazimishwa kukaa nyumbani kuangalia watoto wadogo.' (Hitimisho lililopewa nchi ya Uganda na Kamati, mwaka 2010, Uk. 2-3)

## Watoto ambao ni wanajeshi (ibara ya 22)

Mtoto yeyote hatakiwi kuhusika moja kwa moja katika uhasama au kuajiriwa katika jeshi. Suala la watoto kuhusika katika vita ni changamoto kubwa kwa bara la Afrika na Mkataba unatoa viwango vikali sana kuliko viwango vya kimataifa. Kwa mfano, Itifaki ya Hiari ya Ushiriki wa Watoto katika Vita inaruhusu ushiriki wa hiari wa watoto kati ya umri wa miaka 16 na 18 lakini Mkataba hauruhusu.

## Watoto ambao ni wakimbizi (ibara ya 23)

Mtoto anayetafuta hadhi ya ukimbizi au anayechukuliwa kama ni mkimbizi ana haki ya kupata ulinzi unaofaa na msaada wa kibinadamu. Wakati Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Watoto unaweka masharti kuhusu watoto ambao ni wakimbizi katika mipaka, Mkataba umepanua wigo wa watoto ambao ni wakimbizi kujumuisha watoto waliohamishwa katika makazi ndani ya nchi. Sababu za kuhamishwa ndani ya nchi zimejumuishwa.

## Ulinzi dhidi ya siasa ya ubaguzi wa rangi na ubaguzi (ibara ya 26)

Kipaumblele cha kwanza kitawekwa kwenye mahitaji maalum ya watoto wanaoishi chini ya utawala wa kibaguzi na ambao nchi zao zina vurugu za kijeshi na msaada wa msingi utatolewa kwa watoto hao. Kwa kuwataja watoto walioathirika na ubaguzi wa rangi, Mkataba unakabiliana moja kwa moja na baadhi ya masuala muhimu kama ukosefu wa usawa na upatikanaji wa elimu bora inayoathiri watoto katika Afrika.

## Wajibu wa mtoto (ibara ya 31)

Watoto wa Afrika wamepewa majukumu ya kufanya kazi kwa mshikamano na familia, kuheshimu wazazi wao, wakubwa na wazee muda wote na wanatakiwa kusaidia wakati wa uhitaji, kutumikia taifa kupitia uwezo wao wa kimwili na kiakili na kutunza na kuimarisha maadili na utamaduni wa Mwafrka. Hata hivyo majukumu haya yanategemea umri na uwezo wa kila mtoto.

# E. Kamati ya Afrika ya Wataalam wa Haki na Ustawi wa Mtoto

## Uanzishwaji

Baada ya Mkataba kuanza kutumika mnamo tarehe 29 Novemba mwaka1999, Kamati iliundwa baada ya wajumbe wake kwa kwanza kuchaguliwa tarehe 11 Julai mwaka 2001 wakati wa kikao cha 37 cha Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Lusaka, Zambia.

## Muundo

Kamati ni kikundi cha watu wenye uaminifu, uadilifu, huru na utaalam katika masuala yanayohusu haki na ustawi wa mtoto. Wajumbe wa Kamati hupendekezwa na nchi wanachama na huchaguliwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika. Wajumbe wakishachaguliwa wanahudumu kwa uwezo wao binafsi. Zamani chini ya ibara ya 37(1) ya Mkataba, wajumbe walikua wanachaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano na walikuwa wanastahiki kuchaguliwa tena. Hata hivyo, kupitia uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika,(Assembly/AU/Dec.548 (XXIV), ibara ya 37(1) ilirekebishwa na kwa sasa wajumbe wa Kamati wanaweza kuchaguliwa tena mara moja tu.

## Ofisi

Kamati inachagua Mwenyekiti, Makamu wenyeviti watatu, Katibu na Katibu Msaidizi miongoni mwa wajumbe wake. Wanachaguliwa kwa muhula wa miaka miwili na wanastahiki kuchaguliwa tena.

## Sekretarieti

Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika huteua Katibu wa Kamati. Sekretarieti inawajibu wa kuisaidia Kamati. Wajumbe wake wanahudumia kama kiungo cha mawasiliano yote kuhusu Kamati na kutunza nyaraka za Kamati. Tarehe 21 Disemba 2020, Sekretariati ya Kamati ilihamia Maseru (Lesotho), kwa mujibu wa uamuzi wa Baraza la Utendaji la

Umoja wa Afrika. Ofisi ya Kamati ilizinduliwa rasmi mnamo tarehe 16 Juni 2021.

***Mamlaka ya Kamati***

Ibara ya 42 ya Mkataba inatoa mamlaka ya Kamati

- Kukuza na kulinda haki zilizowekwa kwenye Mkataba. Kamati inakusanya na kuhifadhi taarifa, kutathmini hali kuhusu changamoto zinazohusu haki za watoto, kupanga mikutano, kuhimiza taasisi za kitaifa na za ndani ya nchi na ikiwa kuna umuhimu inatoa maoni yake na mapendekezo kwa serikali. Kamati huandaa 'Kanuni' kwa maana ya 'principles' na 'rules' zinazoendana, na hushirikiana na taasisi zingine katika Bara la Afrika, kimataifa na kikanda na mashirika.
- Kufuatilia utekelezaji kuhakikisha ulinzi wa haki zilizowekwa ndani katika Mkataba.
- Tafsiri ya masharti ya Mkataba kwa ombi la nchi mwanachama, taasisi ya Umoja wa Afrika au mtu yoyote au taasisi inayotambuliwa na Umoja wa Afrika.
- Utekelezaji wa majukumu mengine wanayoelekezwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali.

## Kanuni za Utaratibu

Shughuli na taratibu za Kamati zinaratibiwa na Kanuni za Utaratibu Kamati ilijadili rasimu ya Kanuni za Taratibu katika mkutano wa uzinduzi mwaka 2002. Baadae Kanuni zilirekebishwa na toleo la mwisho la mwaka 2003 linasimamia mwenendo wa shughuli za Kamati.

### Wajumbe wa Kamati

***Wajumbe wa Kamati (hadi Juni 2021)***

**Mwenyekiti**
Joseph Ndayisenga – Burundi (2019 - 2021)
(Katibu Maalum wa watoto anayemaliza muda wake)

**Makamu wa Pili-Mwenyekiti**
Sidikou Aissatou Alassane Moulaye – Niger (Juni 2018 - Juni 2023)
(Katibu Maalum Kuhusu Ushiriki wa Watoto)

**Katibu**

Hermine Gatsing Kembo – Kamerun (Januari 2019 - Januari 2024)
(Katibu Maalum wa Majukumu ya Mzazi na Mtoto)

Anne Musiwa - Zimbabwe (Machi 2021 - Machi 2026)

**Wajumbe Wengine wa Kamati**

(Katibu Maalum wa Afya, Ustawi na Maendeleo)
Aboubekrine El Jera - Mauritania (Machi 2021 - Machi 2026)

(Katibu Maalum wa Ukiukwaji wa Haki dhidi ya Watoto)
Aver Gavar - Nigeria (Julai 2015 - Julai 2020)

(Katibu Maalum wa Watoto Wanaokinzana Sheria)
Theophane Nikyema - Burkina Faso (Machi 2021 - Machi 2026)

(Katibu Maalum wa Watoto na Wanaoshiriki katika Vita)
Robert Doya Nanima – Uganda (Machi 2021 – Machi 2026)

(Katibu Maalum wa Haki ya Jina, Usajili wa Vizazi na Utaifa)
Karoonawtee Chooramun – Mauritius (Machi 2021 - Machi 2026)

(Katibu Maalum wa Elimu)
Moushira Khattab – Misri (Juni 2018 – Juni 2023)

(Katibu Maalum wa Watoto walio katika mazingira hatarishi)
Wilson Almeida Adão (Machi 021 - Machi 2026)

**Wajumbe waliopita wa Kamati/Wajumbe wa Kamati Waliopita**

Dawlat Hassan (2006 - 2011) Misri
Fatima Delladj-Sebba (2010 - 2015) Algeria
Amal Muhammad Al-Hengari (2010 - 2015) Libya
Azza Ashmawy (2013 - 2018) Misri
Dirius Dialé Dore (2001 - 2003) Guinea
Dior Fall Sow (2001 - 2005) Senegali
Jean-Baptiste Zoungrana (2003 - 2008) Burkina Faso
Peter Ebigbo (2003 - 2008) Nigeria
Nakpa Polo (2003 - 2008) Togo
Suzanne Aho-Assouma (2013 - 2018) Togo
Seynabou Ndiaye Diakhaté (2003 - 2008) Senegali
Marie Chantal Koffi Appoh (2005 - 2010) Côte d'Ivoire
Moussa Sissoko (2005 - 2010) Mali
Cyprien Adébayo Yanclo (2007 - 2013) Benin
Agnès Kabore Ouattara (2007 - 2013) Burkina Faso
Maryam Uwais (2007 - 2013) Nigeria
Joyce Aluoch (2001 - 2005) Kenya
Rebecca Mirembe Nyanyintono (2001 - 2003) Uganda
Stratton Nsanzabaanwa (2001 - 2005) Rwanda
Assefa Bequele (2003 - 2008) Ethiopia
Martha Koome (2005 - 2010) Kenya
Felicité Muhimpundu (2010 - 2015) Rwanda
Rudolph Soh (2001 - 2005) Kameruni
Nanitom Motoyam (2001 - 2005) Chad
Julia Sloth Nielsen (2011 - 2016) Afrika Kusini
Karabo Karabo Mohau (2001 - 2003) Lesotho
Louis Pierre Robert Ahnee (2001 - 2005) Mauritius
Lulu Tshiwula (2001 - 2005) Afrika Kusini
Mamosebi T. Pholo (2005 - 2010) Lesotho

Boipelo Lucia Seithlamo (2005 - 2010) Botswana
Andrianirainy Rasamoely (2007 - 2012) Malagalasi
Alfas M Chitakunye (2010 - 2015) Zimbabwe
Julius Clement Mashamba - Tanzania (Julai 2015 - Julai 2020)
Dikere Marie Christine Bocoum – Cote d'Ivoire (Julai 2015 - Julai 2020)
Goitseone Nanikie Nkwe - Botswana (Julai 2015 - Julai 2020)
Maria Mapani-Kawimbe - Zambia (Julai 2015 - Julai 2020)
Benyam Dawit Mezmur – Ethiopia (Julai 2015 - Julai 2020)

## Vikao vya Kamati

Mikutano ya mara kwa mara inajulikana kama 'vikao' chini ya Kanuni za Utaratibu. Kila kikao kinafanyika kwa kipindi kisichozidi wiki mbili. Kamati ina aina mbili za vikao; vikao vya kawaida na vikao vya maalum. Kamati ilifanya kikao chake cha uzinduzi tarehe 29 Aprili 2002.

### Vikao vya kawaida

Kamati inafanya vikao vyake vya kawaida mara mbili kwa mwaka. Vikao vya kawaida vya Kamati ni jukwaa kwa ajili ya kutekeleza mamlaka yake kisheria. Katika vikao hivyo, Kamati hufanya shughuli muhimu sana kama vile:

- Kuitisha vikao vya faragha, maombi ya hadhi ya uangalizi, ripoti ya Katibu Maalum, ripoti ya mtaalamu elekezi (wataalamu el-ekezi), andiko la awali kuhusu sherehe za mtoto wa Afrika za Mwaka, kuchagua ofisi mpya na masuala mengine ya ndani.
- Kupokea mawasilisho kutoka wa wabia kama taasisi za Umoja wa Mataifa, kimataifa na Mashirika Yasiyo ya Serikali ya ndani nchi.
- Kutoa muhtasari na taarifa kuhusu masuala maalum, mada, misheni za uchunguzi na matokea ya vikao na taasisi zingine za Umoja wa Mataifa.
- Kuzingatia ripoti za nchi wanachama.
- Uwasilishaji wa maoni ya jumla kuhusu masharti ya Mkataba wa Watoto wa Afrika.

Hadi Juni 2021, Kamati imefanya vikao 37 vya kawaida na kimoja maalum.

### Vikao maalum

Vikao maalum vya Kamati huitishwa na Mwenyekiti kama Kamati inaamua hivyo. Kama Kamati haipo katika vikao, Mwenyekiti

anaweza kuitisha kikao maalum cha Kamati kwa kushauriana na Ofisi. Mwenyekiti wa Kamati anaweza pia kuitisha vikao maalum:

- Kwa ombi la maandishi la wajumbe wa Kamati walio wengi.
- Kwa ombi la maandishi la nchi wanachama wa Mkataba wa Watoto.

Kamati imekua na kikao kimoja maalum, kilichofanyika Addis Ababa kuanzia tarehe 7 hadi 11 Oktoba 2014, ambacho kilijadili ripoti za nchi za Ethiopia, Guinea, Kenya, Msumbiji na Afrika Kusini.

Kamati inapaswa kuwasilisha ripoti zake za shughuli zilizofanyika katika kutekeleza Mkataba wa Watoto na ripoti nyingine zozote zinazofaa kwa Mkutano wa Umoja wa Afrika kupitia Baraza la Utendaji.

## Vikao vya kawaida vya Kamati tangu mwaka 2001

| Kikao cha | Tarehe | Nchi mwenyeji |
|---|---|---|
| 1ª | 29 Aprili- 3 Mei 2002 | Ethiopia |
| 2ª | 17 - 21 Februari 2003 | Ethiopia |
| 3ª | 10 - 14 Novemba 2003 | Ethiopia |
| 4ª | 24 - 29 Mei 2004 | Ethiopia |
| 5ª | 8 - 12 Novemba 2004 | Ethiopia |
| 6ª | 13 - 17 Juni 2005 | Ethiopia |
| 7ª | 19 - 21 Disemba 2005 | Ethiopia |
| 8ª | 27 Novemba - 1 Disemba 2006 | Ethiopia |
| 9ª | 29 - 31 Mei 2007 | Ethiopia |
| 10ª | 2 - 5 Mei 2008 | Misri |
| 11ª | 26 - 28 Mei 2008 | Ethiopia |
| 12ª | 3 - 5 Novemba 2008 | Ethiopia |
| 13ª | 20 - 22 Aprili 2009 | Ethiopia |
| 14ª | 16 - 19 Novemba 2009 | Ethiopia |
| 15ª | 15 - 19 Machi 2010 | Ethiopia |
| 16ª | 9 - 12 Novemba 2010 | Ethiopia |
| 17ª | 22 - 25 Machi 2011 | Ethiopia |
| 18ª | 27 Novemba- 1 Disemba 2011 | Algeria |
| 19ª | 26 - 30 Machi 2012 | Ethiopia |

| | | |
|---|---|---|
| 20[a] | 12 - 16 Novemba 2012 | Ethiopia |
| 21[a] | 15 - 19 Aprili 2013 | Ethiopia |
| 22[a] | 4 - 8 Novemba 2013 | Ethiopia |
| 23[a] | 9 - 16 Aprili 2014 | Ethiopia |
| 24[a] | 1 - 6 Disemba 2014 | Ethiopia |
| 25[a] | 20 - 24 Aprili 2015 | Ethiopia |
| 26[a] | 1 - 19 Novemba 2015 | Ethiopia |
| 27[a] | 2 - 6 Mei 2016 | Ethiopia |
| 28[a] | 21 Oktoba - 1 Novemba 2016 | Banjul |
| 29[a] | 2 - 9 Mei 2017 | Maseru, Lesotho |
| 30[a] | 6 - 16 Disemba 2017 | Khartoum, Sudan |
| 31[a] | 4 - 24 Mei 2018 | Mali* |
| 32[a] | 12 - 20 Novemba 2018 | Ethiopia |
| 33[a] | 18 - 28 Machi 2019 | Ethiopia |
| 34[a] | 25 Novemba - 5 Disemba 2019 | Misri |
| 35[a] | 31 Agosti - 8 Septemba 2020 | Kwa mtandao |
| 36[a] | 23 Novemba - 4 Disemba 2020 | Kwa mtandao |
| 37[a] | 15 Machi - 26 Machi 2021 | Kwa mtandao |

### Vikao Maalum vya Kamati

| Kikao maalum cha | Tarehe | Nchi Mwenyeji |
|---|---|---|
| 1[a] | 7 - 11 Oktoba 2014 | Ethiopia |

## Mawasiliano na maamuzi

Katika kuhakikisha kwamba kuna ulinzi wa haki za watoto na nchi mwanachama, Kamati inaweza kupokea mawasiliano (malalamiko) kutoka kwa mtu yeyote, kikundi au Shirika Lisilo la Kiserikali linalotambuliwa na Umoja wa Nchi huru za Afrika/Umoja wa Afrika, nchi mwanachama au Umoja wa Mataifa kuhusu suala lolote lilitajwa katika Mkataba. Kila mawasiliano kwa Kamati lazima yawe na jina na anuani ya mwandishi na inatakiwa yashughulikiwe kwa siri. Mpaka sasa, Kamati imepokea mawasiliano manne dhidi ya nchi wanachama na imeshatoa maamuzi yake katika mashauri matatu miongoni mwa hayo.

## Msaada wa Kisheria

Kamati inaweza, kwa ombi la mlalamikaji au kwa uamuzi wake yenyewe kuwezesha upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa mlalamikaji kwa maslahi ya haki na kwa kutumia rasilimali zake zilizopo. Msaada wa kisheria utawezeshwa ikiwa Kamati imeshawishika kwamba:

- Ni muhimu kwa utekelezaji unaofaa wa majukumu ya Kamati, na kuhakikisha usawa kati ya wahusika wa shauri mbele yake; na
- Mlalamikaji hana uwezo wa kukidhi gharama zote au sehemu ya gharama zinazohusika.

## Mamlaka ya Kamati

Mamlaka ya Kamati yanaamuliwa kutegemeana na umri wa mtoto wakati wa ukiukwaji unaodaiwa kutokea. Pale ambapo mawasiliano yamewasilishwa na Kamati isipokuwa hayajahitimishwa kabla ya siku ya mtoto kutimiza miaka 18, Kamati itabaki na mamlaka yake ya kuendelea kushughulikia mawasiliano.

## Vigezo vya kupokea mawasiliano (kifungu cha 9(1) cha Mwongozo wa Mawasiliano

Kwa ajili ya mawasiliano kupokelewa ni lazima ikidhi vigezo vifuatavyo:

- Mawasiliano yaendane na masharti ya Sheria ya Uendeshaji ya Umoja wa Afrika na Mkataba wa Afrika wa Watoto.
- Mawasiliano hayatategemea tu taarifa zilizoenea na vyombo vya habari au haina msingi wowote.
- Mawasiliano hayaibui masuala ambayo yanasubiri kusuluhishwa au yalishasuluhishwa na taasisi nyingine ya kimataifa au utaratibu kwa mujibu wa mkataba wowote wa Umoja wa Afrika na kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa.
- Mawasiliano yamewasilishwa baada ya kutumia nafuu zinazopatikana ndani ya nchi, isipokuwa tu ikiwa ni dhahiri kwamba utaratibu huu ni wa muda mrefu na hauna ufanisi.
- Mawasiliano yanawasilishwa ndani ya muda stahiki baada ya kutumia nafuu za ndani ya nchi katika ngazi ya kitaifa.
- Mawasiliano yasiwe na lugha yoyote ya dharau au kashfa.

## Utaratibu wa mawasiliano

Mawasiliano yanayopelekwa kwa Kamati yanawasilishwa kwa Sekretarieti ambayo hufanya mapitio ya awali na mchakato wa mawasiliano huwa kama ifuatavyo:

- Sekretarieti hupokea mawasiliano, kuyapa jina na namba, kuyasajili, kurekodi tarehe ambayo mawasiliano yalipokelewa, kukiri kupokea mawasiliano kutoka kwa mlalamikaji ndani ya siku 21 tangu tarehe ya kupokea.
- Katibu atahakikisha kwamba mawasiliano yamewasilishwa na Kamati kukidhi vigezo vya mtindo wa uandishi na maudhui yaliyotolewa chini ya kifungu cha 2 cha Mwongozo wa Mawasiliano.
- Endapo mawasiliano hayakidhi vigezo vya fomu na maudhui yaliyotolewa chini ya Kifungu cha 2 cha Mwongozo wa Mawasiliano, Sekretarieti hutoa ombi kwa mlalamikaji au mwakilishi wake kufuata kanuni na kutoa taarifa ndani ya siku 30 za ombi.
- Endapo Sekretarieti ina mashaka yoyote kama vigezo vya mawasiliano vimetimizwa, itashauriana na Mwenyekiti.
- Endapo Sekretarieti imeridhika kwamba taratibu zimefuatwa, hupeleka mawasiliano kwa Kamati.

## Hatua za awali

Kamati hupokea mawasiliano ambayo yanaonesha hali ya uharaka, ukiukwaji mkubwa wa Mkataba wa Afrika wa Watoto na uwezekano wa kutokea madhara yasiyorekebishika kwa mtoto au watoto. Endapo Kamati inafikiri kwamba moja au zaidi ya sababu zilizotajwa hapo juu zipo kwenye mawasiliano, Kamati inaweza kwa uamuzi wake yenyewe au kwa kuombwa kwa mhusika katika shauri, kuiomba nchi mwanachama inayohusika kuchukua hatua za awali kuzuia madhara makubwa au yasiyoweza kurekebishika kwa mwathiriwa au waathiriwa wa ukiukwaji haraka iwezekanavyo.

## Usuluhishi

Wahusika wa mawasiliano wanaweza kusuluhisha wakati wowote kabla ya uamuzi wa Kamati kuhusu msingi wa shauri. Katika mashauri yote yanayoweza kuamuliwa kwa usuluhishi, masharti ya makubaliano yaliyofikiwa lazima yawe katika misingi ya kuheshimu haki za binadamu na ustawi wa mtoto unaotambulika na Mkataba wa Watoto wa Afrika na mikataba mingine inayotumika.

Kamati ambayo itahitimisha usikilizwaji wa mawasiliano. Kamati inaweza, kwa kuzingatia mamlaka yake kisheria chini ya Mkataba wa Afrika wa Watoto, kuamua kuendelea usikilizwaji wa mawasiliano bila kujali notisi ya usuluhishi huo.

Usuluhishi wa kwanza kufanywa na Kamati ulifanyika mwaka 2016 katika shauri la Taasisi ya Haki za Binadamu na Maendeleo Afrika dhidi ya Serikali ya Malawi (2016). Mleta maombi alidai kwamba masharti yaliyomo katika Katiba ya Malawi yanafasili mtoto kuwa mtu chini ya miaka 16 badala ya 'chini ya miaka 18' kama ilivyo katika ibara ya 2 ya Mkataba wa Afrika wa Watoto inajumuisha ukiukwaji wa haki. Kama sehemu ya mchakato wa maamuzi yaliyofikiwa, Serikali ya Malawi ilikubali kuchukua hatua kufanya mabadiliko husika katika Katiba yake, na kuhakikisha kwamba katika kipindi muda mfupi watu wote katika kundi hili wanapaswa kupata haki zote zinazotolewa chini ya Masharti ya Mkataba. Pia ilikubali kuwasilisha ripoti za maendeleo kuhusu hali, ambapo imewasilisha ripoti za mihula nne hadi kufikia mwaka 2018.

### Uamuzi na mapendekezo

Nchi mwanachama katika mawasiliano ambao Kamati imebaini kwamba kumekuwa na ukiukwaji wa ibara yoyote ya Mkataba wa Afrika wa Watoto lazima utoe taarifa kwa Kamati hatua zote zilizochukuliwa kutekeleza uamuzi wa Kamati ndani ya siku 180 toka tarehe ya kupokea uamuzi wa Kamati.

### Ufuatiliaji wa mapendekezo ya Kamati

Kamati huteua Katibu maalum kwa kila mawasiliano kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa uamuzi wa Kamati na nchi mwanachama husika.

## Maamuzi

- ***Talibés wa Senegali dhidi ya Jamhuri ya Senegali***

Mwaka 2012, mawasiliano yaliwasilishwa kwa Kamati kuhusu watoto wapatao 100,000 wa talibés nchini Senegal ambao walipelekwa katika shule za Qur'ani zinazojulikana kama 'daaras' (madrasa) kupata elimu ya dini. Ilibainika kwamba walimu wao wa dini, waliojukilana kama 'marabouts' waliwashurutisha watoto

hao kuombaomba mitaani na kwamba tabia hii imekuwepo tangu miaka ya 1980.

Kamati ilibaini kwamba Senegal ilikiuka ibara ya 11 ya Mkataba wa Afrika wa Watoto kwasababu ya kushindwa kwake kutoa elimu ya bure na ya lazima kwa watoto wote ambayo ni moja ya sababu zilizopelekea talibés walipelekwa na wazazi wao 'daaras' (madrasa).

Kulingana na uamuzi serikali lazima itekeleze sheria zake yenyewe kuwalinda talibés kutokana na udhalilishaji huu na kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa 'daaras' (madrasa) inawaandaa watoto hawa na elimu kamili na hairuhusu kuombaomba kwa kulazimishwa.

- ***Institute for Human Rights and Development in Africa na the Open Society Justice Initiative (kwa niaba ya watoto wa Kinubi wenye asili ya Kenya) dhidi ya Kenya***

Katika shauri hili, waleta maombi walidai kwamba Kenya imekiuka haki ya utaifa na usajili wa watoto wenye asili ya Kinubi nchini Kenya. Walidai kuwa wakati wa zamani za ukoloni, Wanubi walilazimishwa kuhama katika ardhi yao ambayo kwa sasa ni Somali ya kati na waliandikishwa katika jeshi la kikoloni la Kenya. Pia ililalamikiwa kwamba wakati wanubi wanaomba kurudishwa katika makazi yao ya asili walikataliwa na utawala wa kikoloni, Waingereza walishindwa kuwapa uraia wa uingereza katika Kenya kabla ya uhuru wa Kenya. Kwa kipindi kirefu baada ya uhuru, suala la utaifa wa wanubi halikushughulikiwa kabisa na sababu hawakuwa na ardhi ya mababu zao nchini Kenya, walilalamika kwamba Serikali ya Kenya inawafanya wao kama wageni. Hii ilisababisha suala la kwamba wazazi wengi wenye uzao wa Kinubi nchini Kenya kupata shida katika kusajili vizazi vya watoto wao.

Kamati iliamua kwamba 'kuna uhusiano thabiti na wa moja kwa moja kati ya usajili wa kizazi na utaifa. Uhusiano huu unasisitizwa na ukweli kwamba haki zote mbili zimetolewa chini ya ibara moja wa Mkataba wa Afrika wa Watoto (aya ya 42). Pia Kamati iliamua kwamba haikuwa katika maslahi ya mtoto kwamba nchi inataka mtoto wa kinubi asubiri mpaka umri wa miaka 18 kabla hawajaweza kuomba uraia wa Kenya. Kamati ilibaini ukiukwaji wa mara nyingi wa Mkataba wa Afrika wa Watoto na ilipendekeza kwamba Serikali ya Kenya ichukue hatua muhimu zote za kisheria (utungaji wa sheria), kiutawala na zingine ili kuhakikisha kwamba watoto wenye asili ya kinubi nchini Kenya, ambao vinginevyo wanakua hawana utaifa, wanaweza kupata utaifa wa Kenya na uthibitisho wa utaifa

huo wakati wa kuzaliwa.

- ***Hansungule na Wenzake (kwa niaba ya watoto wa Uganda Kaskazini) dhidi ya Uganda***

Shauri hili linahusu uasi na kukosa utulivu hali iliyokwepo Kaskazini mwa Uganda kwa takbirani miaka 20 kati ya mwaka 1986 na 2006. Wakati huu, Serikali ya Uganda ililazimika kushughulikia vitendo vya Jeshi la Waasi la Uganda (Lord's Resistance Army (LRA), ikijumuisha utekaji nyara wa maelfu ya watoto.

Kamati ilibaini kwamba 'utekelezaji wenye ufanisi wa sheria kwa umakini ni sehemu ya wajibu wa nchi wanachama chini ya Mkatabana hivyo kwa kushindwa kutunga sheria maalum ya kukataza kuajiri watoto katika jeshi, Uganda haijatimiza majukumu yake chini ya ibara ya 1(1) ya Mkataba wa Afrika wa Watoto. Kamati ilibaini kwamba katika kipindi cha 2001 hadi 2005, watoto waliandikishwa jeshini na walitumika katika Jeshi la Ulinzi la Uganda kinyume na ibara ya 22(2) ya Mkataba wa Afrika wa Watoto, ambao hauruhusu kuajiri watoto kwa hiyari katika vikosi vya Serikali.

- ***Institute for Human Rights and Development in Africa (IHRDA) dhidi ya Malawi (Mawasiliano Na. 4/Com/001/2014)***

Mawasiliano yaliletwa kwa niaba ya watoto wa Malawi yakipinga ibara ya 23 ya Katiba ya Malawi kwa sababu ilifasili mtoto kama mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 16. Mlalamikaji aliwasilisha kwamba ibara hiyo inakiuka ibara ya 2 ya Mkataba wa Afrika wa Watoto ambao unafasili mtoto kama mtu mwenye umri chini ya miaka 18. Pia mlalamikaji alidai kwamba ibara hiyo haiendani na ibara ya 1 (wajibu wa nchi wanachama) na ibara ya 3 (kutokuwa na ubaguzi) ya Mkataba wa Watoto sababu iliwatenga watoto wa Malawi wa miaka kati ya 16 na 18 kutoka kwenye ulinzi uliotolewa chini ya Mkataba wa Afrika wa Watoto. Walitoa hoja kwamba haki ya jina na utaifa; haki ya kujua na kulelewa na wazazi wako; haki ya kulindwa kutokana na unyonyaji au vitendo vyovyote kazi au adhabu ambayo ni hatari au inaweza kuwa hatari kwa maendeleo ya kiafya; kimwili; kiakili au kiroho au kijamii zitakiukwa na ibara hiyo.

Shauri hilo halikusikilizwa sababu pande husika katika shauri waliwasilisha ombi la kufanya usuluhishi. Ombi la kufanya usuluhishi lilikubaliwa na Kamati kulingana na kifungu cha 13 cha Mwongozo wa Mawasiliano Uliorekebishwa, ambao unaruhusu pande husika

katika mawasiliano kutatua mgogoro wao kwa usuluhishi muda wowote kabla Kamati haijaamua shauri baada ya ya kulisikiliza mawasiliano.

Baada ya kujadili kuhusu maelezo ya vigezo na masharti vya makubaliano ya usuluhishi, Kamati iliamua kufanya usuluhishi na wakati ikiendelea na usuluhishi wa mawasiliano hayo. Serikali ya Malawi ilikubali kufanya kila kitu kilicho ndani ya uwezo wake kurekebisha Katiba na sheria zingine husika ili ziendane na na ibara ya 2 ya Mkataba wa Afrika Kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto ifikapo tarehe 31 Disemba 2018 na kutoa taarifa mara kwa mara kwa Kamati kuhusu maendeleo yaliyofanywa katika kutekeleza Makubaliano haya.

Tangu wakati huo Malawi ilirekebisha Katiba yake kuongeza umri wa mtoto kuwa miaka 18. Pia Malawi iliwasilisha ripoti yake ya nne ya utekelezaji wa makubaliano ya usuluhishi, ikieleza kwamba Malawi iliandaa warsha kuhusu ulinganifu wa sheria katika fasili ya neno mtoto kutoka tarehe 14-15 Disemba 2017 na kwamba Malawi ilikua imepanga kupitia ripoti zake zilizounganishwa kuhusu Mkataba wa Afrika wa Watoto baadae mwezi huo.

## Maoni ya Jumla

Chini ya mamlaka yake ya kisheria ya kutafsiri, Kamati ina uwezo wa kutoa tafsiri sahihi ya Mkataba, ili kufafanua maana yake na wigo, na kuelezea majukumu ya nchi wanachama chini ya Mkataba wa Afrika wa Watoto. Kamati hutumia mamlaka yake kupitia utoaji wa 'Maoni ya Jumla', ambayo ni nyenzo za kawaida zinazotumika na vyombo vya mkataba kufafanua maana ya msingi na wigo wa ibara za mkataba, na pia kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu changamoto zinazohusu mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu.

Mpaka sasa, Kamati imetoa maoni ya Jumla matano. Hivi Karibuni, Kamati ikishirikiana na Tume ya Afrika Iimepitisha maoni ya jumla kuhusu kukomesha ndoa za utotoni. Maoni ya jumla mengine yanajumuisha maoni ya jumla ya ibara ya 31 ya Mkataba wa Afrika wa Watoto kuhusu Majukumu ya Watoto; Maoni ya Jumla ya ibara ya 30 kuhusu watoto wa wazazi waliofungwa na ibara ya 6 kuhusu usajili wa vizazi , jina na utaifa, na kuzuia kukosa utaifa.

- *Maoni ya Jumla Na. 1: (ibara ya 30 ya Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Watoto) kuhusu 'Watoto wa Wazazi waliofungwa gerezani na watoa huduma za msingi' 2013 (GC 1) ambalo linashughulikia watoto wa wazazi waliofungwa gerezani.*

Lengo kuu la GC1 ni kuwezesha uelewa wa ibara ya 30 ya Mkataba wa Afrika wa Watoto na kutoa mwongozo wa kiutendaji kuhusu utekelezaji wake kamili. Kwa mujibu wa Kamati, ibara ya 30 inatumika si kama mama tu bali baba na watoa huduma za msingi ambao wanaweza kuwa wazazi walezi au wanafamilia kwasababu watoto wengi wa Afrika ni yatima au walitenganishwa na wazazi wao lakini bado wanaweza kuwa wanahitaji ulinzi uliowekwa katika ibara ya 30.

Kamati pia iliandaa mwongozo mfupi kuhusu Maoni ya Juma ya 1 ili kurahisisha matumizi na uelewa wake. Mwongozo mfupi unaweza kupatikana kwenye: www.acerwc.org/general-comments/.

- *Maoni ya Jumla kuhusu ibara ya 6 ya Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto: 'Haki ya usajili wa kuzaliwa, jina na utaifa' (GC 2) inashughulika na suala la haki ya usajili wa kuzaliwa, jina na utaifa na kuzuia kukosa utaifa kwa watoto.*

Kamati imefanya utetezi mkubwa wa haki tatu zinazofungamana zilizo katika ibara ya 6(1), (2) na (3) ambazo ni: haki ya kuwa na jina; haki ya usajili wa kuzaliwa, na haki ya utaifa. Pia inafafanua wajibu wa nchi kuhusu utekelezaji wa haki ya utaifa (ibara ya 6 (4)). Lengo la maoni ya jumla ni kutoa maana wigo wa haki hizi na kuelezea majukumu husika ya nchi wanachama wa Mkataba kwa ajili ya utekelezaji. Maoni haya ya jumla yanaelekezwa kwa wadau wote ambao wana wajibu katika utekelezaji wa Mkataba wa Afrika hususan haki zilizowekwa katika ibara ya 6. Hii inajumuisha mawakala wa nchi wanachama -bunge na mahakama mashirika ya kijamii, wanazuoni, mawakili na mamlaka za usajili wa matukio muhimu. Madhumuni yake makuu ni kufafanua kanuni zilizopo katika haki zilizomo katika ibara ya 6 na kuwapa wadau waliotajwa hapo juu mwongozo kuhusu utekelezaji wake katika utendaji.

- *Maoni ya Jumla kuhusu Ibara ya 31 ya Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto: 'Majukumu ya mtoto' (2017)*

Ibara ya 31 ya Mkataba wa Afrika wa Watoto imebuni kwa kuweka jukumu la mtoto ambaye, katika muktadha wa Afrika ana haki na anabeba majukumu kwa familia na jamii. Ibara hii ambayo imeendeleza kusudi la Mkataba wa Afrika katika suala la wajibu na haki, lakini pia inaweza kudhoofisha ulinzi wa haki za watoto, hususan kama nchi na watimiza majukumu wengine wanaamini

kuwa watoto wanapaswa kutetea haki zao kwa kutimiza majukumu yao.

Kwahiyo, Maoni ya Jumla yamekuja kwa wakati muafaka kuhakikisha kwamba wajibu wa watoto hauzuii utekelezaji wa haki zao na kwamba zinatafsiriwa kwa namna ambayo inaheshimu kusudi la haki za watoto- 'kukuza na kulinda haki halali na maslahi ya ustawi wa watoto'. Maoni ya Jumla kwa mfano hufafanua kanuni za msingi zinazoongoza ufafanuzi wa ibara ya 31 na kusisitiza umuhimu wa kutokutenganisha ibara ya 31 kutoka kwenye dhamana zingine ikiwemo katazo la desturi yenye madhara na uonyonyaji.

- *Maoni ya pamoja ya Jumla ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Kamati ya Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto Kuhusu Kumaliza Ndoa za Utotoni (2017).*

Janga la ndoa za utotoni lilihitaji fasili ya pamoja kutoka Tume ya Afrika na Kamati ya Afrika ya Watoto, kama wafasili wenye mamlaka ya Itifaki ya Maputo na Mkataba wa Afrika wa Watoto, ambayo yote inakataza kabisa ndoa za utotoni. Kwa hiyo Maoni ya Jumla hutaja ibara ya 6 (b) ya Itifaki ya Maputo na ibara 21(2) ya Mkataba wa Afrika wa Watoto. Ndoa za Utotoni huathiri wasichana kwa kiwango kikubwa kuliko wavulana. Pia inawaathiri watoto wenye ulemavu, watoto wahamiaji, watoto wakimbizi na watoto wanaoishi katika familia wanazoziongoza. Jitihada hizi za pamoja za kufafanua wajibu wa nchi kuzuia ndoa za watoto ni miongoni mwa baadhi ya jitihada zinazotokana na juhudi mbalimbali za Umoja wa Afrika kuzuia ndoa za utotoni katika bara la Afrika.

- *Maoni ya Jumla ya Ibara ya 22 ya Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto: 'Watoto katika' Mazingira ya Vita (Septemba 2020).*

Kamati ilifafanunua maudhui ya ibara ya 22, ambayo imekusudia kuhakikisha watoto wanalindwa wakati wa vita kwa msingi wa kanuni husika za sheria za kimataifa za haki za binadamu na sheria za kimataifa za kibinadamu. Maoni ya Jumla yanaweka wazi jinsi desturi za sheria za kimataifa za haki za binadamu na sheria za kimataifa za binadamu katika mazingira ya vita zinapaswa kuchangia katika kuboresha hali ya watoto. Ni sehemu ya mfumo sanifu ambao unaongeza ulinzi wa watoto walio katika mazingira ya vita na lazima utumike katika namna ambayo inaendana na kanuni za msingi za haki za binadamu zinazolinda watoto, ikiwemo maslahi bora ya mtoto, haki ya watoto ya ushiriki, kutobaguliwa, na haki ya kuishi, kuendelea kuishi na maendeleo. Maoni ya Jumla yanajadili kwa undani kuhusu maudhui ya kanuni zilizo katika ibara

ya 22 ya Mkataba wa Afrika wa Mtoto. Na mazingira ambayo inatumika, ambayo ni migogoro ya kivita ya kimataifa na isiyo ya kimataifa, mivutano na migongano.

Vilevile, Maoni ya Jumla yanafanunua jukumu la wadau husika, hususan taasisi za kitaifa haki za binadamu, jumuiya za kiuchumi za kikanda na mifumo ya kikanda, vyombo vya habari, sekta binafsi na makundi ya kijeshi yasiyo ya kiserikali, katika kuboresha hali ya watoto walioathirika na mzozo.

## Uwasilishaji wa ripoti ya nchi

Mchakato wa uwasilishaji wa ripoti ni njia ya kufuatilia utekelezaji wa wajibu wa nchi wanachama katika haki za watoto. Baada ya kuridhia Mkataba wa Watoto, kila nchi mwanachama huanza kuwasilisha ripoti kuhusu hatua walizochukua kutekeleza ibara na maendeleo yaliyofanyika katika upatikanaji wa haki zilizotolewa katika Mkataba (ibara ya 43). Mchakato wa kuandaa ripoti kwa ajili ya kuwasilisha kwa Kamati hutoa nafasi muhimu ya kufanya mapitio kamili ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa ili kulinganisha sheria za nchi na sera na Mkataba na kufuatilia maendeleo yaliyofanyika katika kufuatilia haki zilizohakikishwa katika Mkataba. Vilevile, mchakato unahimiza na unawezesha ushiriki unaokubalika, uchambuzi binafsi wa taifa na ukaguzi wa umma wa sera na programu za serikali, desturi za sekta binafsi na kwa ujumla desturi za sekta zote za jamii kwa watoto.

Kamati imepewa mamlaka ya kupokea na kupitia taarifa zilizowasilishwa na nchi wanachama kuhusu hatua ambazo wamechukua katika kutekeleza masharti katika Mkataba na maendeleo yaliyofanyika katika kufurahia haki hizi. Ibara ya 43 ya Mkataba inazitaka nchi wanachama kuwasilisha 'Ripoti ya Awali' ndani ya miaka miwili tangu kuanza kutumika kwa Mkataba, na kisha kuwasilisha 'Ripoti ya Muhula' kila baada ya miaka mitatu. Nchi mwanachama ambayo imewasilisha ripoti kamili ya kwanza kwa Kamati haitahitaji kurudia taarifa za msingi zilizokwishatolewa katika ripoti zake zilizopita katika ripoti zake zinazofuata zitakazowasilishwa kwa mujibu wa ibara ya 43 (3).

### Maudhui ya Ripoti

Kwa mujibu wa ibara ya 43(2) ya Mkataba, ripoti ya nchi

mwanachama huwasilishwa kwa Kamati ikieleza masuala yafutayo:

- Kujumuisha taarifa iliyojitosheleza kuhusu utekelezaji wa Mkataba ndani ya nchi mwanachama na kuonesha vigezo na changamoto kama zipo, zinazoathiri utekelezaji wa wajibu uliopo katika Mkataba.
- Taarifa inayotolewa na nchi mwanachama kuhusu utekelezaji wa kila ibara inapaswa kufanya rejea mahususi ya maoni ya hitimisho na mapendekezo yaliyopita ya Kamati na inajumuisha maelezo ya jinsi gani mapendekezo yametekelezwa au kushughulikiwa kwa vitendo.
- Endapo mapendekezo yaliyopita hayajatekelezwa au kushughulikiwa, nchi mwanachama inapaswa kueleza sababu ya kutotekeleza na kutoa maelezo namna na ndani ya muda ambao mapendekezo yatazingatiwa.
- Taarifa inayotolewa na nchi mwanachama kuhusu utekelezaji wa kila ibara iikijumuisha taarifa za takwimu na taarifa zilizogawanywa kwa mujibu wa vigezo husika ikiwemo umri, jinsia na ulemavu.
- Nchi wanachama wanapaswa kubainisha maoni na mabadiliko muhimu yaliyotokea katika kipindi cha kutoa taarifa.
- Takwimu zinapaswa kuwasilishwa kama kiambatisho tofauti cha ripoti ya muhula.

## Muundo wa Ripoti

- Ripoti inapaswa kuwasilishwa katika njia ya muhtasari na mpangilio. Lugha nyepesi na rahisi itatumika.
- Ripoti ya muhula haipaswi kuzidi kurasa 80 au maneno 3500. Ukomo wa kurasa au idadi ya maneno haitatumika kwa nyaraka (kwa mfano, maandiko ya kisheria) inayoambatishwa katika ripoti hiyo.
- Inapendekezwa kwamba ripoti iambatane na nakala za vifungu vya sheria husika, vitabu vya kisheria, kiutawala na vitabu vingine vilivyorejewa katika ripoti, ikiwa vinapatikana katika lugha inayotumika katika Umoja wa Afrika.
- Ripoti itaonesha maana ya vifupisho vyote vilivyotumika ndani yake, hususan pale ambapo ripoti inarejea, sheria, taasisi za kitaifa, mashirika, na kadhalika, ambayo sio rahisi kueleweka nje ya nchi mwanachama.
- Ripoti inapaswa kuwasilishwa katika moja ya lugha rasmi za Umoja wa Afrika.

## Mchakato wa kuwasilisha ripoti za nchi

Kamati imerahisisha mchakato wa nchi kuwasilisha ripoti, mchakato ambao unaweza kufupishwa kama ifuatavyo:

- Nchi mwanachama kuwasilisha ripoti kwa Kamati.
- Katibu anateuliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Kamati Kujadili hali ya haki za watoto kuhusiana na ripoti ya nchi mwanachama.
- Asasi za kiraia pia hualikwa kuwasilisha ripoti za ziada kwa Kamati kama zipo.
- Kikao cha Kikosi-Kazi kabla ya kikao cha Kamati hujumuisha mjadala na kubaini masuala kwa ajili ya mjadala na Nchi Mwanachama wakati wa kikao cha kawaida.
- Kikao cha wote (wazi) hufanyika ikiwa nchi mwanachama huwasilisha kwa mdomo na kwa ufupi kwamba ipo tayari kuwasilisha ripoti. Mara tu baada ya hapo, Kamati hujadili ripoti na Nchi Mwanachama.
- Kamati huandaa Hitimisho na mapendekezo ambayo hutekelezwa na Nchi mwanachama.

## Maoni ya Hitimisho

Mwisho wa mchakato wa kuwasilisha ripoti, Kamati hutoa mapendekezo na maoni kwa serikali ya nchi iliyowasilisha ripoti kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Watoto. Kamati huonesha maeneo makuu yenye changamoto katika haki zilizopo katika Mkataba wa Afrika wa Watoto na kisha kuhitimisha na kutoa maoni ya jumla. Maoni na mapendekezo ya Kamati huamualiwa katika kikao cha faragha.

***Mapendekezo na maoni yaliyotumwa na Kamati ya Afrika ya Wataalam wa Haki na Ustawi wa Watoto kwa Serikali ya Jamhuri ya Uganda kuhusu Utekelezaji wa Awali wa Ripoti ya Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (yamechapishwa mnamo Novemba2010)***

Katika hitimisho la mapitio ya Ripoti, Kamati ilipata heshima ya kutuma maoni na mapendekezo yafuatayo kwa Serikali ya Jamhuri ya Uganda:

Ibara ya 2: Fasili ya mtoto

Kwa ulinzi bora wa mtoto, Kamati inapendekeza nchi mwanachama kulinganisha maandiko yenye fasili ya mtoto kama ilivyotajwa katika Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto.

Ibara ya 6: Jina na Utaifa

Kamati inapendekeza nchi mwanachama kuhakikisha kwamba usajili wa watoto wakati wa kuzaliwa ni lazima na bure. Kamati ilihimiza Serikali kuongeza uelewa kuhusu mamlaka za mitaa na idadi za watu kuhusu athari za baadae za kutokusajili watoto katika masijala ya matukio muhimu.

Ibara ya 15: Ajira kwa mtoto

Kamati inapendekeza nchi mwanachama kufanya kampeni za kuongeza uelewa kwa kuzingatia wafanyakazi, vyama vya wafanyakazi, mashirika yasiyo ya kiserikali, na wadau wengine, kuhusu madhara ya kutumikisha watoto.

Aidha, Kamati ilipendekeza kwa Nchi Mwanachama kutumia vyombo vya habari kwa ajili ya taarifa na kuongeza kampeni za uelewa na kuunga mkono taasisi na mashirika yanayopambana kuzuia matukio ya kutumikisha watoto.

Ibara ya 22: Migogoro ya kivita

Kamati inaona kwamba ripoti haitoi taarifa za kutosha kuhusu hadhi ya watoto ambao ni askari nchini Uganda. Hivyo ilishauri taarifa zaidi ziwekwe kwenye ripoti zinazofuata.

Article 28: Matumizi ya dawa ya kulevya

Kamati imebaini kwamba ripoti haijazingatia hatua zinazofaa kuchukuliwa kulinda watoto dhidi ya utumiaji wa dawa za kulevya na inapendekeza kwamba hali ya matumizi ya vitu haramu na dawa za kulevya vilevile taarifa na mipango iliyochukuliwa kuzuia janga hili itajwe katika ripoti zinazofuata.

Andiko zima la Hitimisho la Kamati linapatikana: http://www.acerwc.org/concluding-observations/

## Misheni za uchunguzi

Mfumo unaosimamia misheni za Uchunguzi za Kamati ni Mwongozo wa Kufanya Uchunguzi. Katika Mwongozo, misheni ya uchunguzi ni misheni ya timu ya Kamati kwenda nchi mwanachama katika Mkataba kukusanya taarifa kuhusu hali ya haki na ustawi wa watoto katika nchi mwanachama (ibara ya 1). Kamati ina uwezo wa kupokea mawasiliano kutoka kwa mtu yeyote au kikundi cha watu au nchi kuhusu suala lolote na kutumia njia yoyote inayofaa ya kuchunguza suala lolote lilio katika eneo la Mkataba wa Watoto (ibara ya 44 na 45). Kwahiyo, Kamati inaweza kutumia busara zake kuchunguza nchi mwanachama ikiwa kuna taarifa za madai

ya ukiukwaji wa haki za watoto. Ziara za uchunguzi kama hizo ni muhimu kwa kupata uelewa wa uhakika wa ukiukwaji unaodaiwa na kutoa mapendekezo kwa nchi husika.

Baada ya kukamilika kwa misheni ya uchunguzi, Kamati inaandaa ripoti ambayo huwasilishwa kwa Baraza la Utendaji na inapitishwa na Mkutano wa Umoja wa Afrika. Ripoti hiyo inaweza kuchapishwa tu baada ya kupitishwa na Mkutano wa Umoja wa Afrika.

Pia Kamati ina utaratibu wa ufuatiliaji ambao huutaka nchi mwanachama iliyotembelewa kuwasilisha majibu maandishi kuhusu hatua yoyote iliyochukuliwa kutokana na mapendekezo yaliyofanywa katika ripoti ya misheni.

## Lengo

Lengo la misheni ya uchunguzi wa Kamati ni kutafuta na kukusanya taarifa sahihi na za kuaminika kuhusu suala lolote lililojitokeza kwenye Mkataba ili:

- Kutathmini hali ya jumla ya haki za watoto nchini; kufafanua ukweli na kuwawajibisha watu binafsi na serikali kwa watoto ambo ni waathiriwa wa na familia zao.
- Kukuza na kusaidia utekelezaji wa haki na ustawi wa mtoto na taasisi mbalimbali za kiutawala, kisheria na zinazotunga sheria katika nchi , kulingana na Mkataba( ibara ya 2 ya Mwongozo).

## Aina

Kwa mujibu wa ibara ya 3 ya Mwongozo wa Kamati inaweza kufanya misheni za aina 2:

- Uchunguzi wa suala lolote lililopelekwa kwenye Kamati
- Uchunguzi ulioanzishwa na Kamati

## Misheni za uchunguzi zilizofanywa na Kamati

- ***Uganda Kaskazini***

Kamati ilifanya misheni ya uchunguzi Uganda Kaskazini mnamo mwezi Agosti mwaka 2005 kutathmini hali ya watoto katika mgogoro katika nchi hiyo. Kamati iliwasilisha ripoti yake kwa Baraza la Utendaji la Umoja wa Afrika, Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu na Baraza.

- ***Sudani Kusini***

Kamati ilifanya ziara Sudani Kusini na kuanzia tarehe 3 hadi 9 Agosti 2014, ambapo ilikua na vikao vingi na Maafisa wa Serikali, Asasi za Kiraia za kitaifa na kimataifa na mashirika ya Umoja wa Mataifa.

- ***Jamhuri ya Afrika ya Kati***

Kati ya tarehe 15 na 20 Disemba 2014, Kamati ilikua Jamhuri ya Afrika ya Kati kutathmini madhara ya mgogoro wa kivita katika nchi hiyo kwa watoto. Misheni ilionesha uthabiti na ukosefu wa rasilimali kwa ajili ya kuzuia na kutatua hoja mbalimbali zinazowakabili watoto walioathirika na migogoro ya kivita.

- ***Tanzania***

Mnamo August 2015, Kamati ilifanya misheni ya uchunguzi kuhusu hali ya watoto wenye ulemavu wa ngozi katika makazi ya muda nchini Tanzania. Shirika lisilo la Kiserikali, Under the Same Sun ilisababisha uchunguzi kwa kuipa taarifa Kamati kuhusu hali ya kutisha ya watoto wenye ulemavu wa ngozi Tanzania. Kamati ilichapisha ripoti yake ya uchunguzi mwezi Machi 2016.

> Ripoti za misheni za uchunguzi uliofanywa na Kamati zinapatikana:
> http://www.acerwc.org/investigation/ missions-reports/

## Asasi za Kiraia na Kamati

Asasi za Kiraia (AZAKI) huunga mkono shughuli za Kamati. Kamati huzipa AZAKI hadhi ya uangalizi. AZAKI zikiwa na hadhi ya uangalizi na AZAKI nyingine zikifanya kazi za haki za watoto zimeanza kuandaa Jukwaa la AZAKI kabla ya vikao vya Kamati. Kikao cha kwanza cha Jukwaa la AZAKI kabla ya kikao cha Kamati kilifanyika kuanzia tarehe 17 hadi 19 Aprili 2009.

Katika kutathmini ripoti za nchi Kamati inaweza kupata taarifa za ziada kutoka kwa AZAKI ambazo zina hadhi ya uangalizi kwenye Kamati. Kamati huangalia lengo la ripoti ya nchi kwa msaada wa ripoti za ziada kutoka kwa AZAKI. Kwasababu hii, Kamati iliandaa mwongozo kwa AZAKI kukamilisha ripoti za nchi.

## Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu na Kamati

Tofauti na Tume ya Afrika, hakuna ushiriki rasmi kati ya Kamati na Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu. Hata hivyo, hakuna kitu chochote kinachowazuia Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu za nchi wanachama kuwa sehemu ya ujumbe wa kikao cha Kamati.

Mafanikio na Changamoto za Mkataba wa Afrika wa Watoto na Kamati.

## Siku ya Mtoto wa Afrika

Siku ya Mtoto wa Afrika husheherekewa tarehe 16 Juni kila mwaka. Ilipitishwa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika mwaka 1991 na kuendelea na Umoja wa Afrika. Siku ya Mtoto Afrika hutoa fursa kwa serikali, taasisi za kimataifa, na jamii kutoa upya ahadi zao katika kuboresha mazingira ya watoto kwa kuandaa shughuli zinazolenga ujumuishwaji. Siku ya mtoto Afrika ilianzishwa kama kumbukumbu ya zaidi ya wanafunzi 100 ambao waliuawa huko Soweto Afrika Kusini, na Serikali ya kibaguzi kwa kudai haki yao ya elimu bora na kufundishwa katika lugha yao wenyewe mnamo tarehe 16 Juni 1976. Matukio ya kila mwaka yanapangwa na Kamati kukuza haki za watoto. Mwaka 2016 kauli mbiu ilikua ni 'Vita na mgogoro katika Afrika: Kulinda haki zote za watoto.

### Siku ya Mtoto wa Afrika kauli mbiu toka mwaka 2002

| | |
|---|---|
| 2021 | Miaka 30 baada ya kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika: kuharakisha utekelezaji wa Ajenda 2040 kwa Afrika inayofaa kwa watoto |
| 2020 | Upatikanaji wa mfumo rafiki kwa mtoto katika Afrika |
| 2019 | Vitendo vya Kibinadamu katika Afrika: Haki za Watoto Kwanza |
| 2018 | Mtoto Yeyote Asiachwe Nyuma kwa ajili ya Maendeleo ya Afrika |
| 2017 | Ajenda 2030 kwa ajili ya Maendeleo Endelevu kwa Watoto wa Afrika: Kuongeza Ulinzi, Uwezeshaji na Fursa Sawa |
| 2016 | Vita na Migogoro katika Afrika: Kulinda Haki zote za Watoto |
| 2015 | Miaka 25 Baada ya Kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika wa Watoto: Kuongeza Juhudi za Pamoja Katika Kukomesha Ndoa za Utotoni katika Afrika |

| | |
|---|---|
| 2014 | Elimu rafiki, bora, bure ni ya lazima kwa watoto wote |
| 2013 | Kukomesha desturi za kijamii na kiutamaduni zinazowathiri watoto: Wajibu wetu sote |
| 2012 | Haki za watoto wenye Ulemavu: Jukumu la kulinda, kuheshimu, kukuza na kutimiza |
| 2011 | Wote pamoja kwa ajili ya watoto wa mtaani |
| 2010 | Kupanga na kuandaa bajeti kwa ajili ya haki za mtoto: Wajibu wa Pamoja |
| 2008 | Afrika inayofaa kwa Watoto: Wito wa kuharakisha hatua kwa ajili ya kuokoa maisha ya mtoto |
| 2007 | Haki ya kushiriki: Watoto waonekane na kusikilizwa |
| 2006 | Kupambana na usafirishaji haramu wa mtoto |
| 2005 | Haki ya Ulinzi: Acha ukatili dhidi ya watoto |
| 2004 | Yatima wa Afrika: Jukumu letu sote |
| 2003 | Mtoto wa Afrika na familia |
| 2002 | Haki ya kusajiliwa wakati wa kuzaliwa |

## Kuimarisha miundo ya taasisi

Pia Kamati imeendelea kufanya kazi kuboresha muundo wake wa taasisi. Kufanya kazi na Sekretarieti ndogo, Kamati imeweza kuandaa:

- Kanuni za Utaratibu (2003), ambazo kwa sasa zinapitiwa
- Mwongozo kwa ajili ya Ripoti za Awali za Nchi Wanachama (2003)
- Mwongozo wa Uzingatiaji wa Mawasiliano yaliyotolewa kwa ajili ya ibara ya 44 ya Mkataba (2014)
- Mwongozo wa Kamati wa kufanya Uchunguzi (2006)
- Mwongozo wa Vigezo vya Kutoa Hadhi ya Uangalizi katika Kamati kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jumuiya (2006).

## Athari za Mkataba wa Afrika wa Watoto kwenye sheria za ndani ya nchi

### Fasili ya mtoto

Baadhi ya juhudi za marekebisho ya sheria katika Afrika zinaonyesha athari za Mkataba wa Afrika wa Watoto katika zoezi la kuweka viwango katika ngazi ya kitaifa. Katiba za Afrika Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sheria ya Haki za Mtoto ya Nigeria na ya Kenya zote zinafata fasili ya mtoto ya Mkataba wa Watoto.

### Maslahi bora ya mtoto

Baadhi ya nchi za Afrika zimechukua 'zingatio la msingi' fungu la maneno la kanuni, kwa mfano, Katiba ya Ethiopia, Sheria ya Haki za Mtoto ya Nigeria, Sheria ya Ulinzi na Ustawi wa Mtoto ya Lesotho. Vilevile, nchi ya Somali japokuwa haijaridhia Mkataba wa watoto, Sheria yake ya Haki za Watoto ya mwaka 2007 pia inarudia kanuni hiyo kwa maneno yanayofanana.

### Utamaduni wenye madhara

Baadhi ya nchi katika bara la Afrika zinakataza mila zenye madhara ambavyo vinajumuisha ukeketaji wa wanawake. Kwa mfano Sheria ya Watoto ya Afrika Kusini na ya Kenya, na Katiba ya Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Malagalasi imepitisha Sheria ya Ndoa inayokataza ndoa za utotoni, na Kenya na Katiba ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

## Wajibu wa mtoto

Kuna mazingira ya sheria kujumuisha wajibu wa mtoto. Sheria ya Watoto ya Afrika Kusini, ibara ya 16, imeweka msisitizo kwamba 'kila mtoto ana wajibu unaofaa kwa umri wa mtoto na uwezo kwa familia yake, jamii na serikali'. Vilevile, Kifungu cha 40 cha Katiba ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kinaeleza kwamba watoto wana wajibu la kuwasaidia wazazi wao na ibara ya 16 ya Katiba ya Guinea inatoa ujumbe huo huo.

# Bibliografia


Adeola R, Viljoen, F & Makunya, TM 'A commentary on the African Commission's General Comment on the Right to Freedom of Movement and Residence under Article 12(1) of the African Charter on Human and Peoples' Rights' (2021) 65 *Journal of African Law* 139

Adjolohoun, SH 'A crisis of design and judicial practice? Curbing state disengagement from the African Court on Human and Peoples' Rights' (2020) 20 *African Human Rights Law Journal* 1

Adjolohoun, SH 'Les grands silences jurisprudentiels de la Cour africaine des droits de l'homme et des peuples' (2018) 2 *Annuaire africain des droits de l'homme* 24

Adjolohoun, SH & Oré, S 'Entre imperium illimité et decidendi timoré: la réparation devant la Cour africaine des droits de l'homme et des peuples' (2019) 3 *Annuaire africain des droits de l'homme* 318

Ankumah, E (1996) *The African Commission on Human and Peoples' Rights: practice and procedures* The Hague: Martinus Nijhoff

Ayeni, VO (2016) *The impact of the African Charter and the Maputo Protocol in selected African states* Pretoria: Pretoria University Law Press

Anyangwe, C 'The normative power of the right to self-determination under the African Charter and the principle of territorial integrity: competing values of human dignity and system stability' (2018) 2 *African Human Rights Yearbook* 47

Baldé, A 'O direito ao desenvolvimento como um direito fundamental: a sua proteção jurídica na União Africana e na ordem jurídica dos Países Africanos de Língua Oficial Portuguesa' (2019) 3 *African Human Rights Yearbook* 49-70

Banda, F 'Blazing a trail: the African Protocol on women's rights comes into force' (2006) 50 *Journal of African Law* 72

Baricako, G 'La mise en œuvre des décisions de la Commission africaine des droits de l'homme et des peuples par les autorités nationales' in JF Flauss & E Lambert-Abdelgawad (eds) (2004) *L'application nationale de la Charte africaine des droits de l'homme et des peuples* Bruxelles: Bruylant

Bahoze, OB 'Le système africain des droits de l'homme face à l'état d'urgence sanitaire due à la Covid-19' (2020) 4 *Annuaire africain des droits de l'homme* 60

Ben Achour, R 'Les Protocoles normatifs à la Charte africaine des droits de l'homme et des peuples' (2020) 4 *Annuaire africain des droits de l'homme* 83

Bekker, G 'The African Court on Human and Peoples' Rights: safeguarding the interests of African states' (2007) 51 *Journal of African Law* 151

Biegon, J 'Diffusing Tension, Building Trust: Proposals on Guiding Principles Applicable during Consideration of the Activity Reports of the African Commission on Human and Peoples' Rights' (2018) *Policy paper*

Biegon, J & Killander, M 'Human rights developments in the African Union during 2009' (2010) 10 *African Human Rights Law Journal* 212

Boshoff, E 'Protecting the African child in a changing climate: are our existing safeguards adequate?' (2017) 1 *African Human Rights Yearbook* 23

Durojaye, E & Murungi, LN 'The African Women's Protocol and sexual rights' (2014) 18 *The International Journal of Human Rights* 881

Dzesseu, SFM 'Le temps du procès et la sécurité juridique des requérants dans la procédure devant la Cour africaine des droits de l'homme et des peuples' (2019) 3 *Annuaire africain des droits de l'homme* 72

Evans, M & Murray, R (eds) (2006) *The African Charter on Human and Peoples' Rights – The System in Practice 1986 - 2006* Cambridge: Cambridge University Press

Heyns, C & Killander, M (2009) 'The African regional human rights system' in Gomez Isa & de Feyter (eds) *International human rights law in a global context* Bilbao: University of Deusto

Heyns, C & Killander, M (eds) (2013) *Compendium of key human rights documents of the African Union* Pretoria: Pretoria University Law Press

Heyns, C & Stefiszyn, K (2006) *Human rights, peace and justice in Africa: a reader* Pretoria: Pretoria University Law Press

Heyns, C & Van der Linde, M (eds) (2004) *Human Rights Law in Africa* Leiden: Martinus Nijhoff

Kamto, M 'L'application nationale de la Charte africaine des droits de l'homme et des peuples: articulations respectives' in J-F Flauss & E Lambert- Abdelgawad (eds) (2004) *L'application nationale de la Charte africaine des droits de l'homme et des peuples* Bruxelles: Bruylant

Kéké, S 'L'exercice de la compétence contentieuse de la Cour africaine des droits de l'homme et des peuples à l'épreuve de la souveraineté des États' (2018) 2 *Annuaire africain des droits de l'homme* 154

Killander, M & Abebe, A 'Human rights developments in the African Union during 2010 and 2011' (2012) 12 *African Human Rights Law Journal* 199

Killander, M 'African human rights law in theory and practice' in Joseph, SL & MacBeth, A (eds) (2010) *Research handbook on human rights* Cheltenham: Edward Elgar 388

Lloyd, A & Murray, R 'Institutions with responsibility for human rights protection under the African Union' (2004) 48 *Journal of African Law* 165

Makunya, T and Zigashane, S 'La compétence consultative de la Cour africaine des droits de l'homme et des peuples: entre restrictions organiques et limitations matérielles' in Bakama, EP and Makaya, S (eds) (2020) *Droit international des droits de l'homme, justice transitionnelle et droit international pénal* (Editions CAD)

Manby, B 'The African Union, NEPAD, and human rights: The missing agenda' (2004) 26 *Human Rights Quarterly* 983

Mandlate, AC 'A protecção dos direitos humanos na perspectiva da Carta Africana e seus mecanismos de monitorização' in da Silva, JM & Hostmaelingen, N (eds) *Sistemas Internacionais e Nacionais de Direitos Humanos* (2017) 31

Mbaye, K (1992) *Les droits de l'homme en Afrique* Paris: Pédone

Mezmur, BD 'Happy 18th birthday to the African Children's Charter: not counting its days but making its days count' (2017) 1 *African Human Rights Yearbook* 125

Mezmur, BD 'The African Children's Charter versus the UN Convention on the Rights of the Child: a zero sum game?' (2008) 23 *SA Publiekreg/Public Law* 14

Mubiala, M (2005) *Le Système régional africain de protection des droits de l'homme* Bruxelles: Bruylant

Mugwanya, GW (2003) *Human rights in Africa: enhancing human rights through the African regional human rights system* Ardsley, NY: Transnational publishers

Murray, R, Long, D, Ayeni, V, Somé, A 'Monitoring implementation of the decisions and judgments of the African Commission and Court on Human and Peoples' Rights' (2017) 1 *African Human Rights Yearbook* 150

Murray, R & Long, D (2015) *The implementation of the findings of the African Commission on Human and Peoples' Rights* Cambridge: Cambridge University Press

Murray, R (2000) *The African Commission on Human and Peoples' Rights and International Law* Oxford: Hart

Murray, R (2004) *Human Rights in Africa: from the OAU to the African Union* Cambridge: Cambridge University Press

Musila, GM 'The right to an effective remedy under the African Charter on Human and Peoples' Rights' (2006) 6 *African Human Rights Law Journal* 442

Mutua, M 'The African Human Rights Court: a two-legged stool?' (1999) 21 *Human Rights Quarterly* 342

Nabaneh, Satang '2020 in review: a focus on the African Commission on Human and Peoples' Rights' (2021) https://achprindependence.org/wp-content/uploads/2021/04/2020_ACHPR-Review_ENG.pdf (last accessed 2 June 2021)

Nabaneh, Satang 'Maintaining the independence of the African Commission on Human and Peoples' Rights: A commentary on the Rules of Procedure, 2020' (2020), *Technical Report, Coalition for the Independence of the African Commission*

Nkhata, MJ 'A bundle of mystery? Unpacking the application of the 'bundle of rights and guarantees' in the admissibility of applications before the African Court on Human and Peoples' Rights' (2020) 4 *African Human Rights Yearbook* 192

Nmehielle, VOO (2001) *The African human rights system: its laws, practice, and institutions* The Hague: Martinus Nijhoff

Okafor, OC (2007) *The African human rights system: activist forces and international institutions* Cambridge: Cambridge University Press

Onoria, H 'The African Commission on Human and Peoples' Rights and the exhaustion of local remedies under the African Charter' (2003) 3 *African Human Rights Law Journal* 1

Österdahl I (2002) *Implementing human rights in Africa* Uppsala: Iustus Förlag

Ouguergouz, F (2003) T*he African Charter on Human and Peoples' Rights: a comprehensive agenda for human rights* The Hague: Kluwer Law International

Quashigah, K 'The African Charter on Human and Peoples' Rights: towards a more effective reporting mechanism' (2002) 2 *African Human Rights Law Journal* 261

Rudman, A 'The protection against discrimination based on sexual orientation under the African human rights system' (2015) 15 *African Human Rights Law Journal* 1

Sègnonna Horace Adjolohoun (2020) 'A crisis of design and judicial practice? Curbing state disengagement from the African Court on Human and Peoples' Rights' 20 *African Human Rights Law Journal* 1

Sloth-Nielsen, J & Mezmur, BD 'A dutiful child: the implications of article 31 of the African Children's Charter' (2008) 52 *Journal of African Law* 159

Sloth-Nielsen, J (ed) (2008) *Children's rights in Africa: A legal perspective* England: Ashgate Publishing Limited

Sloth-Nielsen, J 'Children's rights litigation in the African region: lessons from the communications procedure under the ACRWC' in T Liefaard & J Doek (eds) (2015) *Litigating the rights of the child* Netherlands: Springer

Ssenyonjo, M (ed) (2012) *The African regional human rights system* Leiden: Martinus Nijhoff

Stefiszyn, K 'The African Union: challenges and opportunities for women' (2005) *African Human Rights Law Journal* 358

Umozurike, O (1997) *The African Charter on Human and Peoples' Rights* The Hague: Kluwer Law International

Van der Linde, M & Louw, L 'Considering the interpretation and implementation of article 24 of the African Charter on Human and Peoples' Rights in light of the SERAC communication' (2003) 3 *African Human Rights Law Journal* 167

Van der Mei, AP 'The advisory jurisdiction of the African Court on Human and Peoples' Rights' (2005) 5 *African Human Rights Law Journal* 27

Viljoen F 'Understanding and overcoming challenges in accessing the African Court on Human and Peoples' Rights' (2018) 67 *International and Comparative Law Quarterly*

Viljoen, F & Louw, L 'State compliance with the recommendations of the African Commission on Human and Peoples' Rights, 1993-2004' (2007) 101 *American Journal of International Law* 1

Viljoen, F & Louw, L 'Status of the findings of the African Commission on Human and Peoples' Rights' (2004) 48 *Journal of African Law* 1

Viljoen, F 'A human rights court for Africa, and Africans' (2004) 1 *Brooklyn Journal of International Law* 30

Viljoen, F 'From a cat into a lion? An overview of the progress and challenges of the African human right system at the African Commission's 25 year mark' (2013) 17 *Law, Democracy & Development* 298

Viljoen, F 'Promising profiles: an interview with the four new members of the African Commission on Human and Peoples' Rights' (2006) 6 *African Human Rights Law Journal* 237

Viljoen, F 'The African Charter on Human and Peoples' Rights: the travaux préparatoires in the light of subsequent practice' (2004) 25 *Human Rights Law Journal* 313

Viljoen, F 'The Special Rapporteur on Prisons and Conditions of Detention in Africa: achievements and possibilities' (2005) 27 *Human Rights Quarterly* 125

Viljoen, F *International human rights law in Africa* (2012) Oxford: Oxford University Press

Wachira, GM & Ayinla, A 'Twenty years of elusive enforcement of the recommendations of the African Commission on Human and Peoples' Rights: A possible remedy' (2006) 6 *African Human Rights Law Journal* 465

UNESCO 'African Court's Landmark Decisions Ensure Prosecution of Crimes against Journalists' Part of a series of interviews with judges, prosecutors and legal experts from around the world in order to showcase good practices to #EndImpunity for Crimes against journalists and #ProtectJournalists' (12 March 2021) https://en.unesco.org/news/african-courts-landmark-decisions-ensure-prosecution-crimes-against-journalists (accessed 29 May 2021)

Zarifis, IN 'The settlement option: friend or foe to human rights protection in Africa?' (2019) 3 *African Human Rights Yearbook* 221